# TAMAA NA ATHARI ZAKE KATIKA JAMII: ULINGANISHI WA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO*

**NA**

**THOMAS OTIENO AKONG'O**

**C50/89938/2016**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA KISWAHILI**

**31 JANUARI, 2022**

## UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJAWAHI KUTOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE

THOMAS OTIENO AKONG'O

SAHIHI ____________________ TAREHE 5/3/2022

(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

WASIMAMIZI

PROF. K. W. WAMITILA

SAHIHI ____________________ TAREHE 06/03/2022

DKT. AMIRI SWALEH

SAHIHI ____________________ TAREHE 06/03/2022

# TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa aila yangu: mama wangu mpendwa, Esther Kabeyeka MMbone, dadake, Sister Geraldine Musimbi, mwanangu Esther Geraldine (Suluhu Samia) na dada yangu Janet Atieno.

## SHUKRANI

Ninashukuru Maulana kunijalia tangu kuanza kozi hii hadi kunifikisha pahali nilipo. Natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. Wamitila na Dkt. Swaleh kwa uongozi na ushauri wao katika kila hatua ya utafiti huu. Mola azidi kuwanyunyizia baraka na maarifa.

Pia natoa shukrani nyingi kwa wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili (UoN) kwa kunifunza, kunishauri na kunielekeza kila nilipohitaji msaada wao. Hawa ni pamoja na Prof. Iribemwangi, Prof. Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Zaja Ombogo, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Mbuthia, Prof. Rayya Timammy, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Sanja na wengine wote, Mungu awabariki.

Tena ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa kunitia moyo na kushiriki vyema mijadala iliyonisaidia pakubwa. Hawa ni Violet Anindo, Agness Mueni, Ruth Nzambi, Obwogi, Ann miongoni mwa wengine. Mungu awabariki.

Napenda kutoa shukrani za pekee kwa binti yangu Princess Esther Geraldine ( Suluhu Samia) na mamake Faith Atieno, mamangu Esther Kabeyeka na shangazi Mtawa Geraldine Musimbi kwa kuvumilia nilipokuwa masomoni na pia kunihimiza kutia bidii ili nihitimishe safari hii ya masomo.

Ninawashukuru marafiki wote kama Steven Kimanzi (Mwalimu wa Shurie Boys) na wengine waliochangia kufanikisha utafiti huu. Maulana azidi kuwaangazia neema zake.

# MUHTASARI

Katika tasnifu hii, tumeshughulikia tamaa na athari zake katika jamii: ulinganishi wa *Ua la Faraja* ya W. E. Mkufya (2008) na *Paradiso* ya J. Habwe (2014). Tumetumia nadharia ya maadili kuhakiki kazi hizi. Tasnifu hii yetu ina sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumeeleza sehemu kama usuli wa utafiti, sababu za kushughulikia mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, maswali ya utafitii, malengo ya utafiti, tatizo la utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia ya maadili iliyotumiwa kuhakiki kazi hizi na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili, tumeshughulikia lengo la kwanza, namna dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa katika riwaya hizi Katika sura ya tatu tumebainisha athari zinazotokana na tamaa na ambazo zinaikumba jamii katika kazi hizi mbili. Vilevile, katika sura ya nne, tumebainisha ushauri uliopendekezwa katika riwaya zote mbili ili kukabiliana na tamaa na athari zake katika jamii. Sura ya tano inaeleza kuhusu matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo kuhusu utafiti huu. Mwisho kuna marejeleo ya utafiti huu.

## YALIYOMO

KURASA

**UNGAMO** .......... **i**

**TABARUKU** .......... **ii**

**SHUKRANI** .......... **iii**

**MUHTASARI** .......... **iv**

**YALIYOMO** .......... **v**

**SURA YA KWANZA**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .......... 2

1.3 Maswali ya Utafiti .......... 2

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 3

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......... 3

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 4

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada .......... 5

1.8 Msingi wa Kinadharia .......... 8

1.9 Mbinu za Utafiti .......... 17

1.10 Hitimisho .......... 17

**SURA YA PILI**

**UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA DHAMIRA YA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO***

2.0 Utangulizi .......... 18

2.1 Aina za Wahusika .......... 18

2.2 Wahusika Wakuu katika *Ua la Faraja* .......... 18

2.2.1 Uteuzi wa Ngoma kama Baba Mzazi .......... 19

2.2.2 Uteuzi wa Tabu Kama Mama Mzazi ........ 21
2.2.3 Uteuzi wa Queen ........ 24
2.2.4 Uteuzi wa Omolo kama Mwanamume Mwenye Mlahaka Mwema ........ 26
2.2.5 Grace dadake Tabu ........ 30
2.2.6 Daktari Hans kama kielelezo cha matumaini mma ........ 31
2.3.0 Wahusika wasaidizi katika *Ua la Faraja* ........ 32
2.3.1 Mhusika Mpemba kama mtu mwenye kueneza Uvumi ........ 33
2.3.2 Wahusika Chiku na Pendo kama Wasaka Mapenzi ........ 33
2.3.3 Juma kama mwana wa Ngoma na Tabu ........ 34
2.3.4 Mhusika Asha kama kahaba ........ 36
2.4.0 Wahusika wakuu katika *Paradiso* ........ 37
2.4.1 Michael kama Mhubiri mzinzi ........ 37
2.4.2 Mango kama Mhubiri mwenye tamaa ........ 39
2.4.3 Lydia kama Mwanamke Mvumilivu ........ 40
2.4.4 Patricia kama Msomi mwenye tamaa ya Mapenzi ........ 41
2.5.0 Wahusika wasaidizi katika *Paradiso* ........ 43
2.5.1 Apondi kama mwenye bidii ........ 43
2.5.2 Musa Bosire kama Mchungaji Mzinifu ........ 43
2.5.3 Salome kama Mshiriki Mzinzi ........ 44
2.5.4 Washiriki wa Budalangi Church of God kama Walafi ........ 45
2.5.5 Chifu Mohamed Owaki kama Mtumishi Mlafi ........ 46
2.6 Matumizi ya Lugha-/ Mbinu za uandishi/ Kunga nyingine Katika *Ua la Faraja* ........ 47
2.6.1 Mbinu ya Majazi na suala la maadili ........ 47
2.6.2 Mbinu ya urudiaji na dhamira ya tamaa na maadili ........ 48
2.6.3 Uzungumzi nafsi ........ 53

2.7 Matumizi ya Mbinu za Uandishi -/ Lugha/ Kunga nyingine Katika *Paradiso* ....................... 54

2.7.1 Mbinu ya urudiaji na dhamira ya tamaa na maadili ....................................................... 54

2.7.2 Matumizi ya Uzungumzi nafsi ........................................................................................ 58

2.7.3 Matumizi ya Ishara ......................................................................................................... 59

2.8 Hitimisho ............................................................................................................................. 59

**SURA YA TATU**

**MATATIZO YANAYOSABABISHWA NA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO***

3.0 Utangulizi ........................................................................................................................... 61

3.1 Tamaa na Matatizo yake katika *Ua la Faraja* na *Paradiso* .................................................. 61

3.1.1 Matatizo ya Ulevi katika Familia ..................................................................................... 61

3.1.2 Matatizo ya Udanganyifu na Kusambaratika kwa familia .............................................. 65

3.1.3 Matatizo yanayotokana na Ulafi ..................................................................................... 67

3.1.4 Matatizo ya Uzinzi katika familia na jamii ..................................................................... 70

3.1.5 Matatizo ya Pesa na Anasa ............................................................................................. 75

3.1.6 Matatizo Katika Ndoa .................................................................................................... 76

3.1.7 Matatizo ya Uongozi ...................................................................................................... 82

3.1.8 Ushindani kati ya Usasa na Ukale .................................................................................. 85

3.1.9 Matatizo ya Mali / Pesa na Tamaa .................................................................................. 89

3.2 Dini na Anasa ...................................................................................................................... 92

3.2.1 Mapenzi na Wivu ............................................................................................................ 94

3.3 Hitimisho ............................................................................................................................. 96

**SURA YA NNE**

**USHAURI DHIDI YA ATHARI ZA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO***

4.0 Utangulizi ........................................................................................................................... 97

4.1 Ushauri Dhidi ya Tamaa na athari zake katika *Ua la Faraja* ................................................ 97

4.1.1 Ukweli kuhusu Ugonjwa Hatari wa Ukimwi ........ 97
4.1.2 Tahadhari Dhidi ya Ugonjwa wa Ukimwi ........ 98
4.1.3 Ushirikiano ........ 99
4.1.4 Kutopoteza Matumaini Maishani ........ 101
4.1.5 Mipango katika Maisha ........ 102
4.1.6 Kutowambukiza watu wengine Virusi vya Ukimwi ........ 103
4.1.7 Kutokuwa na Tamaa ya Pesa / Mali ........ 104
4.1.8 Kuwasaidia Mayatima ........ 105
4.1.9 Kukiri Makosa na Kuomba Msamaha ........ 106
4.2 Ushauri Dhidi ya Tamaa na athari zake Katika *Paradiso* ........ 107
4.2.1 Ushauri / Nasaha ........ 107
4.2.2 Matumizi ya Wahusika wa Kitanzia ........ 108
4.2.3 Ushirikiano Katika Jamii ........ 110
4.2.4 Umuhimu wa Uvumilivu ........ 110
4.2.5 Umuhimu wa Maombi/ Sala ........ 111
4.2.6 Kukiri Makosa na Kuomba Msamaha ........ 112
4.3 Hitimisho ........ 114

**SURA YA TANO**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi ........ 115
5.1 Matokeo ........ 115
5.2 Muhtasari ........ 116
5.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........ 117
MAREJELEO ........ 118

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Tamaa imehusishwa na mwanadamu kwa kipindi kirefu. Tamaa kama dhana inafafanuliwa kama hali ya kutaka sana kitu, kuwa na hamu; matamanio ya kitu ama jambo; matumaini ya kupata jambo au kitu. Mwanadamu, amekuwa na hali hii ya uchu ya kutaka kitu kwa sababu ya tamaa. Kati ya vitu mtu anavyoweza kuvitamani ni chakula, pesa, mali, mapenzi na kadhalika. Mtu hutamani kwa kuwa ana lengo fulani, aidha anaweza kutamani kwa kuwa ana msukumo wa kupata usiokuwa na mipaka. Msukumo wa kulimbika au kuhodhi vitu kwa mfano, huchochewa na mazingira, jamii au saikolojia.

Kuna kutaka kwa aina mbili: kutaka vitu ambavyo ni vya kawaida pasi na kutawaliwa na uroho na kule kutawaliwa na uroho/ ulafi. Kutaka kwa kawaida ni ile hali ya mtu kuwa hana kitu au anacho lakini anatamani kupata kingine kwa njia ya haki ambayo inakubalika kulingana na kanuni, maadili na matarajio ya jamii. Kulingana na hali ya namna hii, jamii hufaidi. Kwa upande mwingine, mtu anapotafuta kile akitakacho kwa njia isiyokuwa halali na kutotosheka na kile alichonacho, basi husababisha matokeo hasi katika jamii. Hali kama hii hutawaliwa na uroho na kutojali mbinu anazozitumia ili kufikia malengo yake. Tamaa ya namna hii huweza kumfanya mtu kutenda kila aina ya uozo katika jamii ilmuradi amekidhi mahitaji yake. Vitendo hivi basi, huifanya jamii kuathirika pakubwa kwa njia hasi. Uasherati kwa mfano, humfanya mtu kutumia pesa nyingi na hatimaye mtu husahau kutekeleza miradi, majukumu na wajibu wake muhimu maishani. Kama ni mwanamke, huenda akaendeleza uovu wa kuwa kahaba kwa lengo la kupata pesa. Hali ya kujihusisha na anasa kama uzinzi, husababisha vifo vya mapema na kuacha miradi isiyokamilika.

Utafiti huu kwa hivyo, umechunguza jinsi waandishi hawa wawili, W. E. Mkufya katika *Ua la Faraja* na J. Habwe katika *Paradiso*, wamelishughulikia mada ya tamaa na athari zake katika jamii.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia suala la tamaa na athari zake katika *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Kutokana na maandishi, tasnifu na makala za kitaaluma tuliyoyapitia, imebainika kuwa tatizo hili halijashughulikiwa. Utafiti huu, umechunguza na kubainisha tamaa na aina zake katika jamii zinazosawiriwa na athari za tamaa hizo katika kazi teule. Tamaa husababisha maovu ambayo huwa na athari anuwai katika jamii.

Tanui (2014: 4) anabainisha kwamba tamaa imekuwa tatizo kubwa katika jamii. Tamaa imewasukuma watu kufanya mambo bila kujali matokeo yake. Kupata pesa kwa njia ambayo si halali, kwa mfano, na kuzitumia kwa manufaa yao ya kibinafsi imekuwa kama ibada. Hali hii imeifanya asilimia kubwa ya watu kuathirika pakubwa. Umuhimu wa utafiti huu kuhusu tamaa, umenuia kuihamasisha jamii dhidi ya tamaa na athari zake ili iweze kuipiga vita na kuepukana nayo.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza kwa nini suala la tamaa limebainishwa sana katika kazi hizi kwani wahusika wengi wametawaliwa na tamaa huku wengine wakiathirika nayo. Tamaa inaonekana kukita mizizi katika jamii kwa mfano imewafanya watu kujihusisha na vitendo viovu kama vile unywaji wa pombe kupindukia na ukahaba ambao umesababisha madhara aina aina. Tamaa imewafanya watu katika familia kukosa kuwajibika katika majukumu yao. Baadhi yao wanapata pesa nyingi na kuzitumia vibaya hasa katika anasa iliyo na matokeo hasi kama vile kuambukizwa virusi vya Ukimwi, ugomvi wa kifamilia na mengineo. Vilevile, katika riwaya hizi dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa kwa kutumia mbinu tofautitofauti kama vile uzungumzi nafsi, wahusika, urudiaji na ishara. Mbinu hizi zimetumika ili kutoa taswira kamili ya namna tamaa ilivyoathiri jamii. Kwa msingi huu basi, kuna haja ya kulishughulikia suala hili katika utafiti wa aina hii. Katika kufanya hivyo, utafiti huu umetuwezesha kubaini mwonoulimwengu wa waandishi hawa wawili wanaotoka katika jamii mbili tofauti.

Tamaa katika utafiti huu, imeshughulikiwa kama matamanio au uchu unaomrenga au kumtawala mtu na kumfanya atende mambo yasiyofaa.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

i. Je, dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa vipi katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*?
ii. Je, kuna athari gani zinayotokana na tamaa na ambayo zinaikumba jamii katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*?

iii. Je, riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso* zinapendekeza ushauri upi ili kukabiliana na tamaa na athari zake katika jamii?

**1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu ulilenga:

i. Kuchanganua jinsi dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*.

*ii.* Kubainisha athari zinazotokana na tamaa na ambazo zinaikumba jamii katika *Ua la Faraja* na *Paradiso.*

iii. Kubainisha ushauri uliopendekezwa katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso* ili kukabiliana na tamaa na athari zake katika jamii.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Mada hii ilichaguliwa kufanyiwa utafiti kwa kuwa suala la tamaa limebainishwa zaidi kwenye kazi hizi. Wahusika wengi wametawaliwa na tamaa, huku wengine wakiathirika nayo.

Aidha, kazi hizi kwa kuwa zinafanana katika kuangazia suala la tamaa kama ule wa wahusika wakuu kuwa na tamaa, ulichangia kuchaguliwa kwa mada hii.

Uchambuzi wa kazi hizi mbili ulinuia kuonyesha namna tamaa na athari zake imekita mizizi katika jamii kila upande, iwe ni mjini au mashambani, maabadani na sehemu za starehe, kote watu wanaonekana kuwa na tamaa.

Tumeshughulikia tamaa ili tujue madhara yake katika jamii. Kwa mfano, tamaa ambayo imewafanya watu kujihusisha na vitendo viovu kama vile ukahaba imesababisha madhara ya aina gani. Kwa msingi huu, tumewajibika kuishughuilikia ili watu wapate kufahamu madhara yake na kuchukua tahadhari.

Aidha, tumeshughulikia mada hii kwa kuwa tulitamani kuangalia suala hili kwa kuziangazia kazi hizi za waandishi wawili ambao wanatoka katika jamii tofauti na kuchunguza ni nini hasa katika kazi hizi zilizoteuliwa kutafitiwa ilichangia katika mada ya utafiti huu.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kwamba, utafiti huu utawafaidi wasomaji wa fasihi. Kwa mfano, watakuwa na uelewa kuhusu matatizo ya tamaa na athari zake katika jamii. Hii itawafanya kuchukua tahadhari maishani mwao.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika riwaya mbili za Kiswahili za, W. E. Mkufya, *Ua la Faraja* (2008) na J. Habwe, *Paradiso* (2014). Maudhui yaliyochanganuliwa ni yale yenye uhusiano na tamaa na athari zake katika jamii. Kwa mfano, tamaa ya kupata mali, tamaa ya unywaji wa pombe, tamaa ya uongozi, tamaa ya mapenzi, tamaa ya kufanya ngono na kadhalika. Tumebainisha matatizo ya aina hizi za tamaa na athari zake katika jamii na vilevile ushauri unaoweza kutolewa ili kuzuia matatizo hayo ya tamaa na athari zake katika jamii.

Aidha, tumebainisha namna dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa katika kazi hizi. Utafiti huu umebainisha jinsi waandishi W. E. Mkufya, katika *Ua la Faraja* na J. Habwe, katika *Paradiso* wameyashughulikia maudhui ya tamaa na athari zake katika jamii. Pia tulilenga kufanyia riwaya hizi mbili uchanganuzi ili kujua ni kwa nini suala la tamaa limechimuzwa sana katika kazi hizi.

Vilevile, tumedhamiria kujua ni kwa nini wahusika wakuu kuwa wakawa na tamaa jinsi walivyo. Isitoshe, kwa vile suala la tamaa limerejelewa sana, tumelichunguza ili tujue madhara yake katika jamii na kisha kuihamasisha jamii dhidi ya tamaa na athari zake ili iweze kuipiga vita kisha kuepukana nayo.

Kumekuwepo na uchambuzi wa kazi hizi mbili ili kuonyesha namna tamaa na athari zake imekita mizizi kila sehemu katika jamii, mijini au mashambani, maabadani na sehemu za burudani, kote watu wanatamaa.

Tena, tumechanganua kazi hizi mbili ili tuweze kulinganisha kazi hizi za waandishi wawili ambao wanatoka katika jamii mbili tofauti na namna wamelishughulikia suala la tamaa na kuonyesha madhara yake katika jamii. Kwa mfano, tamaa imewafanya watu kujihusisha na maovu kama vile ukahaba ambao umesababisha madhara ya namna. Ulinganishi huu umetuwezesha kushughulikia mada ya tamaa kwa upevu ili watu wapate kufahamu madhara yake na kuchukua tahadhari.

Aidha, tumechunguza ni nini hasa katika kazi hizi zilizoteuliwa kutafitiwa ilichangia katika mada ya utafiti huu.

### 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Gwako (2014) ametafiti kuhusu swala la maadili kuhusu vijana wa kiume katika tenzi mbili. Tenzi alizotafitia ni za Kijumwa, *Siraji* na S. Robert, *Adili*. Katika utafiti wake ametumia nadharia ya maadili. Kijumwa anamshauri mwanaye Hewala aache kuwa na tamaa. Kwa mfano, anapokula aache kuomba chakula kingi na pia kuramba vidole. Miongoni mwa mambo anayomshauri ni kuwa afanyapo kazi asiwe na tamaa ya kudai ujira mwingi wala asinyakue mali ili amiliki kila kitu. Kwa upande wetu, tulinuia kuchunguza namna tamaa ya kula chakula huwa ni kero kwa jamii na athari zake kwa kuangazia kazi mbili tofauti, *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Katika utafiti wake Gwako ameongozwa na nadharia ya maadili katika kushughulikia tamaa na vipengele kama wahusika, lugha na mtindo. Kwa upande wetu, pia tumetumia nadharia ya maadili kuchunguza tamaa na vipengele vingine kama vile wahusika, mtindo na lugha.

Gwako akiwa tofauti nasi, ameshughulikia utanzu wa ushairi nasi tumeshughulikia riwaya. Tofauti hii imekuwa ya manufaa kwetu kwani imetusaidia kujua ni aina gani ya tamaa inapigwa vita. Kwa kufanya hivi imetuwezesha kupambanua kwa kina tamaa na athari zake kwa jamii.

Tanui (2014) amechunguza kuhusu usawiri wa maudhui ambayo yanatumiwa kufunzia wanafunzi maadili vyuoni. Ametumia nadharia ya mseto ya hisia na uhalisia katika kuchunguza kuhusu maudhui na kati ya maudhui hayo ni tamaa. Tanui, ameelezea tamaa kuwa ni ile hali ya mtu kuwa na hamu ya kitu kama vile mapenzi, cheo na hata chakula. Kwake, jambo kuu aliloangazia ni tamaa ya pesa. Ameonyesha namna mwanafunzi wa chuo kikuu ametawaliwa na tamaa ya pesa zisizotumika kununulia vitu vya kimsingi chuoni na badala yake zikamfanya kuambukizwa virusi vya Ukimwi.

Tamaa ya mali na tamaa ya kuishi katika jiji pia imesawiriwa kama kero. Utafiti huu basi kama wetu, umeshughulikia tamaa kama kipengele cha maudhui. Tumechunguza kuhusu tamaa ya mwanamke kutaka kuolewa na mzee ambaye ni tajiri. Kwa jumla, tumeeleza namna tamaa ya namna hii huwa na athari hasi kwa jamii.

Kanyange (2015), ametafiti kuhusu maudhui ya uadilifu yanayopatikana katika nyimbo za Joseph Ngala. Kati ya nyimbo alizoshughulikia ni 'Fuateni mambo ya Sheria' na 'Mwana Mpotevu'. Katika utafiti wake, ametumia nadharia ya uadilifu iitwayo unufaishaji hasi. Ngala katika wimbo wa Fuateni mambo ya Sheria, anaishauri jamii kuacha kuwa na tamaa kwa mfano ya pesa au mali. Ameelezea maovu ambayo mtu hutenda na humpata kwa sababu ya tamaa. Kwa mfano, kuiba na kisha kufungwa katika gereza. Zaidi ya hayo, ameihamasisha jamii namna ya kudhibiti tamaa yao kwa mfano kuwa wavumilivu na kuonyesha kwamba mali ya kuibwa haina baraka. Katika wimbo wa *Mwana Mpotevu* anaihimiza jamii iache kupapia raha za dunia na badala yake iwe na sifa ya kufanya mambo kwa utaratibu, kwa vile tamaa husababisha uharibifu wa mali. Utafiti wa Kanyange basi, umetusidia sana kwa vile umetuongoza katika kutafiti aina ya maovu wahusika katika kazi hizi teule zilizotafitiwa wametenda kwa sababu ya tamaa tena kubaini mikakati kuhusu baadhi ya matatizo ya tamaa na athari zake katika jamii.

Naye Anyango (2016), ametafiti kuhusu usawiri wa uovu katika riwaya teule *Salamu kutoka Kuzimu* (1984) na *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) za Ben R. Mtobwa. Ametumia nadharia ya maadili ili kufanikisha malengo yake. Katika utafiti wake, amechunguza aina ya tamaa kuhusu mali na uongozi. Ameonyesha namna mali inavyomfanya mtu kutenda mabaya kama vile kuua. Anatoa mfano wa mhusika Waridi kumua mwenzake kwa sababu ya tamaa ya mali. Katika utafiti wake ameshughulikia mauaji kama mfano wa uovu unaosababishwa na tamaa ya mtu.

Basi, tumechunguza maovu mengine yanayosababishwa na mtu anapokuwa na tamaa ya pesa. Utafiti wake ukiwa sawa na wetu, alitumia nadharia ya maadili. Utafiti wake, ulitufaa kujua zaidi namna nadharia hii inapaswa kutumiwa ili kupata kufahamu zaidi kuhusu upotovu wa maadili katika kazi tulizolenga kuzishughulikia.

Kipkemoi (2018), amechunguza simulizi za virusi vya Ukimwi/ zinavyodhihirika kwenye nyimbo za jamii za Kenya kibaadausasa. Anaelezea kuhusu tamaa ambayo imeikumba jamii. Ametaja madhara ya tamaa kama kuharibu ndoa na kadhalika. Amerejelea tamaa ya mapenzi na athari yake

ambayo ni kuambukizwa virusi vya ukimwi. Watu wanaonywa kutahadhari na tamaa ya anasa na starehe kwani husababisha majuto. Ili kufikia malego yake aliweza kuongozwa na nadharia ya baadausasa. Kwa upande wetu pia, tumechunguza namna watu wameathirika na maisha ya usasa hasa anasa na starehe na jinsi imewaletea matatizo. Utafiti huu wao basi, umetufaa kwa kutupa hoja nyingi kuhusu namna tamaa ya mapenzi, anasa na starehe imeweza kusambaratisha ndoa katika jamii hasa kuhusu maisha ya usasa. Aidha, utafiti wao umetusaidia kujua namna ya kufanya ulinganishi wa maudhui katika kazi tulizozitafitia, *Ua la Faraja* na *Paradiso.*

Masoud (2018), ametafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika *Mfadhili*, riwaya ya H. I. Tuwa, akiongozwa na nadharia ya ufeministi wa kiafrika. Katika utafiti wake ameshughulikia vipengele vya tamaa kama vile, matamanio na kujiridhisha kimwili. Ameonyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama chombo cha kuridhisha mapenzi ya kimwili. Mwanamke anatumiwa kama chombo cha starehe. Isitoshe, amemchora mwanamke kama mtu mwenye tamaa ya pesa inayompelekea kuwa msaliti na pia kujiridhisha kimwili. Utafiti huu wake ni sawa na wetu kwa msingi kwamba, ameshughulikia riwaya. Tofauti iliopo baina ya utafiti wake na wetu ni kuwa Masoud amechanganua na kuhakiki riwaya moja ilhali sisi tumetumia riwaya mbili.

Aidha, ametumia nadharia ya ufeministi ya kiafrika nasi tulilenga kutumia nadharia ya maadili. Utafiti wake ulitufaa kwa kuwa, ulituongoza kushughulikia sababu zinazowafanya wanawake kuwa na tamaa ya mwili. Katika utafiti huu tuliwalega wanaume pia ili tujue ni kwa nini wanatawaliwa na tamaa ya mapenzi.

Muthui (2019), ametafiti kuhusu maudhui katika tamthilia za Kiswahili zinazotahiniwa katika shule za upili nchini Kenya, *Mstahiki Meya* na *Kigogo*. Katika utafiti wake ametumia nadharia ya uhalisia. Muthui ameelezea maana ya tamaa kuwa mtu kutaka kitu kupindukia na kuweza kutumia njia ya kila aina ili kukipata. Amesema pia kwamba, tamaa ni mbaya. Kwa mujibu wake, aina hii ya tamaa, hudhulumu watu wengine. Kwa mfano, kuna utekelezaji wa maovu kama vile mauaji, kuwa na tamaa ya mapenzi, kuvunja na kusambaratisha ndoa za watu na kuwa na tamaa ya mali. Tamaa ya aina hii husababisha uongozi mbaya na huwafanya watawaliwa kuchoshwa na kususia uongozi huo. Utafiti wa Muthui kama wetu, ulilenga kushughulikia aina ya tamaa inayosababisha dhuluma katika jamii. Utafiti wake, ulitufaa sana kujua mengi zaidi kuhusu aina ya tamaa na athari zake katika jamii. Tofauti iliopo kati ya utafiti wake na wetu ni kwamba, utafiti wake umechunguza tamaa ya aina mbili, yaani mbaya na nzuri, nasi tumetafiti kuhusu tamaa ya namna moja, yaani

tamaa mbaya. Hali hii ya kushughulikia tamaa kama tendo mbaya, imetuwezesha kuichunguza kwa njia iliyo pevu na kina.

Tofauti nyingine baina ya utafiti wake na wetu ni kuwa, Muthui ametumia tanzu ya tamthilia, nasi tumetumia tanzu ya riwaya. Isitoshe, utafiti wake umeongozwa na nadharia ya uhalisia na wetu umeongozwa na nadharia ya maadili. Tofauti hizi zote zimekuwa za manufaa ili kutuwezesha kubaini ikiwa aina ya tamaa tuliyoichunguza katika tanzu na tofauti imeweza kushughulikiwa vya kutosha katika utafiti wa Muthui.

**1.8 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu ulilenga kuongozwa na nadharia ya maadili kushughulikia tamaa na athari zake katika jamii katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Nadharia hii ilinuia kueleza mambo muhimu ambayo binadamu anafaa kushughulikia katika maisha. Nadharia ya maadili kimsingi huelezea wema. Nadharia ya maadili imetuwezesha kuchunguza dhamira na maadili, na utambulisho wa kimaadili. Kati ya vipengele vimeshughulikiwa vya dhamira ya tamaa ni pamoja na uozo katika jamii, ushauri dhidi ya uozo katika jamii, mtindo yaani lugha, wahusika kama vile wenye sifa nzuri za kuigwa na pia walio na sifa mbaya ya kuepukwa. Tumechunguza uvumilivu katika jamii kama sifa ya maadili, upendo, namna watu huiga tabia na jinsi dhamira ya tamaa ilivyoendelezwa katika kazi zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti. Tulizingatia hoja kuu zifuatazo:

i. Maadili ya jamii hutegemea mahusiano kati ya wanajamii na pia mazingira yao.

ii. Dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga jamii kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii.

iii. Uzuri au ubaya wa kitendo inalingana na jamii.

Waliuweka msingi wa nadharia ya maadili hapo mwanzoni kama vile Plato na Aristotle wanasema kuwa majukumu ya fasihi ni kufichua maovu ambayo yako miongoni mwa jamii na pia kuielekeza jamii kutenda mema huku ikibainisha njia zinazoushinda uovu.

Nadharia hii inaelezea sanaa ya fasihi kama inayotoa mifano bora ya kuigwa na kuziacha potovu. Nadharia hii imetufaa katika kutuelekeza kutambua maovu yapatikanayo miongoni mwa jamii na jinsi ya kuielekeza jamii kutenda mema namna ilivyoonyeshwa katika riwaya hizi mbili zilizoteuliwa kutafitiwa. Katika maelezo haya tuna mhimili kuhusu dhamira ya msanii ambayo ni kuandika kuhusu mambo yanayoijenga jamii kimaadili huku akikemea maovu katika jamii hiyo. Mhimili huu ulitufaa kutambua maadili ambayo waandishi walinuia kuwapitishia wasomaji kupitia kazi zao hizi mbili. Kwa mfano, kuasi ulevi, chuki, tamaa ya ngono, mapenzi nje ya ndoa, tamaa ya mali, ulafi wa chakula na tamaa ya pesa.

Msingi wa baadhi ya mawazo ya nadharia ya maadili ni mawazo ya Plato na Aristotle. Nadharia hii iliasisiwa Ugiriki na mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato. Plato alikuwa mwanafunzi wa Socrates na mwalimu wa Aristotle. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), Plato aliishi kuanzia mwaka wa 427 - 345 KKM. Plato alishikilia kuwa sababu kuu ya fasihi ilikuwa ni kuadilisha. Akasisitiza kwamba endapo fasihi haingeadilisha basi, ilifaa ipigwe marufuku. Wazo la Plato la fasihi isiyoadilisha kupigwa marufuku, ilitusaidia kubaini namna waandishi wa kazi mbili tulizotafitia wanavyoiadilisha jamii kwa kutoa mapendekezo ya ushauri dhidi ya maovu ya tamaa na athari zake.

Katika kitabu *The Republic*, Plato anazungumzia Jamhuri dhahania iliyo kielelezo bora na ambayo ina kiongozi aliye na maadili ya hali ya juu sana. Kulingana na Plato, ili viongozi wasipoteze maadili, wanapaswa kutengwa na maovu. Anapendekeza kulelewa kwa wanaotakiwa kuwa viongozi wa Jamhuri katika mazingira mema ambayo hawawezi kuathiriwa vibaya kimaadili. Anasisitiza kwamba ni sharti shairi kuchunguzwa na kufanyiwa mchujo kabla athari yake kupitishwa kwa jamii. Plato anapendekeza kwamba mtunzi wa kazi anapaswa kuyaeleza mazuri tu yanayohusu majagina pia watawalao nchi.

Baadaye kukaja watalaamu wengine ambao nao waliweza kuendeleza nadharia hii. Hawa ni pamoja na Horace, Aristotle, Tolstoy na Hough. Kuhusu mchango wao kwa mfano, Aristotle aliamini kwamba, binadamu anafaa kuiga matendo mema na kuacha mabaya. Horace kwa upande wake katika andiko la *The Art of Poetry* (1640) aliendeleza mawazo ya Aristotle na kuyafanya kuwa sheria ambazo zilinuiwa kufuatwa na watunzi chipukizi. Alipendekeza kwamba fasihi

lazima iwe na lengo la uadilishaji na usisimuaji. Tolstoy, aliendeleza nadharia ya maadili kwa kupendekeza kwamba, uzuri wote wa sanaa, unategemea maadili ambayo hupokezwa jamii.
Hough, kwa upande wake, alichukulia fasihi ni sawa na utimilifu wa maisha. Jukumu kuu la nadharia hii ni kupendekeza jinsi ya kutatua matatizo ya kijamii. Inafanya hivyo kwa lengo la kujenga jamii bora ambayo ina maelewano yanayotokana na kuchunguza kazi za kifasi, ubinadamu na vilevile masuala yanayohusu maadili. Kwa kutumia nadharia hii, tuliweza kutambua baadhi ya matatizo yanayosababishwa na tamaa na athari zake katika jamii kwenye kazi tulizolenga kushughulikia. Aidha, kipengele cha nadharia hii kinachohusu jukumu la fasihi ni uadilishaji na usisimuaji, umetuwezesha kuchunguza namna kazi tulizodhamiria kutafitia zinavyoadilisha na kuwasisimua wasomaji. Tumezingatia visa vinavyosimuliwa na waandishi na namna walivyovisimulia visa hivyo katika kazi hizi mbili.

Wafula na Njogu (2007: 28), wanasema kuwa Aristotle alisisitiza kwamba, fasihi husawiri kiubunifu kuhusu mambo yaathiriayo maisha ya mtu. Aristotle alisema kwamba, uigizaji waweza ukawa ni wa heri ama wa shari. Kwa mujibu huu, ni shughuli ya jamii kutathmini kwa kuangalia na kuchuja mambo ambayo ni bora kuigwa na kuyapuuza ambayo hayafai. Kufuatana na haya fasihi inachukuliwa kuwa kioo cha jamii.

Kulingana na Carroll (2008: 4), wanafalsafa kuanzia Plato hadi Hume walihisi kwamba mbeko kuhusu sanaa haikuwa tatizo. Katika Karne ya 18 kulikuwa na watalaamu wenye mawazo kwamba, kitengo cha ujumi na kile cha maadili kilikuwa tofauti na huru kutoka kwa kingine. Kabla ya karne ya 18, ujumi na maadili yalikisiwa kuwa kitu kimoja. Kutoka karne ya 18, kukawa na tofauti. Anavyodhani Caroll ni kwamba, makubaliano kuhusu kutengwa kwa dhana hizi mbili ulifanyika baada ya msisitizo uliyotolewa katika kitabu cha I. Kant, *Critique of the Power of Judgement* (1790). Anasema kwamba uamuzi kuhusu hisia huwa haujalishi bali hukumu ya maadili ndiyo huonyesha umuhimu wa fikira halisi. Kuna dhana mbili muhimu zilizotumika katika mjadala wa sanaa na maadili. Hizi ni uhakiki wa maadili na uhakiki wa elimu ujumi. Hata hivyo, dhana hizi zimekuwa zikitumika sawa pasi na kuzitofautishwa. Kulichunguzwa ikiwa maadili inachangia kuwepo kwa ujumi au ni ujumi unachangia kuwepo kwa maadili.

Kulikuwa na uhusiano kati ya nadharia ya ujumi na maadili. Uhusiano huu ni kwamba, kitu kilichukuliwa kuwa kimekamilika, ikiwa kilikuwa kizuri na pia kuwa na maadili. Maadili ilichukuliwa kuwa muhimu kwa vile ilichangia ukamilifu wa kitu. Kwa mfano, Christian Wolf, Alexander Gottlieb Baumgarten, Georg Friedrich Meier, Moses Mendelssohn na Johann Georg Sulzer ni baadhi ya waliozungumza kuhusu nadharia ya ujumi. Neno 'ujumi' lilianzishwa na mwananadharia Baumgarten. Alitumia dhana hii kumaanisha mwitikio wa hisia uliyo wazi na fikra wazi. Alisema kwamba, uzuri wa kitu unahusu ukamilifu wake ikiwa kinaweza kusababisha furaha kwetu kwa kutumia hisia ya fikra ya ukamilifu. Wolf anafafanua ukamilifu kwa njia ya kidhahania tu kama ushirikiano wa sehemu za kifaa na zingine na lengo la kifaa. Anasema kwamba katika sanaa, uwasilishaji ni wa maana kwa kuwa lengo lake kuu ni kule kufananisha kifaa na kile kitu kinachowasilishwa. Hata hivyo, kinachowasilishwa sharti kifanane na kifaa. Kwa hivyo, uhakiki na utimilifu wa kimaadili ni mojawapo wa ukamilifu wa uwasilishaji ambao unaweza kuwasilishwa na sanaa kama hiyo. Kimaadili, umuhimu wa kile kinachowasilishwa kinachangia kwa ukamilifu wa kifaa, na uhakiki wa maadili wa maudhui ya kazi ya sanaa itakuwa sehemu ya uhakiki wa kazi ya sanaa. Kipengele hiki kilikuwa cha manufaa katika kutafitia tabia za wahusika wenye sura nzuri tukilinganisha na maadili yao. Aidha, maelezo ya Wolf kuhusu ukamilifu wa kifaa na uhakiki wa kazi ya sanaa, umetusaidia kuhakiki maadili yanayopatikana katika maudhui katika kazi hizi tulizolenga kutafitia.

Jambo ambalo mwananadharia Baumgarten ametilia mkazo zaidi kuliko Wolf ni kuhusu ukamilifu wa uwasilishaji wenyewe kuliko uwasilishaji wa maudhui wakati alibadili fomyula ya Wolf kwamba, uzuri ni hisia ya kufikiria ukamilifu na kuwa, urembo ni kama ukamilifu wa hisia ya kufikiriwa. Aliweza kutaja kuwa uzuri unahusisha ukamilifu wa uwasilishaji wa sanaa ambao hauhusu tu sifa kama mali, ukweli, uwazi na furaha na maadili. Ameeleza kwa uwazi kwamba sanaa inawasilisha maudhui muhimu ya maadili. Amesisitiza kwamba, chochote kinachoweza kuwa kizuri ni lazima kiwe na uzuri wa ujumi. Aidha, anaongezea kuwa, hakuna kitu kinachoweza kuwa kizuri bila maadili kwani mtu awazapo kuhusu uzuri bila shaka lazima awaze maadili. Kipengele hiki cha mwananadharia Baumgarten yanayopatikana kuhusu kilicho kizuri lazima kiwe na maadili, ilitusaidia kushughulikia maudhui katika kazi tulizolenga kutafitia ikiwa maudhui hayo yana maadili.

Meier (2008:7) anasema kuwa, ili uwasilishaji mzuri upendeze, ni lazima uwe na mali. Kwa mfano, uzuri unaofikiriwa lazima uwasilishe aina nyingi ya vitu katika mfano mmoja na uvutie. Anachukulia uhakiki wa maadili ya kazi ya sanaa kuwa sawa na uhakiki wa namna maudhui yanavyowasilishwa. Kipengele hiki cha Meier, kimetufaa sana kuchunguza namna maudhui katika kazi tulizolenga kuchunguza ilivyowasilishwa kwa kurejelea mbinu za lugha na usimulizi.

Shaftesbury (2008: 13), anasema kwamba, ni kupitia maadili sanaa inaweza kuonyesha mambo mazuri na pia yale maovu. Anapendekeza kwamba, wakati wa kuhakiki sanaa, uzuri wake utawale ule ubaya kuhusiana na maadili. Hata hivyo, anaona kutenganisha uhakiki wa kimaadili kutoka kwa ujumi kama jambo la ziada. Hutcheson sawa na Shaftesbury, anachukulia kwamba uhakiki wa kiujumi usitenganishwe na maadili bali uwe pamoja. Anashikilia kuwa kazi za kisanaa hazipaswi tu kuonyesha mambo yaliyo mazuri kimaadili kutumia vitendo au sifa. Kipengele cha Shaftesbury na Hutcheson kuhusu maadili kupatikana kwa sanaa kwa kuonyesha mambo yaliyo mazuri na pia yale maovu, imetufaa kwa kushughulikia usimulizi wa maudhui yanayohusu mambo mema na maovu katika kazi tulizodhamiria kuchunguza.

Kwa mujibu wa mwanafalsafa Immanuel Kant, kitu kinachodhibiti akili ya mwanadamu ni mwanadamu kuwa na lengo la kutenda mema. Fikra inaamua tendo ambalo ni la kimaadili nalo tendo huchukuliwa ni la kimaadili ikiwa ni lenye mantiki ili kubainisha thamani ya tendo na wala si matokeo ya tendo. Kulingana na Kant, urazini wa mwanadamu ndiyo muhimu na pia chanzo cha hadhi ya mwanadamu kujitawala. Kila mtu ana wajibu wa kimaadili, ya kuheshimu hadhi vilevile thamani yake na ya wenzake. Kant anazungumzia dhana kama uzuri mnato. Anasema kuna aina mbili ya urembo. Urembo uliohuru ambao anasema hauelezei vile kifaa kinafaa kuwa. Urembo mnato, kwa upande mwingine, unaelezea namna kifaa kinafaa kuwa na ukamilifu wake. Anatoa mfano wa mwanadamu kama urembo mnato. Mwanamume, mwanamke na mtoto ni baadhi ya mifano ya urembo mnato wa mwanadamu. Kuna uzuri wa nyumba, mfano wake ni kanisa na kadhalika. Mifano hizi kama vifaa, vinahusishwa na kazi zao. Uzuri wa vifaa unapatikana kutoka kwenye lengo lililokusudiwa la vifaa hivyo. Kwa mfano, kama ni kanisa inafaa itumiwe katika kuabudu. Kwake anachukulia kuwa, kuna tofauti kati ya maadili na ujumi. Hukumu wa kazi ya sanaa hasa kuhusu uzuri, huwa na mchanganyiko wa fikira, sheria na kuelewa. Lengo la sanaa ni kufurahisha. Kant anasisitiza kwamba katika sanaa kuna maudhui ya kimaadili ambapo

hayawezi kuweka mpaka kuhusu jinsi kazi inaweza kuwa na uhuru wa kusisimua nguvu za fikira. Hata hivyo, anashikilia kwamba katika kazi ya sanaa, maudhui yake yawe ya kimaadili. Kant anazungumzia vilevile, masharti kuhusu urembo kama wakilishi la kitu kibovu. Anasema kwamba, kitu kizuri kisiweze kuwakilisha kile kibaya. Maelezo ya Kant kuhusu maudhui ya kimaadili katika sanaa kutokuwa kizuizi cha kuwa na uhuru wa kusisimua fikira, imetufaidi katika kutafiti jinsi waandishi katika kazi mbili tulizolenga kutafitia walikuwa na uhuru wa kuwasilisha maudhui yao. Tumezingatia jinsi waliwachora wahusika katika kazi hizi.

Kando na hayo, anazungumzia maudhui ya kimaadili kama kisababishi cha uvumilivu na utoshelezaji wa kibinafsi. Anatetea kwamba, uhakiki wa aina hii ni vitengo viwili tofauti, yaani maadili na ujumi ukiwa una vifaa sawa. Maudhui ya kimaadili ni muhimu katika kutekeleza wajibu wa kazi ya sanaa. Kwa mujibu huu, kutumia maadili kuhakiki kazi za sanaa, ni kufaulu kuhakiki kazi hizo.

Kwa mujibu wa mwanafalsafa Jean Jacques Rousseau (1755), ni katika maisha ya kawaida mtu huwa mzuri isipokuwa baadaye huja kupotoshwa na jamii ambayo hufikiria kwamba, imestaarabika. Rousseau anaamini kuwa binadamu anafaa kuongozwa na sheria za kiasili zinazochangia binadamu kuwa mwema. Rousseau, anaonelea kuwa, ujumi na maadili ambao hupotosha wanajamii, huwa inategemea maadili ambayo hupitishwa na wanajamii. Kwake la maana katika maisha ya binadamu ni upendo katika familia na huu kwa hakika ndiyo msingi wa furaha. Anasisitiza kwamba kinachompotosha mwanadamu huwa ni jamii.

Aidha, isitoshe ikiwa watu hawaelewi maumbile ya binadamu, basi haki ya kiasili na sheria, haina maana. Watu wanapaswa kuelewa maumbile ya mwanadamu. Katika kitabu chake, Rousseau, *Moral Education* (1762), anasema kwamba, ili mtu aonekane mwema, ni lazima atende mema. Anachukulia kuwa mtu akiwa na maadili ya hali ya juu ni kama mtu kuwa na kipawa. Anachukulia kwamba, lengo kuu la elimu ni kukuza maadili. Mawazo ya mwanafalsafa Rousseau, yametufaa kutuelekeza kushughulikia vipengele kama upendo katika jamii, namna wahusika wanapotoshwa na wenzao na pia anasa, umuhimu wa elimu, mtu mwema ni wa namna gani na umuhimu wa sheria za utamaduni. Kutokana na haya tunapata mhimili, maadili ya jamii hutegemea mahusiano kati ya wanajamii na mazingira yao. Mhimili huu ulitusaidia sana katika uchunguzi tuliodhamiria

kufanya kuhusu namna mtu anaathirika kutokana na mazingira yake na pia watu anaoshirikiana nao.

Kwa mujibu wa Leo Tolstoy (1960), ujumi pamoja na ule uzuri wote ambao ni wa sanaa, unategemea maadili ambayo yanapokezwa wanajamii. Ili sanaa iweze kuwaelekeza watu wawe na tabia njema, Tolstoy anapendekeza kwamba, sanaa inafaa iwe ya kidini. Tolstoy alikuwa na mawazo sawa na ya Plato kwa kumuunga mkono kuishutumu sanaa isiyojenga maadili. Aliweza kusisitiza kwamba, jukumu la sanaa lilipaswa kujenga udugu miongoni mwa watu pasipo na ubaguzi wa namna yoyote kama wa kitabaka. Anachukulia dini kuwa muhimu zaidi kwani huleta umoja baina ya watu ambao wote hukisiwa ni sawa. Wawili hawa, yaani Plato na Tolstoy, wanapendekeza kwamba kupitia sanaa, wanajamii hupata mwono ambao ni wa maisha ya kimaadili. Kulingana na Tolstoy, sanaa iliyo nzuri ni ile inaweza kupitisha ujumbe kwa watu wengi na pia fasihi hiyo ieleweke na kila mtu. Tena sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yale yanahusiana na maadili ya jamii. Anachukulia fasihi kama zao la jamii. Isitoshe, fasihi inaweza kueleweka ikihusishwa na mazingira ambayo ni ya kijamii yanayoizalisha. Hii ni kwa sababu, mwandishi huwa na ufahamu pia huathiriwa na jamii yake ili kuandika yanayoiongoza jamii hiyo. Kwa msingi huu, fasihi huwa kielelezo cha jamii. Ni kutokana na fasihi tunapata kuelewa namna jamii ilivyo. Katika kazi tulizochunguza, tumejua jamii imetawaliwa na tamaa ya namna gani. Maelezo ya Tolstoy kuhusu nadharia ya maadili imetusaidia kuchunguza kazi tunazotafitia vipengele kama utabaka katika jamii, umuhimu wa dini katika jamii na pia mikakati dhidi ya maovu.

Gitobu (2014: 9) akimnukuu Hough (1966) alisema kwamba, nadharia ya kimaadili inatilia mkazo kwamba kanuni za ukamilifu ambao ni wa fasihi ni sawa na utimilifu wa maisha. Aidha, nadharia hii inahusu kiini kilichomo kwenye utendaji ambao ni sawa na usio sawa. Inalenga kuchanganua kilichomo katika vitendo ambavyo huvifanya vitendo hivyo kutokuwa sawa ama kuwa sawa. Fasihi hata hivyo, inamulika jamii nyingi sana ambazo zinatofautiana pakubwa katika dhana ya maadili. Wanaofuata nadharia ya maadili huamini kwamba sanaa inafaa kuyafichua uozo katika jamii na kisha kuielekeza kutenda mema kutumia njia za kulemea maovu. Hough, anachukulia kwamba, sheria iliyo bora katika fasihi huwa pia bora maishani. Gitobu akimnukuu Hough katika kitabu chake *The Moral Theory* (1998), anaeleza kwamba, fasihi ni sharti ihusiane na upeo fulani

wa mwanadamu. Anasema kuwa fasihi sharti iwakilishe taswira ambayo ni ya uhalisia. Anaonelea kwamba, kazi ya fasihi huwa na wahusika walio na mambo mema ambayo yanafaa kuigwa na pia wahusika wenye sifa mbovu za kuepukwa. Anasema kwamba, fasihi ina malighafi ya kutoa uamuzi ambao ni wa kimaadili namna maisha yanavyofanya. Kwa maoni ya Hough, ni kupitia kwa fasihi ambapo wanadamu wanaweza kuwa wadugu. Anachukulia fasihi kuwa na mchango mkubwa katika matendo pia thamani ya binadamu. Kutoka kwa maelezo haya ya Hough, tumeweza kushughulikia vipengele vinavyohusu namna uozo wa jamii umefichuliwa na pia uozo huo kulemewa, wahusika na maadili. Kwa mfano, wahusika walio na mambo mema ya kuigwa na wenye sifa mbovu za kuepukwa pia tumemulika maadili za jamii nyingi tofauti katika kazi tunazolenga kuchunguza. Aidha, kutokana na maelezo ya Gitobu, imetuelekeza kuchunguza dhamira ya fasihi katika kazi tulizolenga kutafitia kwa mfano watu waishi kama wadugu.

Kulingana na Njogu na Chimerah, nadharia hii inajikita kwenye imani kwamba wanadamu pamoja na viumbe wote walio hai, wana sifa ya kitu kiitwacho tabia wasichozaliwa nacho. Mtu hujifunza tabia. Kuna aina mbili za tabia: tabia chanya na hasi. Mtu ataiga tabia mzuri endapo atampata yule wa kumwelekeza kutenda mema ikiwa angali mchanga. Maelezo ya Njogu na Chimerah kuhusu mtu kujifunza tabia ilikuwa ya umuhimu sana hasa kuhusu wahusika watoto namna wanaweza kuiga tabia iliyo chanya na pia hasi. Vilevile tumechunguza kipengele kuhusu uongozi na maadili kwa kuzingatia kiongozi mzuri anastahili kuwa na sifa za aina gani.

Wamitila (2003: 266-267) anasema kwamba, nadharia ya kimaadili hutumiwa kuelezea usomaji wa kifasihi. Kando na kufanya hivyo, pia hutumiwa katika tathmini ya kifasihi kwa msingi wa kuangalia uhusiano wake ambao ni wa ubinadamu vilevile masuala ya kimaadili. Wamitila akirejelea kazi ya Plato, *The Republic* (1960), anapendekeza umuhimu wa kuchunguzwa na kuchujwa kwa ushairi kabla ushairi huo haujapitishwa kwa jamii kwa sababu ya athari zake kwa jamii. Plato pamoja na wafuasi wake waliamini kwamba kazi ya ushairi ni lazima kumtumikia mtu kiroho. Shairi pia ilifaa kumrutubisha mtu vilevile kumfanya awe na uadilifu wa kijamii. Kwa kufanya hivyo, ushairi unaweza kumwelekeza yule anayehusika kuwa mwanajamii mzuri. Kulingana na Wamitila (2003: 55), umuhimu wa fasihi hautoki tu namna inavyosemwa bali kutoka kwa kile kinachosemwa. Fasihi ni kitu kinachohakiki maisha kuhusu mwanadamu. Katika uhakiki, mhakiki anafaa aone jinsi kazi husika inaweza kumfaa msomaji wake kwa kutoa funzo. Kutokana

na maelezo haya ya Wamitila kuhusu nadharia ya maadili, tumenufaika kuchunguza namna maudhui yamewasilishwa katika kazi tulizolenga kutafitia. Kwa mfano, matumizi ya majazi, urudiaji, taswira na jazanda. Isitoshe, tumeshughulikia funzo iliyotolewa kuhusu kazi hizi.

Wafula na Njogu (2007: 28), wanasema kuwa Aristotle alisisitiza kwamba, fasihi husawiri kiubunifu kuhusu mambo yaathiriayo maisha ya mtu. Aristotle anasema kwamba, uigizaji waweza ukawa ni wa heri ama shari. Kwa mujibu huu, ni shughuli ya jamii kutathmini kwa kuangalia na kuchuja mambo ambayo ni bora kuigwa na kuyapuuza ambayo hayafai. Kufuatana na haya, fasihi inachukuliwa kuwa kioo cha jamii.

Kwa mujibu wa Vaughn (2008), maadili huzungumzia imani kuhusu mema na uovu, ubaya ama uzuri. Kulingana naye, katika maadili, imani inahusu mambo kama thamani, hukumu, sheria na kanuni. Vaughn anachukulia kwamba, maadili husaidia kuongoza matendo, kufasili thamana ya mwanadamu na pia sheria zinazomwongoza. Maadili humpa mwanadamu sababu ya kujitambua na pia maadili hujibu maswali ambayo yanahusu namna ya kuishi vizuri. Kwa maoni ya Vaughn, nadharia hii ni maelezo kuhusu kinachofanya tendo lolote lionekane ni zuri au baya. Mchango wa Vaughn hapa kuhusu nadharia ya maadili ni muhimu sana, kwa vile imetusaidia kuhakiki vipengele muhimu kama imani kuhusu mema na uovu, ubaya ama uzuri na pia kinachofanya tendo kuonekana zuri au baya katika kazi tunazotafitia.

Watuha (2011) akimnukuu Timmons (2002), anasema kwamba, kuna madhumuni ya aina mbili muhimu kuhusu nadharia ya maadili kama vile kiutendaji na ya nadharia. Kwanza, nadharia ambayo ni ya maadili ya kiutendaji huhusu utaratibu kama kutambua jambo lilo sawa na lisilo sawa. Kwa upande mwingine, maadili ya kinadharia uhusu kiini ambacho kiko kwenye utendaji ambao ni sawa na pia usio sawa, uzuri ama ubaya wa jambo. Kulingana na Watuha, kila jamii huwa ina kanuni zake zinazoifanya kuchukulia kitendo kuonekana sawa au si sawa. Mchango wa Watuha kuhusu nadharia ya maadili kwamba, kila jamii ina kanuni zake za kuchukulia kitendo kukubalika au kutokubalika, inatupa mhimili kwamba uzuri au ubaya wa kitendo inalingana na jamii. Mhimili huu umekuwa wa maana sana katika kutafiti vitendo vya wahusika katika kazi tulizoshughulikia. Kwa mfano, kwa nini wahusika fulani wanalewa sana, kupenda ngono, wanaume wengine kupenda wanawake wengi, nao wanawake wengine vilevile kupenda kuwa na wanaume wengi na wahusika fulani pia kupenda pesa sana. Utafiti huu kwa hivyo, umeongozwa

na nadharia ya maadili kwa kuzingatia vipengele vilivyopendekezwa kushughulikiwa katika utafiti huu.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti ulihusisha kusoma na kuhakiki matini za *Ua la Faraja* na *Paradiso* maktabani. Kati ya matini zilizosomwa ni pamoja na tasnifu na hasa za uzamili zenye uhusiano na mada hii na riwaya teule. Pia tulisoma kwa uangalifu na kikamilifu nadharia tuliyonuia kutumia. Vilevile , tulipata msaada kutoka kwa wataalamu wa fasihi kuhusu nadharia teule na kazi hizi ili kufanikisha utafiti huu. Maktaba zilizotumiwa ni za Vyuo Vikuu vya Kenyatta na Nairobi. Bila shaka, zote hizi zimetuwezesha kupata data inayotosheleza utafiti huu. Data ilikusanywa, kupangwa, kuchanganuliwa na kuwakilishwa kwa njia ya maandishi.

### 1.10 Hitimisho

Kwa ufupi, utafiti ulilenga kushughulikia aina za tamaa na athari zake katika jamii kwa kutumia mihimili ya nadharia ya maadili. Katika sura hii ya kwanza, tumezungumzia masuala muhimu yaliyoongoza utafiti huu kama vile usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia na mwisho, mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu. Tumebaini kwamba nadharia ya maadili imefaa sana kushughulikia utafiti huu kwani inazungumzia maswala muhimu tunayoshughulikia.

# SURA YA PILI
# UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA DHAMIRA YA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumechunguza namna dhamira ya tamaa ilivyokuzwa na kuendelezwa katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*. Tumechunguza dhamira hiyo kwa kuwaangalia na kuwachanganua wahusika mbalimbali. Tumechunguza wahusika wakuu na wadogo katika kazi hii pamoja na mbinu za uwasilishaji wao ambazo zinafungamana na dhamira ya tamaa tuliyoichunguza katika kazi zinazohusika. Tumefanya hivyo kwa lengo la kutuwezesha kujua baadhi za njia waandishi wa kazi hizi wamezitumia kuwasilisha, kuendeleza na kukuza dhamira ya tamaa.

## 2.1 Aina za Wahusika

Waandishi Mkufya na Habwe wameweza kushughulikia suala la tamaa na athari zake katika jamii kwa kutumia wahusika kuwasilisha jumbe zao. Kazi hii imewachunguza wahusika hao kwa kuwagawa katika matapo kadha. Wasemavyo Njogu na Chimerah (1999: 144), kuna njia nyingi ambazo hutumiwa kuelezea wahusika katika fasihi. Kwa mfano, kuchunguza jinsi wahusika katika kazi ya fasihi fulani walivyosawiriwa na pia wanavyochangia hasa katika uendelezi wa maudhui na dhamira. Watalaamu hawa wametaja kuwepo kwa wahusika kama vile mhusika wa kisaikolojia, mhusika kwezwa, mhusika wa kimapinduzi na mhusika jumui.

Wahusika wanaopatikana katika kazi yoyote ya kifasihi huweza kugawika katika makundi mawili makuu kutegemea dhima na nafasi zao: wahusika wakuu ambao wanachukua nafasi kubwa na kufungamanishwa na masuala yanayozungumziwa kwa upana na wahusika wadogo ambao wanachukua nafasi ndogo japo muhimu katika uendelezaji wa dhamira. Msingi huu unaifungamanisha sehemu hii na inayofuata.

## *2.2* Wahusika Wakuu katika *Ua la Faraja*

Wahusika wanaopatikana katika tapo hili wasemavyo Njogu na Chimerah (1999: 41), ndio wanaitawala hadithi nzima. Kazi yao muhimu ikiwa ni kuisongeza riwaya mbele kwa kuwahusisha na visa kama matendo na migorogoro iliyo muhimu. Ni kutoka kwao basi tunapata dhamira kuu ya mwandishi, msimamo wa mwandishi dhidi ya matukio vilevile maudhui. Ni hawa wahusika

wakuu ndiyo vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia matendo na maneno yao. Wahusika hawa wakuu wanapoingiliana na wahusika wengine, ndio huwa mbinu ya kufafanua dhamira kuu. Kutokana na maelezo haya, tumechunguza *Ua la Faraja*, na tunaweza kusema kwamba, wahusika wakuu ni kama Ngoma, Tabu, Omolo na Grace.

### 2.2.1 Uteuzi wa Ngoma kama Baba Mzazi

Ngoma anapenda anasa sana. Anapenda kubugia kinywaji cha bia hasa katika *Malaika Bar.* Akiwa mlevi, anapenda sana kucheza muziki na vimada wanaofanya kazi katika baa hiyo kwa mfano, Pendo. Anachangamkia anasa kama vile kunywa pombe na tena kuchoma nyama anayoila na vipusa. Kupitia kwa mhusika huyu, dhamira ya tamaa inaendelezwa na kukuzwa. Tamaa ikiwa imemtawala, anajihusisha na uzinzi bila kutumia kinga na kuishia kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa Ukimwi. Anajihusisha na anasa kwa vile ana uwezo/ pesa nyingi. Hata hivyo, pesa zake nyingi haziinufaisha familia yake. Anaitelekeza aila yake na kuifanya kuishi maisha ya ukata. Hali hii gumu inamlazimu mkewe kuanzisha biashara ya genge akisaidiwa na Juma ili kuweza kuikimu familia yake. Tamaa ya ngono inampelekea Ngoma kuambukizwa ugonjwa wa Ukimwi, naye kumwambukiza Tabu. Pia, uvumi unaenea kotekote kuhusu uhusiano kati yake na Queen unaomfanya Tabu kungamua mahusiano yao, unaosababisha kuathirika kwa ndoa ya wawili hawa. Tena, kuna hali ya kukumbwa na simanzi, hali inayomfanya Tabu kugombana na mumewe kila uchao. Ni kutokana na kilio chake anaziteka hisia za dadake, Grace. Baadaye, Ngoma anaugua. Tunaona kuwa, kutokana na hali hii, anatengwa na mke na watoto wake. Ni kutokana na mhusika huyu tunajua kwamba, ukosefu wa maadili humfanya mtu kutorokwa na famila yake anapowahitaji. Vilevile, kuna talaka inayotokea kati yake na mkewe. Tumeona kuwa hata baada ya Ngoma kufanya bidii na kujenga nyumba, kuwa na magari ya kusafirishia abiria na kupata pesa nyingi kila siku, kiasi kikubwa kiliishia katika anasa kama unywaji wa pombe na kuwafurahisha wanawake. Suala hili la tamaa ya anasa linaishia kusababisha shida katika ndoa yake. Matokeo ni kutumia pesa nyingi kujitibu ugonjwa anaoambukizwa na kuhisi maumivi mwilini na hata fedheha. Kwa sababu ya uozo huu, amesawiriwa kama mhusika msababishi wa majuto katika familia yake kwani amemwambukiza Tabu virusi hali ambayo haichukuliwi na wanawe kama tendo la utu. Anaonekana kama mtu anayealika kifo katika boma lake; badala ya kuleta furaha analeta majonzi.

Mwandishi amemtumia mhusika huyu kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake katika jamii kwa kumrejelea katika sehemu kubwa ya riwaya hii. Mwanzo, alipotoka kimaadili,

hakuwa mswalihina lakini katika safari yake ya mwishomwisho, anapoanza kuugua anaanza kuwa mwadilifu na mswalihina. Hii ni ishara tosha kuwa kapoteza matumaini ya kuendelea kuishi katika ulimwengu, alikuwa anajiandaa katika safari yake ya mwisho. Ni tajiri na mfanyibiashara wa magari ya uchukuzi wa abiria. Biashara hii inampa pesa nyingi sana lakini mtaa wa Tandika uliokuwa wa anasa kupindukia ulipata kumshawishi sawa na ulivyowashawishi watu wengine katika sehemu hiyo ili kuogelea katika anasa. Wanajumuika katika *Malaika Bar* kila wakati na kutumia kiasi kikubwa cha pesa. Kama mteja wa sehemu hii ya burudani, anashiriki ulevi ambao ni uraibu wake. Wanakunywa na marafiki kama Rajabu asemavyo mwandishi:

> "Haikuchukua muda Ngoma aliwasili. Ngoma alikuwa mmoja wa washiriki wa Rajabu katika unywaji wao. Alikuwa amekwishalewa kwani aliingia moja kwa moja na kuanza kumpa mkono kila aliyekuwepo, bila kujali kama wanafahamiana au la." (uk. 6).

Kutokana na dondoo hili, tunaona kwamba, Mzee Ngoma alikuwa mlevi kiasi kwamba kupitia kwake mwandishi ameweza kuwasilisha maudhui na kuendeleza dhamira ya madhara ya ulevi. Ana uwezo wa kunywa pombe kila siku kwa vile ana pesa nyingi.

Ni dhahiri kuwa kutokana na mhusika huyu maudhui ya chuki na kuwadharau jerani yanapatikana. Ngoma hana mlahaka mwema na jirani yake. Mfano mzuri ni ule anapompata Omolo katika jumba la burudani, *Malaika Bar*, anawasalimu watu wengine lakini anapomfikia anasita kumpa mkono. Tunapata taswira ya chuki:

> Akamtazama toka juu mpaka chini, kisha akasema,"Ah, hapana, wewe tumeshasalamiana toka jana na juzi." Akapita (uk. 6).

Aidha, ni kutokana na mhusika huyu, dhamira kuhusu tamaa ya wanawake kuwatamani wanaume inapatikana. Mzee Ngoma anazoena sana na warembo kama Pendo na Chiku lakini, anaogopewa na watu wengine. Wanawake hawa wanamzoea na kutumia nafasi hiyo kupunja pesa zake. Akiwa na tamaa ya anasa, pesa zake zinatumiwa vibaya:

> Ngoma alipowafikia wachoma nyama katika ziara yake ya salamu, wakamuuliza, "Mzee tuchome mingapi?" (uk.7).

Ngoma ametumiwa kama kielelezo cha watu wenye pesa na huitumia vibaya katika anasa na kuwafanya watoto wao kukosa malezi ya baba mzazi. Hii ni kwa sababu anaaga dunia baada ya

kuambukizwa ugonjwa na kuwafanya watoto kubaki bila baba wala mama mzazi. Mwandishi anasema:

> "Ngoma alikuwa na kifua kikuu. Aliogopa kuwaambukiza wanawe, akawaruhusu waondoke wakaishi kwa babu yao. Sasa alikuwa kitandani anakohoa na kujutia uhai wake." (uk. 213).

Tamaa ya kunywa pombe sana na kujihusisha na wanawake inamtenganisha Ngoma na watoto wake hasa, Juma. Anamchukia Juma na hata kumlaani. Lakini kutokana na jitihada za Grace na Omolo, anakubali kumsamehe na kumuondolea laana. Katika hatima ya uhai wake anaiacha familia yake ikiwa imeshikamana, hii ni baada ya kufutilia mbali talaka ya mkewe na kuwarithisha wanawe mirathi kwa kuandika wosia. Mkufya ametekeleza yanayosemwa katika mhimili huu kwamba, dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga jamii kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii. Ameonyesha namna uozo wa Ngoma unasababisha matatizo mengi katika jamii. Nadharia hii inakemea maovu kama haya.

Tabia ya Ngoma kuwapenda wanawake wengi inaweza kufananishwa na tabia ya Mango katika riwaya ya *Paradiso.* Mango ana wake wengi wanaomshinda kuwakimu kwa kuwa ana mapato duni. Tofauti kati yake na Ngoma ni kwamba, yeye si mlevi na amewaoa wake kama vile Apondi na Sakina. Ngoma ana mke mmoja halali, Tabu na wengine wengi nje ya ndoa kama vile Queen, Asha, Pendo na Chiku. Hii ni kwa sababu ya tamaa. Tofauti ingine ni hakuna mke wa Mango hata mmoja anayemuambukiza ugonjwa wa zinaa jinsi Queen alivyomuambukiza Ngoma.

### 2.2.2 Uteuzi wa Tabu Kama Mama Mzazi.

Mama huwatunza wanawe kuanzia utotoni hadi umri wafikie wa makamo. Mtoto anapozaliwa, mama humshughulikia pakubwa katika malezi. Ni mama humnyonyesha hadi anapofikia umri wa kula vyakula. Ni kupitia ukaribu wa mama na mtoto, huwafanya kujenga mahusiano ya karibu na mtoto kumpenda. Kwa mujibu huu, Tabu ameteuliwa na mwandishi wa riwaya hii kama mhusika mkuu ambaye ni mzazi wa watoto kama vile Juma, Aisha na Rahma, Abu na Nuru. Yeye ni mke wa Ngoma ambaye amesawiriwa kama mhusika wa kipekee anayeambukizwa virusi vya ukimwi kutoka kwa mumewe bila kuhusika katika anasa ya uzinzi kisha kuteseka anapougua na kutalakiwa. Jina Tabu ni la kimajazi, kumaanisha shida anazopitia mhusika huyu. Anatelekezwa na mumewe; anaamua kuanzisha biashara ya kuuza vitu katika genge ili kuweza kuikimu familia.

Anafanya hivi akisaidiana na mwanawe wa kwanza wa kiume, Juma. Hali inayoathiri masomo ya Juma kwani anachukua muda mwingi kila asubuhi kwenda kumsaidia mamake kuchagua na kununua bidhaa sokoni kisha aelekee shuleni. Kwa mujibu wa Pitcher na Imelda (2004), kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha namna ugavi wa majukumu hufanywa kulingana na jinsia ya mwanajamii. Madai ya wawili hawa yamethibitishwa kwa kumrejelea Hartman (1982) anayesema kuwa jamii huyagawa majukumu kwa kuzingatia utaratibu fulani ambao ni maalumu. Wanaume hufanya kazi kwa staha na zile zinaonekana kuwa duni, huachiwa wanawake. Wanawake hugawiwa majukumu ya nyumbani. Ngoma anamiliki biashara ya hadhi inayomweka katika tabaka la juu. Anapata pesa nyingi ambazo anatumia katika anasa hasa za pombe na uasherati. Kiasi ingine kubwa anaiweka kama akiba. Anasa inamfanya Mzee Ngoma kuitelekeza familia yake hali inayomsukuma na kumlazimisha Tabu kuchukua majukumu ya nyumbani kwa kuanzisha biashara ya genge ambayo ni ya wanawake kwa sababu ni duni. Kutokana na jinsi hali ilivyo, Tabu hawezi kutumia pesa anazopata kununua nguo za maana. Hali hii inamfanya kujiuliza kama kuna umuhimu wa ndoa yao. Ngoma hamtunzi pamoja na wanawe kwani penzi yake kwa Tabu haiko. Vituko hivi vinamfanya kulaani maovu yote yanayopatikana katika ndoa. Tena, anavichukulia vipingamizi vya kijamii vinavyomzuia kutoroka mwanamume kama: utumwa, uonevu na usaliti uliojificha katika asasi ya ndoa:

> Alijiwazia moyoni: "Huyu mume hanipi matunzo wala hawatunzi wanawe. Penzi lake kwangu halipo. Kama tukilala kitandani akinihitaji, inakuwa kama anatimiza wajibu tu, hana mapenzi na mimi... Anarudi amelewa…" (uk.112 – 113).

Tabu ametumiwa na mwandishi kuonyesha namna wanawake katika ndoa huteseka na watoto kwa kutelekezwa na mume hata kama mume huyo ana pesa nyingi. Pesa hizi nyingi huishia katika anasa ambayo husababishia familia majonzi. Kando na kuteseka kwa kutopewa pesa za matumizi, anaambukizwa virusi vya ukimwi. Tunamshuhudia Tabu akinyenyekea na kuuliza:

> "Baba Juma, mbona mambo haya wayauliza leo? Huko nyuma kote Juma na mimi tumekuwa tukisaidiana. Kila asubuhi yeye huamka kutangulia kwenda kuninunulia… Sasa mbona wauliza leo kama ndiyo leo waijua nyumba hii?" (uk. 106).

Tumeona tena kwamba, Tabu ametumiwa kuonyesha namna madhara ya ugonjwa wa mama huwaathiri watoto. Walipogombana, majerani na watoto walisikia. Watoto wanajua wazazi wao hawataishi muda mrefu kabla kuaga dunia na watasalia mayatima.

> “ Siku aliyopata habari, Tabu alilia mchana wote ikiwa amejifungia chumbani. Mume wake alirudi nyumbani saa saba usiku. Ugomvi mkubwa ulizuka na katika zogo hilo, hata majerani wakajua kiini cha mzozo… Hofu ya ukimwi ikahama … watoto” (uk. 32).

Mwandishi anamchukulia kama mvumilivu. Tena ametumiwa kuonyesha ukubalifu wake kuhusu ukweli wa ugonjwa wa ukimwi kwa kuwahudumia wanawe huku akifuata ushauri wa daktari Hans. Anavumilia hadi pale mumewe anapozidiwa na ugonjwa hospitalini. Yeye ni kielelezo cha mapenzi na upendo katika ndoa hata baada ya kukosewa na mumewe kwa kuambukizwa virusi vya ukimwi. Anajitwika majukumu ya kumshughulikia kwa kumletea chakula hospitalini, kumlisha, kumhimiza na kumbembeleza ale. Kwa kufanya hivi, ndoa yao inaonekana kurudi kuwa kawaida kama hapo mwanzo. Hali hii inampelekea Ngoma kumwomba radhi:

> “Nisamehe mke wangu,” alijikusuru kusema na machozi yakatoka tena…
>
> “Jitahidi Baba Juma, angalau kikombe kimoja cha uji au chai,” Tabu alimbembeleza, lakini kwa masikitiko, Ngoma alitingisha kichwa ... (uk. 292).

Tabu pia, ameangaziwa kama mtu wa kutekeleza nafasi muhimu katika kuwahimiza Grace na Omolo kufunga ndoa. Anafanya hivyo siku zake za mwisho akiwa kitandani akiugua. Ni kupitia kwake tunapata hoja muhimu ya watu kuweza kuoana baada ya kupimwa na kuhakikisha wao hawana virusi vya ukimwi. Akiwa anazumgumza kwa shida, anawashikanisha mikono Grace na Omolo. Tendo hili ni ishara ya wao kuhitajika kuishi pamoja kama bwana na bibi. Tabu anatumiwa na mwandishi kuzungumzia maswala ya ndoa kwa wanaotaka kuoa na kuolewa; wahakikishe wamepimwa na hawana virusi vya ukimwi. Anamhimiza Omolo kumuoa dadake Grace kama ishara yake ya kuthamini ndoa na kutahadharisha watu kumakinika wanapotaka kupata jiko:

> “… Omolo. Najua anampenda Grace na wote wamepima, hawana virusi. Wahimize waoane…” “ Grace alipofika karibu na kutaka kumshika

dada yake begani, Tabu akauchukua mkono … (uk. 337- 338).

Hii ilikuwa inaashiria kwamba waoane na waishi pamoja kama bibi na bwana. Na katika ndoa wanapaswa kupendana na kuaminiana. Kupitia kwake, mwandishi anatuarifu umuhimu wa ndoa na mapenzi baina ya wanandoa watarajiwa. Kama tunavyoona nadharia ya maadili, inaeleza sanaa ya fasihi kama inayotoa mifano bora ya kuigwa na kuziacha zile potovu. Nadharia hii imetuwezesha kutambua maovu yapatikanayo miongoni mwa jamii na jinsi ya kuyaondosha. Jamii inapaswa kuasi maovu na kutenda mema.

Tabu ni kama Apondi katika riwaya ya *Paradiso.* Mango anamtelekeza Apondi kwa sababu ya tamaa ya kuwapenda wanawake wengi. Hii inampelekea Apondi kufanya kazi nyingi ngumu tena ya sulubu ili kuikimu familia yake. Kazi ya kuwalimia watu shamba inamsababishia ugonjwa unaomfisha. Chanzo cha Apondi kuwa mgonjwa ni tamaa ya mumewe kuwa na wake wengi kisha kukosa kuwapa mahitaji muhimu kama chakula na mavazi. Tofauti kati yake na Tabu ni kwamba, kifo chake (Apondi) kimesababishwa na ugonjwa tofauti wala si Ukimwi. Kwa hivyo ni mwaadilifu..

### 2.2.3 Uteuzi wa Queen

Queen ni katika wahusika wakuu katika kazi hii. Jina lake ni la kimajazi linalodhihirisha alivyoumbwa na kujirembesha. Yeye ni ‘Malkia’. Anaishi maisha ambayo hayana tabu kwani ana pesa nyingi. Mwanamke akiwa katika hali hii huwavutia wanaume wengi. Queen ana sifa hizo kwa sababu ana elimu na kupata kazi nzuri ya uanasheria katika kampuni fulani. Hii inamwezesha kuwa na pesa nyingi ambazo anazitumia kwa anasa, kununulia ploti na kujengea nyumba ya kifahari. Ana friji, chakula cha bei kama kuku na vileo kama pombe kali ya bei ya juu. Hali yake ya kuwa na pesa nyingi na kuishi maisha ya anasa, inamzubaisha hadi anachelewa kupata jiko na pia kuwa na mwana. Kupenda pesa na anasa inamfanya kuwapenda watu waliokuwa na pesa kama Ngoma. Anashiriki nao katika tendo la ngono bila kinga na hatimaye kuambukizwa virusi vya ugonjwa hatari wa ukimwi. Analimbikiziwa lawama na wengi katika kitongoji cha Tandika kuwa ndiye kamwambukiza Ngoma virusi vya ugonjwa hatari wa ukimwi:

> “Wewe mke wangu, nani kakudanganya kwamba una UKIMWI? Kwani umehakikisha wapi?...”
>
> Hasira zikamjia …Tabu “Kwani hujui? Queen aliyepata *mkanda wa jeshi* juzi …”

(uk. 28).

Baada ya kumwambukiza Ngoma virusi, boma la Mzee Ngoma linaathirika pakubwa. Kwa mfano, Ngoma na Tabu wanashikwa na hofu na kunakuwa na malumbano na migogoro. Unapofika wakati wa kuonana kimwili, Ngoma anataka watumie kondomu, tendo ambalo hawajazoea. Hii inawafanya kukosa kulifurahia na kulichangamkia ngono.

Kwa sababu Queen hajaolewa na ana pesa nyingi, anazuru majumba ya starehe na burudani kama *Malaika Bar*. Hapa anakunywa pombe, anacheza densi na kuwapata wanaume ambao wanammezea mate na kisha kushiriki nao ngono. Tabia ya Queen inaelekea kukiuka mazoea ya jamii nyingi kuwa yeye hafungwi na itikadi na imani kuwa mwanamume ndiye anayepaswa kumwandama mwanamke na kwa kiasi kikubwa anaakisi mtazamo unaohusishwa na jamii za kisasa na ambao labda baadhi ya wanajamii huenda wakauona kama unaokwenda kinyume na maadili waliyoyazoea. Hafungwi na itikadi hii, basi anawaandama wanaume kama Omolo na kuwakaribisha kwake kwa vileo na kisha kuwalaghai kushiriki tendo la mapenzi. Anaishia kuugua kutokana na Ukimwi. Akiwa katika hali hii, hana wa kumtegemea isipokuwa Omolo. Kwa mfano, anamtafutia mfanyikazi wa nyumbani na pia kuwafikishia wazazi wake ujumbe kumhusu kule Mwanza, Tanzania. Kuna taswira ya kutorokwa na watu wa karibu na uenezaji uvumi kumhusu na kuchekwa, hii ni baada ya kulemewa na makali ya ugonjwa. Makali ya ukimwi unamfanya kumtumia Omolo kwa kila jambo. Mathalan, kumpelekea mamake ujumbe kumhusu na kisha kuja naye hadi Tandika. Tunaelezwa:

> "Kila mgonjwa huhitaji dawa, lakini ukishaambiwa ugonjwa huu hauna tiba sasa unakunywa dawa za nini?… "Ah, si ujinga tu! Mimi, kusema kweli, mama angeweza kuja nikampa maagizo yote na kumkabidhi nyumba, najiondoa …" (uk.139-141).

Tumeona kwamba Queen, alipokaribia kujitoa uhai, siku hiyo alikuwa na furaha ghaya. Anafanya sherehe ambapo ananunua pombe, soda na pia nyama inapikwa kwa wingi. Anaandika barua namna mali yake ingerithiwa. Katika barua hiyo, anatoa ushauri wote ambao anamwachia Omolo. Anatafakari kuhusu kifo na kuhitimisha kwamba ni jambo la lazima:

> "Akacheka sana. Akaenda kwenye friji, akalifungua na kutoa chupa ya *Brandy…* Akakoroga kwa kidole, kisha akanywa mafunda ... Akamimina vidonge vyote kumi na vitatu, akavitia mdomoni kisha akameza kwa funda tatu za *Brandy …*" (uk.171).

Mhusika Queen ametumiwa na mwandishi wa riwaya hii kama balozi wa ushauri. Kwa wale wanaotaka kuoa wapate kupimwa kwanza na kuaminiana katika chuo cha ndoa. Katika safari yake ya mwisho, anahakikishia watu kutenda mema kwani hataki waathirike kwa kuambukizwa virusi vya ugonjwa hatari ya Ukimwi. Hataki mtu mwingine hasa aliye na sifa kama Omolo kuangamia bila kuzaa mtoto.

Tumeona kwamba Queen hakuolewa kwa sababu ya kuchukua muda masomoni, kutofungwa na sheria za jadi na utamaduni kwani aliishi mtaani, Tandika. Vilevile, pesa na anasa nyingi inachochea uozo wa maisha yake unamfanya kusalia kapera. Jumbe hii inaturejesha katika mhimili kwamba, maadili ya jamii hutegemea mahusiano kati ya wanajamii na pia mazingira yao. Kinachochangia hali ya Queen kupenda anasa ni mahusiano yake na watu wa Tandika kama vile Ngoma vilevile kuishi katika mtaa wa Tandika uliokuwa wa anasa.

Tunaona kwamba, Queen amemfana Nice katika riwaya ya *Paradiso* kwa hulka kama vile urembo na kupenda sana anasa. Maisha ya Queen inaharibika kwa sababu ya kujihusisha na anasa. Vilevile, Nice anaenda ng'ambo kusoma, lakini anakosa kukamilisha elimu kwa vile anayumbishwa na anasa. Tofauti kati ya wawili hawa ni kwamba, Queen anaathirika na kuanga dunia kutokana na makali ya Ukimwi, huku Nice anasalia ameharibika. Hii ni kwa sababu ya tamaa.

### 2.2.4 Uteuzi wa Omolo kama Mwanamume Mwenye Mlahaka Mwema

Omolo kama mmoja wa wahusika wakuu, ana mwingiliano mzuri na watu. Ni msomi aliyebahatika kupata kazi nzuri tena kubwa ya mshahara mkubwa katika mtaa wa Tandika, eneo lilojaa anasa kwani ina sehemu nyingi za burudani kama vile *Malaika Bar, Mwangaza Bar, Hotel Victoria* na nyinginezo. Yeye huja sehemu hizi kila mara kujiburudisha hasa nyakati za jioni. Anasa yake ni kunywa bia na kula nyama choma. Wakati mwingine hujumuika katika gumzo na akina dada kama Pendo na Chiku. Haoni faida ya pesa. Pendo na Chiku wanashinda wakiguzisha vifua vyao vilivyojaa maziwa katika mgongo wake kama ishara ya kumsisimua na kumtaka wafanye mahaba. Hata hivyo, anastahimili mawimbi haya ya tamaa:

> 'Pendo na Chiku walikuwa wanamzongazongakumgusa mgongoni kwa
> vifua vyao vilivyojaa maziwa…Yakobo, aliyekuwa… na kusema, "Nyie
> wanawake siku moja mtambaka Jaluo wa watu!" (uk.16).

Amechukua muda akiwa kapera licha ya mamake kumpendekezea aende nyumbani kijijini akaoe. Hii ni kwa sababu amechukia asasi ya ndoa na hivyo, hapendi kutembelewa na mwanamke nyumbani kwake wala kuwa na haja ya kupata watoto. Kwa maoni yake, anafahamu watu walioa lakini anasikitishwa na malalamiko yao ya kila siku kuhusu ndoa. Hii inamfanya kujishughulisha na uraibu wa kunywa bia na kusikiza muziki. Karibu kila siku baada ya kazi, analazimika kuzuru majumba ya burudani ili apate uhondo wa anasa. Anapata kukutana na kufamihiana na Queen kwa mara ya kwanza wanapohudhuria mkutano pamoja. Ni wakati huu ambapo uhusiano wao unaibukia. Hata hivyo, ni wa kirafiki usiohusu miili yao:

> "Walikutana mara ya kwanza kabisa walipohudhuria semina ya usimamizi wa fedha za miradi ya wawekezaji binafsi wadogowadogo. Omolo alivutiwa na michango ya mawazo aliyotoa Queen katika semina hiyo …" (uk. 47).

Wanaporudi Dar es Salaam, Queen anafurahi ghaya kwa kugundua kwamba Omolo pia ni mkazi wa kitongoji cha Tandika. Hii ni kwa sababu alikuwa na tamaa ya kufanya naye mahaba. Uchu unampelekea kufanya juu na chini kuhakikisha kwamba anamtembelea kwake na urafiki unashamiri. Hata hivyo, anashangazwa na hali ya Omolo kutokuwa mchangamfu. Anafaulu kumnasa kwa sababu ana pesa. Queen anamwalika katika klabu ya *Kiti moto*. Ni kuanzia hapa ndipo Queen aliposisitiza kuwa wapitie kwake kustarehe kwa kuinywa kileo cha *Duncan.* Mwandishi amemtumia Omolo kama kielelezo cha wanaume wasiotawaliwa na tamaa. Hali yake ya kuwa imara inadhihirika kwa kutolegeza kamba na kupapia kumtembelea Queen mara tu anapomwuliza kwenda kwake. Anakubali kuandamana naye baada ya kileo kilichokuwa kwake kutumiwa kama chambo cha kumvutia na kumnasa:

> "Basi ngoja nikuwekee kidogo tu halafu tuchanganye na *juice* ya nanasi…"
> … Alishangaa kuona hisia ngeni zinamjia. Damu yake ilisisimka. Kichwa kilikuwa ni kama kinavimba… hamu ya kimwili... chumbani. (uk. 51- 52).

Wanapotumia mpira katika duru ya kwanza, unakuwa sawa, lakini mara ya pili mpira unachanika. Kitendo hiki kinamfanya atoke mara moja na kuenda kujiosha. Hatua ya kufanya hivyo ni dhihirisho anaogopa kuambukizwa virusi. Huenda hii ndiyo maana hakuambukizwa virusi. Hali ya kutotawaliwa na tamaa inapelekea kumlaumu Queen kwa kumhadaa na kumuekea madawa ya kumsisimua mwili ili afanye mapenzi.

Mwandishi anamsawiri Omolo kama mhusika anayeogopa kutahiriwa hapo mwanzoni. Anatoa sababu ya kuwa hivyo kwamba, hakupenda mambo ya wanawake. Kukataa kwake huku kunaashiria kutotawaliwa na tamaa. Anapendwa sana na Tabu kwani ni jirani mwema. Kwa ukuruba huu anakubali ombi la Tabu la kumpa Grace kazi pasi na kuwa na tamaa ya kutaka chochote. Baadaye, alimtafutia Juma na ndugu yake Grace kazi katika kampuni ambayo amesimamia. Matangusano mema baina yake na watu inapelekea watoto wa Tabu kumwita 'Mjomba'.

Omolo anabainika kama mhusika au mtu mwenye utu na ubinadamu. Queen akiwa amezidiwa na maradhi huku ametorokwa na kila mtu, akichekwa na kusemwa namna anavyougua, yeye mwenyewe anamsaidia kwa kumpelekea mamake, Bi. Kimaro barua ambazo majibu hawakupata; wakakosa kujua kama zilifika ama hazikufika. Tena, Queen anapomtaka mamake, anachukua jukumu la kuenda hadi Mwanza kumtafuta na kisha kumlete Tandika.

Hakuwa mtu wakuchoka kwani aliendelea kumshughulikia Queen. Hata anapofariki, ni yeye anatwikwa jukumu la kuijulisha ofisi anakofanya kazi na pia kupanga na kushiriki katika mazishi yake. Zaidi ya hayo, anahakikisha kwamba, wosia, maelekezo na ushauri alioutoa Queen anaufuata hadi mwisho. Kwanza, hakufaa kumweleza mtu kwamba alijiua. Ilistahili isalie siri kwa vile sheria za dini na nchi zinakataa mtu kujitoa uhai, na kama ingejulikana alifanya hivyo, ingewapa ndugu zake shida kudai urasimu alikokuwa akifanya kazi. Omolo ni msiri. Mama naye, angepata shida kumpata mchungaji wa kumzika. Pesa zilizokuwa kwenye benki na hati ya nyumba inafaa ikabidhiwe mama yake ili azitumie kwa furaha na zingine kumtunzia Dadii na hapo baadaye, nyumba amrithishe. Omolo ametumiwa kama kielelezo kwa watu wengine ili wahakikishe kwamba, wamepima damu na pia kutafuta mpenzi na yeye pia afanye hivyo kisha wafunge ndoa. Anashauriwa kwamba, ngono haina starehe isipokuwa huwa ni majuto baada ya kuishiriki:

> "… sijakuambukiza huu ugonjwa, tulitumia mpira. Tafadhali, nenda
> ukahakikishe. Kapime… nakusihi, tafuta mpenzi, naye akapime damu,
> umuoe na uwe mwaminifu na yeye awe mwaminifu kwako." (uk. 178).

Moyo wake wa upendo na huruma haukukomea kumtendea Queen mema tu, bali anamsaidia vilevile Mzee Ngoma aliyekuwa hasidi wake kuhusu Queen.

Walipokutana naye katika nyumba ya Queen, Ngoma akawa anamchukia. Hata hivyo, anapoona Ngoma hana mtu wa kumtunza, anajawa na huruma. Anadhihirisha mguso wa hisia zake kwa kurejesha Tabu na kujenga uhusiano wa ndoa yao iliyokuwa tayari imesambaratika. Pia, kumrejesha Juma nyumbani. Matokeo ikawa, Juma anasamehewa na talaka baina ya Ngoma na Tabu inafutiliwa mbali. Aidha, watoto wake wote wanarithishwa mali.

Omolo amesawiriwa kama mfano mzuri wa watu wanaofuata ushauri. Anafanya namna wosia aliopewa na Ngoma na kukataa kata kata kuwapa jamaa yake wanaotaka kuleta shida wakidai mali. Jamaa wa Ngoma wanapoona mambo kuhusu urithi maji kazidi unga na kukosa kufanyika namna wanavyotaka, wanaichukia na kujitenga na familia ya Ngoma.

Aidha, ni mfano mzuri wa watu wanaofuata ushauri wa watu wenye hekima. Anatii kupimwa virusi vya ukimwi na kisha kutahiriwa anavyoshauri Hans. Vilevile, anashauriwa kutambua umuhimu wa kuoa Grace. Kutokana na huruma wake anakumbwa na hofu Grace anapokuwa mja mzito. Wasiwasi yake inatokana na hali ya kumhurumia kiumbe atakayezaliwa kwa kuja dunia kuteseka kwani ulimwengu umejaa mambo mengi yanayosikitisha. Hata hivyo, inadhihirika kwamba, ni ushauri wa Hans, unapunguza makali ya hofu hii.

Tena, utendakazi wake unamfanya kuenziwa na pia kuaminiwa na wengi. Kwa mfano, anaalikwa na kupendekezwa na Catherine na Asha awe kati ya viongozi wa hazina ya mayatima wanaoachwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa wa Ukimwi. Hazina hii inadhamiria kuwafaa pakubwa mayatima kama kuwaonyesha namna ya kutumia mali wanaoachiwa. Kulingana na uchambuzi tuliofanya katika utafiti huu, umetusaidia kubaini kwamba Omolo alipata sifa hizi zote za heshima kwa vile alikosa kutawaliwa na tamaa katika maisha yake. Wafula na Njogu (2007: 28), wakirejelea nadharia ya maadili wanasema kuwa ni shughuli ya jamii kutathmini kwa kuangalia na kuchuja mambo ambayo ni bora kuigwa na kuyapuuza ambayo hayafai. Catherine na Asha wanamthamini Omolo kuwa mtu mzuri kwa kuzingatia mema anayofanya na kutaka wafanye kazi pamoja.

Kwa hivyo, tukilinganisha Omolo wa riwaya ya *Ua la Faraja* na wahusika wengine katika riwaya ya *Paradiso*, ni bayana kwamba, hakuna mwenye mlahaka mzuri kama Omolo. Hana tamaa ya ngono, mali / pesa na kazi. Kwa mfano, anamsaidia Mzee Ngoma kuyauza magari yake bila kutaka

amlipe tena anaweka wosia ya Queen na kufanya jinsi anavyoshauriwa bila tamaa ya kuibadilisha ili imfaidi.

### 2.2.5 Grace dadake Tabu

Ameteuliwa na mwandishi kama mhusika mkuu asiyejihusisha na anasa wala tamaa. Hata baada ya kuwa na kazi nzuri katika kampuni moja na Omolo, hana tamaa ya kutumia pesa zake katika anasa. Anachukia chochote kinachomleta Queen karibu na Omolo kwa kuhofia kwamba, angemshawishi kutenda maovu. Hii ni kufuatia hulka mbaya za Queen. Mapenzi yake kwa Omolo ni kwa ajili ya ustaraabu wake. Ni dhahiri kwamba, ni mwenye chuki kwani anamchukia shemejie, Ngoma kwa kumwambukiza dadake virusi vya ukimwi alivyovipata kutokana na uasherati. Ana huruma na pia maadili, kwani akiwa na Omolo, wanawashughulikia Mzee Ngoma na Tabu wanapozidiwa. Ni wa kuelewa mambo kwani anamtuliza dadake anapokuwa akilia na kumshawishi kwenda kupimwa damu kwanza ili kuthibitisha kama ameambukizwa virusi vya ugonjwa hatari wa Ukimwi. Katika kufanya hivyo, mwandishi amemsawiri kama mtu wa kuleta mawiano katika ndoa. Alifanya hivi kwa kushirikiana na Omolo kuijenga upya tena familia ya dadake. Ni msichana mwaminifu asiyerandaranda kama wengine na kupumbazwa na anasa hata kama ana kisomo, kazi na hata pesa. Analenga kupata mume wa kumuoa na waishi maisha ya kuaminiana. Kutokana na ushauri wa dadake na daktari Hans, anaolewa na Omolo na kubarikiwa na mwana mmoja kwa jina Tumaini. Kutokana na ukaribu aliokuwa nao na dadake na jitihada kuhusu maisha, baada ya Tabu kuionyesha dunia kisogo, jamaa yake inamtwika majukumu ya kuwa mama ya familia iliyokuwa ya dadake. Tunajulishwa kwamba, babu aliitahadharisha jamaa:

> "… kumtaja mrithi yaani msimamizi wa nyumba hii… marehemu
> apate mtu wa kumpokea usimamizi wa nyumba na wanawe… ni nyinyi
> mnaotakiwa kumchagua mama yenu… wakasema, "Ma'mdogo Grace."
> (uk. 357-358)

Kutokana na dondoo hii, ni bayana kwamba anapendwa na watoto wa dadake wote. Ni kwa sababu hii wanampendekeza kuwa kiongozi wao na pia mama yao. Na yeyote anayekuwa na tatizo anafaa kumuendea. Katika utafiti huu, tumeweza kufasiri kwamba, Grace anachaguliwa kwa sababu ya wasifu wake wa kupendeza. Hakuwa mpenda anasa wala uasherati namna wanawake wengi wa wakati wake walivyokuwa. Alikuwa mwaminifu na mwenye bidii ambayo ni taswira kamili ya

dadake, Tabu. Ni kwa sababu hii ya kutokuwa na tamaa inampelekea kuziguza nyoyo za wengi na kuteuliwa kama kinara wa aila ya dadake kwani hangeweza kutumia mali ya watoto wa dada yake shaghalabaghala. Kama anavyochukulia Vaughn (2008) katika nadharia ya maadili, maadili husaidia kuongoza matendo, kufasili thamani ya mwanadamu na pia sheria zinazomwongoza, jamaa ya Ngoma inaweza kumtambua Grace kuwa wa thamani kwa sababu ya matendo yake mema. Hii ndiyo maana familia hii ikamchagua kuiongoza.

Katika *Ua la Faraja*, Grace amesawiriwa kama mwanamke ambaye hana tamaa ya ngono na pia mali. Tukimlinganisha na wahusika wengine katika riwaya ya *Paradiso*, hakuna mhusika ambaye ni dada ya mhusika mwingine aliye na maadili mfano wa Grace. Ni mvumilivu kwa vile ana pesa lakini hajihusishi na anasa. Vilevile, anatenda tendo la ngono na Omolo baada ya wao kupimwa na kisha kufanya harusi.

### 2.2.6 Daktari Hans kama kielelezo cha matumaini mma

Yeye ni mhusika mkuu kwani amesawiriwa kama amechukua sehemu kubwa ya riwaya na kutoa ushauri ufaafu kwa wale wanaohusika. Ametumiwa kusawiri matatizo yanayoikumba ndoa kama vile ugonjwa wa ukimwi na anasa. Kwa maoni yake, takwimu zinaonyesha kwamba, nchini Marekani ukimwi ulikuwa unapungua na barani Afrika, ulikuwa unazidi kuenea. Anaelezea kuhusu nadharia yake inayoelezea kuenea kwa ukimwi. Kulingana na Hans, ukimwi unaenea kwa kasi sana barani Afrika kwa sababu ya uhusiano mkubwa na matatizo ya mvurugiko wa kiuchumi na kijamii, hasa matatizo ya kiutamaduni. Hii ina maana kwamba, watu wengi wanapata ugonjwa huu kwa kutafuta pesa. Wale hawana pesa hupewa na wale wanazo lakini ni wagonjwa. Wenye pesa huzitoa na kuwapa wasiokuwa nazo ili wafanye mapenzi na mwisho huwaambukiza magonjwa. Tena, imedhihirika kwamba, ukimwi ulianza wakati vijana wengi Wafrika walikuwa katika njia panda ya kiutamaduni. Walichanganyikiwa kuifuata ujadi au usasa kwani viongozi wengi wa Kiafrika, kama vile wanasiasa na wasomi walikuwa wanaiga na kutukuza utamaduni na maadili ya kigeni. Kutokana na sababu hizi inaweza kuchukuliwa kuwa, ukosefu wa maadili unachangia katika uambukizaji na ueneaji kwa ugonjwa huu. Hapa kuna maana kwamba, Mwafrika asili hakuwa na uasherati, ulafi, ulevi, ubinafsi na ufahari. Baada ya kuiga tabia ya kigeni, akaishia kuwa na sifa hizi ambazo zinamwangamiza. Mtoto mwafrika alifunzwa umuhimu ya haya yote hasa ngono na ndoa. Ameonyesha wazi kwamba, dini ya kigeni ilikuwa na tamaduni

na maadili geni ambazo Waafrika wengi hawakuelekezwa kuhusu makuzi, elimu ya watoto dhidi ya ngono, ndoa na uzazi:

> "Katika Uafrika ngono haikuwa kitu cha kuogopwa… ngono na uzazi vilichukuliwa kama sehemu muhimu ya maisha ya mtu… vilipewa heshima na kuandaliwa miiko kwa ufanisi wake. Kulikuwa na miiko ya ndoa na ufanisi wake…" (uk.40).

Hans ameonyesha wazi chanzo cha tamaa na maafa miongoni mwa jamii ya Mwafrika kuwa ni mvurugiko wa kiuchumi, mvurugiko wa jamii na pia watu wengi kuwa na tamaa ya kutafuta pesa. Hans ametumiwa kama kielelezo cha kuipa matumaini jamii iliyoathirika kwa ugonjwa hatari. Kwa mfano, anapendekeza kwamba mtu aliye na virusi anaweza kuishi zaidi hata kuliko asiye navyo. Kwa mujibu wa Vaughn (2008), maadili humpa mwanadamu sababu ya kujitambua na pia maadili hujibu maswali yanahusu namna ya kuishi vizuri. Maoni haya yanaweza kuunga mkono maoni ya Hans kuhusu chanzo cha maafa miongoni mwa jamii ya Mwafrika. Mwanadamu anafaa kujitambua na pia aishi vizuri ili kuepuka matatizo yanayoweza kuepukwa.

Hakuna wa kufananishwa na Dkt. Hans katika riwaya hii ingine, *Paradiso*. Yeye ni mshauri mwema kwani anawashauri Omolo, Tabu, Juma na wengineo kuhusu afya na maisha. Hana tamaa ya mali / pesa na mapenzi. Ana maadili. Katika riwaya ya *Paradiso* Michael ni mshauri mwenye tamaa ya mapenzi kwani anafanya mapenzi na Patricia na kumpa mimba. Hana maadili. Ni kielelezo kibaya katika jamii.

### *2.3.0* **Wahusika wasaidizi katika *Ua la Faraja***

Wahusika wasaidizi ni wale wahusika wanaozungumziwa katika sehemu ndogo tu katika kazi za fasihi. Huwa hawatawali riwaya kuanzia mwanzo hadi mwisho pia, wanabadilika. Kwa mfano, mwanzo wakiwa wazuri mwisho huwa wabaya. Wahusika hawa hueleza mengi kuwahusu wahusika wakuu. Wahusika wasaidizi humsaidia msomaji amwelewe vyema mhusika mkuu. Kupitia maingiliano kati ya mhusika mkuu na mhusika msaidizi, msomaji anapata kumwelewa mhusika mkuu zaidi.

### 2.3.1 Mhusika Mpemba kama mtu mwenye kueneza Uvumi

Katika riwaya hii, mwandishi amemtumia mhusika Mpemba kama mtu anayeeneza uvumi. Anamsawiri kama mhusika aliyekaribu na Ngoma na kwa sababu hii anatoa habari nyeti kumhusu. Yeye kama mshiriki wake wa kunywa bia pamoja katika Malaika Bar, anamuelewa kemkem. Ni kutokana naye tunajua kwamba Queen alikuwa anaugua ugonjwa hatari wa Ukimwi:

> Aliwadokezea wenziwe, "E jama ee! Mwajua kwamba Queen amepatwa na mkanda la jeshi?" (uk.14).

Kutokana na mazungumzo ya wote hawa tunafahamu kwamba, Ngoma alikuwa mzinzi aliyewanyemelea wanawake wengi. Kwa sababu ya kuwa na tabia hii mbaya ya kufanya ngono na wanawake wengi pasi na kinga, anaambukizwa virusi vya Ukimwi. Ukweli huu tunaupata kupitia mke wa Mpemba aliyehadithiwa na mke wa jirani yake Ngoma kuwa alisikia wakizozana. Mkewe anamlaumu kwa kumwambukiza ugonjwa hatari wa Ukimwi. Tumeona kwamba, mwandishi amemtumia Mpemba kama muenezaji uvumi ili kutupasha matokeo ya tamaa ya ngono katika familia ya Ngoma, rafiki yake Queen na hata walevi wenzake kwa vile kuna mshutuko baada ya wao kujua kwamba Ngoma ameambukizwa ugonjwa na Queen.

Hakuna mhusika kama Mpemba katika riwaya ya *Paradiso* kwani katika riwaya hii ni kundi la washiriki wa kanisa ndilo linaeneza uvumi wa mapenzi kati ya Musa na Salome. Lakini katika riwaya ya *Ua la Faraja,* Mpemba anafanya hivyo kama mtu mmoja anayeeneza mahusiano na kuugua kwa Queen na Ngoma.

### 2.3.2 Wahusika Chiku na Pendo kama Wasaka Mapenzi

Chiku na Pendo wametumiwa na mwandishi wa riwaya hii kuonyesha namna dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa na wawili hawa. Wamechorwa kama wahusika wahitaji wanaotafuta pesa, chakula, kinywaji na hata mahaba kutoka kwa wanaume katika mazingira ya anasa. Wanawahimiza wateja kujihusisha na mahaba pasi na kinga. Ukweli huu unajitokeza wanapomkemea kwa matusi Jose muuza kondomu. Walishinda wakijibanza kwa kila mwanamume ili wanunuliwe pombe / au chakula na hata baada ya hii kutimizwa, hawatosheki kwani wao wanataka ngono. Kwa mfano, wanashinda wakimguzisha Omolo matiti yao kwenye mgongo wake. Hii ni ishara kwamba, ni jinsi ya kumsisimua ili wafanye mahaba. Tabia ya

kumtaka mtu kwa nguvu ni ya kuogofya. Usumbufu huu unamzindua Yakobo na kuwatahadharisha kwamba, kuna siku watakuja kumbaka Jaluo:

> Yakobo, aliyekuwa anafurahia vituko vya Pendo na Chiku, akacheka na kusema,
>
> "Nyie wanawake siku moja mtambaka Jaluo wa watu!" (uk. 16).

Tamaa ya wanawake kuwasaka wanaume na hasa wateja ni kero kwa wateja hao. Ni bugdha na inawafanya wateja kutorokea kungine. Hali kama hii humfanya mwenye baa kukosa wateja na mwisho kufunga baa. Ni ukweli kama mchana kuwa, wawili hawa wanafaulu kupata nyama, vinywaji na hata mapenzi ya muda inayowafanya kuambukizwa virusi vya Ukimwi na kuionyesha dunia kisogo. Katika utafiti huu, mwandishi ametuonyesha jinsi wawili hawa wanavyowataka wanaume mahaba kwa nguvu kiasi kwamba wakawa ni kero kwa wateja. Wanafanya mahaba pasi na kinga na hatima yao inakuwa ni kifo. Kutokana na tabia waliokuwa nayo, waliwaambukiza wengi virusi vya Ukimwi. Tukirejelea maoni ya Vaughn katika nadharia ya maadili kuhusu kinachofanya tendo lolote lionekane ni zuri au baya, tumepata kwamba, tabia ya Pendo na Chiku haikuwa nzuri kwani inachukiza vilevile inachangia kueneza Ukimwi.

Katika riwaya ya *Paradiso*, hakuna usawiri wa wanawake wanaotafuta mapenzi na pesa / mali katika mazingara ya starehe na anasa jinsi Pendo na Chiku wanavyofanya katika baa. Tabia ya wawili hawa kumtaka mwanamume kwa nguvu, inaweza kulinganishwa na hulka ya Lona, mkewe Joshua. Lona anatumia nguvu kumtaka Boribori kufanya naye ngono. Tofauti kati ya Lona na wawili hawa ni kwamba, Lona ameolewa lakini Pendo na Chiku hawajaolewa.

### 2.3.3 Juma kama mwana wa Ngoma na Tabu

Kavuria (2008: 108-110), anazungumzia masuala yanayohusu haki za watoto. Haki hizi zinaambatana na maafikiano ya Muungano wa Umoja wa Kimataifa yaliyofanyika tarehe 20/ 11/ 1959 (Kabeberi, 1990). Maafikiano hayo ya haki za watoto yalitokana na umuhimu wa kimataifa wa kutetea haki za wanadamu, wakiwemo watoto. Baada ya mapatano hayo ya kimataifa, nchi kadhaa husika za muungano huu, kama Kenya, zilianza kubuni sheria ili kulinda haki za watoto katika sheria ya haki za watoto (2001). Haki zinazotiliwa maanani zaidi ni ulinzi wa watoto kuhusu ukatili na mila zilizopitwa na wakati, elimu na zingine. Utetezi wa haki ya namna hizi unazingatiwa sana na msanii huyu. Mkufya katika riwaya ya *Ua la Faraja*, anaonyesha juhudi ya jamii kutilia nguvu elimu ya watoto. Watoto wanaofanya vyema shuleni wanahimizwa kusoma.

Kwa mfano, Juma anahimizwa na mama yake kuenda shuleni na kusoma hata baada ya kumsaidia kununua bidhaa za kuuza katika soko. Juma akiwa mwanawe Ngoma na Tabu anafaa kupewa nafasi murwa ya kusoma. Nafasi hii anaikosa kwani muda mrefu anautumia kumsaidia mamake kununua bidhaa za kuuza katika genge. Anapofanya hivyo, anafika shuleni kama amechelewa na kuchoka. Inaelekea kwamba, hata baada ya kujikakamua na kuhudhuria masomo ya ziada baada ya madarasa kila siku, hakuweza kufanya vyema. Hata baada ya kukamilisha darasa la nane, anahimizwa na Omolo kuendelea na masomo lakini anakataa kwani anataka kutafuta kazi ili amsaidie mama yake. Yeye pamoja na watoto wao wengine, walipata kutelekezwa kwani baba yao hakujali walienda shuleni au la, walikula au walivaa nini. Ngoma anawanyima haki ya kutangamana naye kwa vile alikuwa mlevi na mkali kama simba. Anamdhulumu kwa kukosa kumsikiza na kutaka kumpinga, sababu inayompelekea kutoroka na kuenda kuishi kwa babu yake. Kutokana na Juma, tunapata mambo mengi kumhusu baba yake. Ngoma ni mlevi kiasi cha kuwanyima watoto wake mapenzi ya mzazi. Ni kupitia kwake tunaona athari ya tamaa ya anasa inavyoiathiri familia. Babake, anaifilisi mali yake licha ya kupata pesa nyingi kila siku. Hana la maana analofanyia pesa ila kuwanunulia wanawake na pia yeye mwenyewe pombe. Ni kutokana na anasa yake anaambukizwa Ukimwi na kisha kumuambukiza Tabu. Matokeo ya tabia hii mbaya inawahuzunisha watoto wake kwani inawafanya kusalia mayatima mapema. Mwandishi anasema kwamba:

> "… aliposikia dhoruba ile ya habari kwamba kuna uwezekano kuwa baba amemwambuki mama virusi vya UKIMWI, moyo wake ulipasuka kama bomu . Akaangukia kitandani na kulia sana." (uk. 35).

Baba yao anamkosesha furaha kwa kumwambukiza mama yake virusi. Anamfanya kulia na kumfanya awe na chuki, hofu, mawazo mengi na hata hali ya kunuia kumuadhibu. Vitendo vichafu vya mzazi vinatamausha kwani alijua hangeweza kutimiza ndoto yake. Hangeweza kumpa mamake: maisha mazuri, kuona tabasamu yake na pia hangeweza kuipangusa machozi ya mama yake. Haya yote yanatokea kwa sababu ya tamaa. Tamaa hapa, imeonyeshwa kuwanyima watoto haki nyingi kama zilizotajwa. Mwandishi amemtumia Juma kama kielelezo cha watoto wanaume wanaodhulumiwa na wanaume ambao ni watu wa karibu kama baba mzazi. Gitobu (2014: 9), alisema kwamba, fasihi inafaa kufichua uozo katika jamii na kisha kuielekeza kutenda mema

kutumia njia za kulemea maovu. Tumeona namna Mkufya alivyofichua maovu yanayotendewa watoto hasa watoto wavulana. Uozo huu unafaa kukomeshwa.

Katika riwaya ya *Paradiso*, Mango anatelekeza Apondi na watoto wake. Anawaacha Budalangi bila kuwapa mahitaji muhimu. Hali hii inamfanya Michael kukosa kuendelea na masomo na badala yake anaamua kujifunza useremala ili amsaidie mama yake. Maisha yake ni sawa na Juma kwa vile hata yeye (Juma) anaacha kuendelea na shule ili kumsaidia mamake kuuza genge. Apondi naye anaamua kufanya kazi ngumu kama vile kuwalimia watu shamba na kuuza samaki ili kukidhi mahitaji ya familia yake. Apondi anaaga dunia kutokana na athari ya kazi ngumu anayofanya. Mateso yote wanayopitia mama na watoto wao imesababishwa na tamaa ya waume wao kuwa na tamaa ya wanawake wengi.

### 2.3.4 Mhusika Asha kama kahaba

Inachukuliwa kwamba ukahaba ulianza kitambo. Tofauti ilioko sasa na wakati huo ni kuwa, hapo zamani haukuwa umeenea sana kama enzi hii. Hapo awali kilichokuwa kizuizi kwa ukahaba kushamiri ni: mila na itikadi kali zilizokuwepo katika jamii, kanuni za dini na hali ya maisha kwa jumla ambayo haikuwa mbaya kwa mfano uchumi. Tunachukulia kuwa, tofauti iliyoko kwa sasa inayopelekea watu wengi kuwa makahaba ni kuwepo kwa kinyume ya sababu tulizotaja hapo awali. Sababu zingine tunaweza kuongezea ni kuwepo kwa maingiliano ya watu tofauti, kukosa kushika na kufuata dini pamoja na watu kuchukulia kuwa ukahaba ndio mtindo wa maisha. Wanaume kwa wanawake ni makahaba. Katika kazi hii, tuna mhusika Asha ambaye anapenda biashara hii. Ni kahaba kwani anaandamana na watu walio na pesa kama Msafiri, Ngoma na Hastings na kufanya nao mapenzi ya mwili. Hajaolewa na hataki kuolewa kwa sababu anachukulia asasi ya ndoa kama utumwa. Ni bayana kwamba tamaa ya mapenzi huwakumba hata wanawake wenye pesa. Wanawake wa aina hawa ni wa majigambo na hutumia pesa zao kama kishikio cha kuwanasa wanaume. Wanawanunulia pombe na hata chakula katika sehemu za burudani na starehe. Uwezo wa pesa unawafanya kutangamana na wanaume tajiri na kufanya nao mahaba. Kutokana na tabia yake tunaona jinsi ugonjwa hatari wa Ukimwi unavyoenea kutoka mwanamume / mwanamke mmoja hadi mwingine kwa sababu ya tamaa. Kwa mfano, Queen alipomwambukiza Ngoma, naye akamwambukiza Asha aliyemwambukiza Msafiri na kuendelea. Ni kielelezo kuwa mapenzi hayachagui hata mfanyi biashara. Asha ni mwana biashara anayemiliki hoteli ya kifahari ya Hotel Victoria katika kitongoji cha Tandika.  Ana pesa chungu nzima. Ingawa yeye ni tajiri,

hatosheka kwani aliendelea kuhitaji pesa zaidi. Thibitisho ya madai haya ni hali ya kumnata sana Msafiri anapotoka safarini Kigali kwa vile yeye huwa na pesa nyingi:

> " Kila alipowasili toka Kigali Asha aliambatana naye kila mahali, Asha akiwa mtangulizi, yeye akifuata nyuma." (uk. 81- 82).

Kutokana na dondoo hili tunaona kuwa kuna kutawaliwa na tamaa ya pesa. Sababu kuu ni kuwa Msafiri alikuwa na pesa ndiyo maana hakujitenga naye. Pesa zote zinaishia kwake. Hata hivyo, Msafiri baada ya kuambukizwa virusi vya ugonjwa na kufilisika, anamfurusha na kuamuacha aende kwao. Hakumsaidia wala kumsindikiza. Tumetahadharishwa kwamba, tamaa ina matamu na matokeo yake ni machungu mithili pilipili. Kwa mujibu wa Jean Jacques Rousseau (1755), kitu cha maana katika maisha ya binadamu ni upendo na huu ndiyo msingi wa furaha. Tumeona kwamba Asha hakuwa na upendo, kwa vile anamkosesha Msafiri furaha anapomfurusha. Tabia yake ni sawa na Sakina katika riwaya ya *Paradiso*. Apondi anamchukulia Sakina kuwa kahaba kwa vile Mango hajamuoa rasmi wala kumpeleka Budalangi. Anashukiwa kuchukua pesa nyingi za Mango jinsi Asha anavyozichukua za Msafiri katika *Ua la Faraja*. Hali yao ni sawa kwa sababu, 'ndoa' yao haieleweki.

### *2.4.0* **Wahusika wakuu katika *Paradiso***

### 2.4.1 Michael kama Mhubiri mzinzi

Michael anasawiriwa kama mhusika mkuu ambaye ni mhubiri mzinzi. Anajipata katika kashfa hii baada ya Patricia kumshawishi na kumleta karibu. Baada ya kutembelewa na Patricia ofisini mwake naye kumtembelea Patricia kwake, waliweza kuotesha mahusiano. Anasahau sheria ya ndoa hasa ya dini yake kuwa anafaa kuitii jiko lake. Anavunja sheria hii kwa kufanya tendo la ndoa na Patricia. Aidha, kutokana na tendo hili, waliweza kumzaa mtoto. Tokeo ambalo linamletea matatizo mengi si haba. Tena anamkosesha mkewe mapenzi kwa kupenda Patricia sana. Ni kutokana na ukosefu huu wa mapenzi unamfanya Lydia kuanza kubugia kileo kinachokuwa chanzo cha wao kuzozana. Michael anajipata pabaya katika mikono ya sheria baada ya kuvunja sheria kwa kumpinga na kisha kumjeruhi. Kulingana na sheria na maadili ni kinyume kumpiga mke vibaya na hata kumjeruhi. Hatua hii inamsababishia shida kadha. Kwanza, anatiwa nguvu na asikari wanaomhoji na pia kutishia kumuua. Pili, anatatizika kisaikolojia kwani anahojiwa na kutishwa. Zaidi ya hayo, anakumbwa na hofu kufikiri kuwa kamuua mkewe pasi na kutarajia.

Tatu, analazimika kugharamia malipo ya hospitali. Katika utafiti huu, tumeona kwamba, dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa kupitia Michael kwa sababu ya vitendo vyake. Tamaa iliweza kumshawishi kiasi kwamba anavunja sheria ya uaminifu na haki aliyoshinda akihubiri. Kama mhubiri, anafaa kuwa kielelezo chema katika jamii kwa kudumisha maadili. Anagharamia malipo ya kuzaliwa kwa Mango mdogo ya hosipitali na hata malezi yake: Mkewe amependekeza kuwa wamsaidie Patricia kushughulikia bili za hospitali. "Ama angemchukua kabisa huyo mwanawe akamwangalia pamoja na wengine alionao." (uk.193).

Kuna uoga fulini unaotokana na tamaa. Aliogopa kumtelekeza Patricia kwani kufanya hivyo kungemletea soni na hata kufungwa. Ili kutuliza hali, anaamua kuubeba mzigo huu ili azidi kuwa mtu muadilifu katika jamii. Uzinzi unazua ugomvi, chuki, na utuaji mzigo wa gharama usiwohitajika. Kwa mfano, Michael anajipata katika hali hii. Anajitahidi kuepuka kusemwa kutokana na maovu anayofanya kwani ni kinyume kwa kiongozi kama yeye anayetarajiwa kuwa kielelezo cha jamii. Kama hangechukua majukumu ya kumlea mtoto wake na Patricia, basi angekumbana na mkono wa sheria. Theodores na wengine (2002: 158) wakimnukuu Bentham (1978) wanasema kuwa wema halisi wa jamii unapaswa kuhusishwa na sheria za nchi. Hivyo basi, yaliyo katika sheria ndiyo huchukuliwa na wanajamii kama adilifu. Wanaendelea kusema kuwa, avunjaye sheria kwa kutenda linalosababisha uchungu kwa walio wengi katika jamii, basi anapaswa kuadhibiwa ili kulinda jamii isidhuriwe na mtu kama huyu: adhabu ilenge kumbadilisha. Michael kama hangechukua jukumu la kumlea Mango mdogo, basi angekumbana na mkono wa sheria ili adilishwe. Rousseau anavyosema katika kitabu chake, *Moral Education* (1762) kwamba, ili mtu aonekane mwema lazima atende mema, inamlazimu Michael kumshughulikia Patricia ili aendelee kuonekana mwanamume mwema. Kwa hivyo, tumeona kwamba, katika riwaya ya *Ua la Faraja*, hakuna mhubiri mwenye tamaa ya pesa / mali au mapenzi. Sheikh Rajabu ni mtu mwaminifu. Anatimiza yote anayoelekezwa afanye katika wosia wa Ngoma kuhusu pesa anazostahili kukabidhi msikiti. Yeye ni tofauti na Michael ambaye ni mzinzi kwani Michael anaonana kimwili na Patricia na kumpachika mimba.

### 2.4.2 Mango kama Mhubiri mwenye tamaa

Mango ni mhubiri mwenye wake wengi. Mke wake wa kwanza ni Apondi anayeishi kule Budalangi. Pamoja na wake wenza wenzake wamesalia huko nyumbani wakijitegemea kwa kuwalimia watu shamba, kulima shamba lao na kukuza mimie kama mihogo. Kando na haya, wanauza samaki ili kujikimu. Ni wao wanaowasomesha watoto wao. Mango kama mume amekosa kuwajibika kwani ameoa wake wengi lakini hawapi pesa za chakula, nguo na hata kuwasomesha watoto. Ametawaliwa na tamaa ya kuwa na wake wengi ilhali hawezi kuwagharamia. Kule Mombasa, kipato chake cha kazi ni duni sana kwani yeye hufanya kazi ya kupakia na kupakua mizigo katika meli za bandarini. Wakati mwingine huwauzia watu maji katika mtaa. Lakushangaza ni kuwa pesa hizi zote huishia kwa hawara yake, Sakina. Habwe amemtumia Mango kama kielelezo cha watu katika jamii wasiojali majukumu yao. Ametawaliwa na tamaa kiasi kwamba hata baada ya kuteuliwa kama kasisi na kushauriwa kufanya harusi na pia kuwaacha wake zake wengine, anakataa kata kata. Tamaa inamfanya kukosa kuwajibika kuwasomesha watoto wake, kuwalisha na pia kuwavalisha barabara. Tamaa ya wake wengi inamfanya kuchukua muda kuitembelea familia yake kule Budalangi. Badadala yake anapotelea kwa mahawara wake huko pwani. Hii ni ishara tosha kwamba, hakuwashughulikia wake hawa wengine. Inaelekea kwamba aliwakosesha mapenzi na kukosa kuwajibika:

> "Mango sasa alifanywa mzee wa kanisa … baadhi ya waumini walioona kuwa hakustahili kwa kuwa alikuwa na wake watano na hapana kati wao aliyeolewa naye kwa harusi." (uk.22).

Kukataa kuufuata ushauri wa wazee wa kanisa kuwa awaasi wake zake wengine ili aihudumie kanisa ipasavyo, inaashiria kwamba, ni mtu asiyewajibika. Hakujali waumini wangesema nini kumhusu. Anasahau kuwa anafaa kuwa mfano mwema wa kuigwa. Ukali aliokuwa nao, unamsawiri kama mtu asiyetaka kuelezwa ukweli hasa kutoka kwa wanawake. Kulingana na hali yake ya kuwa na wake wengi na hata hawara, mwandishi amemtumia kuangazia namna dhamira ya tamaa ilivyokuzwa na kuendelezwa katika riwaya hii. Amechorwa kama mtu aliyelemazwa kutokana na kuoa wake wengi. Kulingana na Kanyange (2015: 28) kwa kutumia vigezo vya uamuaji kama tendo ni adilifu, hali ya Mango kususia kuwatema wake wengine na hali yeye ni kasisi ambaye anafaa kuwa mfano wa kuigwa na waumini katika jamii, si adilifu. Inatoa taswira ya kuhubiri maji na kunywa divani kwa vile watu watachukulia kuwa, wanahadaiwa. Na kwa

kuangazia kigezo cha uwezekano, Mango akiwaacha wake wengine, atakumbwa na uchungu sana. Tena si tendo la uadilifu kwake kufanya. Inaonekana kwamba, mtunzi anakashifu tendo la kutawaliwa na tamaa na pia kutowajibika ambao hutokea katika jamii kwa wanaopewa majukumu ya uongozi lakini wanakataa kuyatekeleza / kuyatilia maanani ingawa wao huwa na uwezo wa kufanya hivyo. Basi, tendo la namna hii si adilifu kwani huzidishia uchungu na masikitiko watu wengine kama alivyohisi mhusika. Mwandishi anamalizia kwa kuhimiza wanajamii kutotawaliwa na tamaa kwani ina athari hasi. Wafula na Njogu (2007: 28) wanasema kwamba nadharia ya maadili inashauri jamii kutathmini kwa kuangalia na kuchuja mambo ambayo ni bora kuigwa na kuyapuuzwa ambayo hayafai. Kwa mujibu huu, jamii inapaswa kupuuza tabia ya kuoa wake wengi jinsi Mango alivyooa kwa vile huwalimbikizia majukumu wasioweza kutekeleza. Tukirejelea riwaya ya *Ua la Faraja* kwa mfano, hakuna mhubiri au kiongozi wa dini ambaye ameoa wanawake wengi jinsi Mango mhusika wa riwaya ya *Paradiso* ameoa. Tamaa ya kuwa na wake wengi inamfanya kuenda kinyume na matakwa ya kanisa lake la kuoa mke mmoja wa ndoa.

### 2.4.3 Lydia kama Mwanamke Mvumilivu

Uvumilivu unachukuliwa kuwa ni sifa ya kimaadili ambayo husaidia hali ya kutofanya maamuzi kwa haraka. Husaidia mtu kukubali hali ya maisha kama vile matatizo anayokumbana nayo katika maisha ya sasa ikitarajiwa kwamba siku zijazo zitakuwa bora. Daima mtu anapokumbwa na matatizo, watu humshauri awe mtulivu na mvumilivu na hata kabla hajawazia kuhusu suluhisho kamili la lile linalomkera. Hali hii ya utulivu ni muhimu kwake kwa sababu itamsaidia kuweza kufikiria vyema na pia kwa makini kuhusu suluhisho la shida inayomkumba badala ya kuwazia suluhisho kwa haraka na ambalo linaweza kumsababishia madhara mengi. Tendo hili ni adilifu na kuikosa si uadilifu. Inachukuliwa kuwa hivi kwa sababu, watu wasio na uvumilivu hawaridhiki na huwa na uwezekano mkubwa wa kupata maradhi ya moyo kutokana na kujiuzulu kazini kwa haraka, kukasirika, kuvunja urafiki wao na wengine kwa haraka na hata kukosa msukumo wa haraka wa kufikia lengo lao wanapokabiliwa na changamoto. Matokeo ya namna haya, yanaleta uchungu kwa yeyote anayehusika na hivyo basi, si adilifu.

Mwandishi wa riwaya ya *Paradiso*, ameonyesha kwamba, pana haja ya kuwa mvumilivu. Anatoa mfano wa mhusika Lydia aliyekuwa mvumilivu na kusoma hadi chuo kikuu, hatimaye akafuzu. Ni uvumilivu unampelekea kufuzu na shahada ya ualimu na kuwa mwalimu. Hakupapia hali ya ulimwengu ya kujihusisha na wanaume kwani hakuwa na mtoto kabla ya kupata jiko. Mwandishi

amemtumia kama kielelezo cha watu wanaotawaliwa na uvumilivu katika maisha na kisha kufaulu. Hata baada ya kumpata Micheal akihubiri, anapata kujenga mahusiano naye kwanza ndipo wakafikia uamuzi wa kufunga akidi.

Vilevile, Michael anapozini na kumpachika Patricia mimba, anachukua hatua mwafaka. Kwanza, anamshuku mumewe kwa kuwa na mahusiano haramu kule nje. Pili, anamdokezea Patricia kama rafiki kuwa mumewe alikuwa na mwanamke mwingine na kayaona ndotoni. Tatu, anaposikia uvumi kutoka kwa walimwengu kwamba Patricia na mumewe walionekana katika hoteli ya kifahari kule Kisumu, anaamua kumjulisha mamake mzazi anayeandamana naye hadi kwa kina bwana ili kushtakia na kupata suluhisho. Nne, anaamua kurudi kwake na kuishi na mume wake. Tano, anavumilia mume wake kuigharamia bili anakozalia Patricia na malezi ya mwanawe. Sita, anavumilia na kuitikia msamaha anayoutoa rafiki yake kwa kunuia kuivuruga ndoa yao. Tunaelezwa kwamba:

"Ee, mwanangu huyo amekuwa kiruka njia hivyo?" Aliuliza Awinja, mamake Lydia.

"Asharuka na kufikia hatua hiyo," Lydia alisisitiza. (uk.156).

Kwa mujibu wa mukatadha huu, hatua aliyoichukua Lydia ilikuwa ya uvumilivu na pia ya hekima. Hakuparamia kuivunja ndoa kabla kuwafahamisha wazazi wao. Ni kutokana na hatua hii ya busara, ndoa yake iliweza kustahamili mawimbi na majaribio. Dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa kwa kuonyesha uvumilivu ukiitawala tamaa. Kama anavyochukulia Tolstoy (1960) katika nadharia ya maadili kwamba, nadharia hii inajukumu kuu la kutatua matatizo ya jamii, Lydia hakukosea anapokuwa mvumilivu kutekeleza mambo yake. Uvumilivu unamfaa pakubwa kumwepusha na maovu. Lydia ni mfano mzuri wa Grace dadake Tabu katika riwaya la *Ua la Faraja*. Grace ni mvumilivu kwani hana tamaa ya mapenzi hadi anapoolewa na Omolo. Ana pesa lakini hajihusishi na anasa. Tofauti baina ya wawili hawa ni kwamba, Grace ametafutiwa mume, Omolo, naye Lydia amejitafutia mume, Michael.

### 2.4.4 Patricia kama Msomi mwenye tamaa ya Mapenzi

Katika riwaya ya *Paradiso*, mhusika Patricia amesoma hadi chuo kikuu na kufuzu na shahada ya elimu. Anafunza hisabati na fizikia katika shule ya upili. Masomo anayofunza ni ishara tosha kwamba ni gwinji katika maswala ya elimu. Hata hivyo, alipokuwa akisoma na pia akifanya kazi, alipata kuchezewa shere kimapenzi na mapwagu wa anasa ya mapenzi na kuishia kupachikwa

mimba na kuzaa watoto. Ana cheche za mapenzi kuhusu Michael, bwana ya rafiki yake. Anamtembelea ofisini mwake na kumpa busu ya kunyonyana midomo na ulimi. Mahusianao kati ya wawili hawa yanakomaa na kumfanya Michael kuifanya mazoea ya kuenda kwake na kukesha huko. Tamaa ya mapenzi inamfanya kumtamani bwana wa rafikiye na kujuta namna hakuumbwa na bahati kama wengine. Ni sababu ya kutawaliwa na tamaa anaonana mwili na Michael na hata mwishowe kupachikwa mimba. Kama msomi, hafai kujiachilia namna hii kwa sababu ya tamaa na kupachikwa mimba ovyoovyo. Mwandishi amemtumia kama kielelezo cha kukuza na kuendeleza dhamira kuhusu tamaa kwa kumsawiri kama msomi anayelegezwa na tamaa ya mapenzi na kukosa kuwa muadilifu. Hali yake ya kushiriki ngono, inamkosanisha na mama na hata rafiki yake. Kama asemavyo mwandishi:

> Patricia alifunga safari ya mawazo lakini alishindwa kufika gatini ambako angeshukia. “Kwa nini Lydia lakini si mimi?” Pattricia asliudadisi moyo wake. (uk.145).

Tunaweza kusema kwamba, tamaa ya mapenzi inamfanya Patricia kukumbwa na biwi la mawazo na kuwaonea wenzake gere. Kwa mfano, anashangazwa ni kwa nini iwe Lydia tu anayefanikiwa kumpata mchumba. Mtu aliyesoma kama yeye anafaa kudhibiti tamaa ya mapenzi. Akifanya hivyo, atakuwa anachangia ukamilifu wake kwani ameelimika, na elimu huzingatiwa kuwa ni kitu azizi kinachoadilisha jamii. Endapo hawezi kuwa kielezo bora katika jamii, basi wanajamii wanakosa kutambua umuhimu wa elimu. Vilevile, jamii ambayo ina wasomi wenye sifa ya aina hii ya tamaa ya mapenzi, wanakosa kielezo chanya cha kuigwa na hatima huwa kukosa kuona manufaa ya elimu. Hivyo basi, sifa ya jamii kama hii ni kuwa na maovu mengi kama kuwa na watoto wengi wanaozaliwa nje ya ndoa. Mwandishi amemtumia Patricia kama mfano wa watu wanaoshindwa kudhibiti tamaa yao na kuishia kuharibu maisha yao licha wao kuwa wasomi. Udhaifu wake huu wa kuyumbishwa na uchu umetumiwa kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa. Patricia ni msomi lakini amekosa maadili. Kama asemavyo Wolf katika nadharia ya maadili kwamba, chochote kinachoweza kuwa kizuri lazima kiwe na uzuri wa ujumi. Ujumi hapa unachukuliwa kama maadili. Tunaweza kusema kwamba, Patricia ni sawa na Queen, Asha, Chiku na Pendo katika riwaya ya *Ua la Faraja.* Hii ni kwa sababu wote wanatawaliwa na tamaa ya mapenzi. Tofauti baina yao ni kwamba, Patricia ni mwalimu, nao Chiku na Pendo ni wahudumu katika baa. Wote wamekosa maadili kwa kutaka ngono nje ya ndoa.

### *2.5.0* Wahusika wasaidizi katika *Paradiso*

### 2.5.1 Apondi kama mwenye bidii

Katika riwaya ya *Paradiso,* Apondi amesawiriwa kupatikana mashambani, Budalangi na mwenye bidii ya mchwa. Ni mke wa kwanza wa Mango lakini hapati pesa kutoka kwake. Ni bidii yake inamlisha, kulisha familia yake na kumvisha. Shida zake zinatokana na tamaa ya mumewe kuwaoa wake wengi ilhali hana uwezo wa kuwakimu. Ametumiwa kutujuza namna tamaa ya mume kuwao wake wengi inavyoathiri mahitaji ya familia nzima. Kwa mfano, anaathirika vibaya kutokana na jitihada zake za kuwalimia watu shamba na kuuza samaki ili kuwalea na kuwasomesha watoto kwani Mango hawafanyii lolote la maana. Vilevile, amechorwa kama mhusika anayeugua kutokana na bidii yake. Tunaelezwa, "… ni yule aliyelima kama tingatinga katika mashamba ya watu kujikimu yeye na wanawe." (uk.90).

Tumefasiri kwamba, maradhi yanayomfisha Apondi, kiini kilikuwa ni kufanya kazi gumu ya kuwalimia watu shamba. Hii inamsababishia maradhi ya kifua na mengine inamfanya kuonyesha dunia kisogo. Chanzo cha matatizo haya ni tamaa kutoka kwa mume wake kuoa wake wengi na kutokuwa na uwezo wa kuwakimu. Habwe alimewakilisha taswira ya uhalisia kuhusu maisha ya Apondi katika mazingira ya Budalangi jinsi nadharia ya maadili inavyosisitiza. Kwa mfano namna Apondi anavyojipatia riziki. Apondi ana hulka sawa na Tabu wa riwaya ya *Ua la Faraja*. Tabu anauza mboga katika genge ili kuikimu familia yake. Kisha anaaga dunia kutokana na athari ya ugonjwa aliyoambukizwa na mumewe, Ngoma. Pia, Apondi anaaga kwa sababu ya ugonjwa anaoupata kwa kufanya kazi ngumu ili aweze kuikidhi familia yake. Hii ni kwa sababu Mango amemtelekeza.

### 2.5.2 Musa Bosire kama Mchungaji Mzinifu

Ni mhubiri wa Kanisa la New Jerusalem. Kama mhubiri anapaswa kuwa kielelezo bora katika jamii. Hapaswi kutawaliwa na tamaa, anapaswa kuhakikisha kwamba, jamii ina maadili mema. Anafaa kukemea maovu kama tamaa ya kuzini na wake wa watu. Tamaa ina nguvu hata ya kumyumbisha mtumishi wa Mungu. Tamaa inamtawala anapomwona Salome ni mrembo wa kuvutia na kutamanika. Ukweli ni kwamba, kuna watu wanaokosa mwelekeo wanapokumbana na mwanamke wa aina huyu. Si ajabu urembo wa Salome unamvutia na kumfanya kukosa kujidhibiti. Mke kama yeye aliyeumbwa na kaumbika ni jaribio kubwa kwa kila mwanaume. Tunaweza

kusema, huenda urembo alio nao Salome ndio ulimsisimua uchu wa Musa kupita kiasi. Hii ndiyo maana wanapopata fursa kidogo, hawajali matukio yao. Tena, hamu kubwa ya kupata mtoto aliyokuwa nayo Salome inamfanya kushawishika kwa haraka na urahisi. Wote basi walikuwa na hamu kuu, wakaamua kutenda tendo la mahaba katika nyumba ya Kyalo. Yanayojia ni kufumaniwa na mwenye nyumba wakiwa katika tendo la ngono. Matokeo yanakuwa ni kupata kichapo cha mbwa nusura hata kuuawa, "Huyu mpaka nimwue," Kyalo alisema wazi huku hamaki zimempanda (uk. 52).

Mwandishi anatutahadharisha kwamba, tamaa huweza kumpumbaza na hata kumporomosha mtu. Hii ni kwa sababu, Musa anaacha kuhubiri baada ya kufumaniwa, kujeruhiwa, kutibiwa na kuruhusiwa kuondoka hospitalini. Anahisi hakuna mtu angeweza kumsikiza tena. Hii ni kufuatia kuenea kwa maovu aliyofumaniwa akitekeleza kwa wenyewe, na mke wa wenyewe tena mshiriki wake. Anaogopa kukejeliwa na kuchekwa. Dhamira ya tamaa imeendelezwa na kukuzwa kumtumia Musa kama mtumishi wa Mungu anayeyumbishwa nayo na kuasi dini. Bila shaka, ni gumu sana kwa mtu wa kawaida kuepuka kujihusisha na majaribio ya tamaa.

Hata hivyo, katika riwaya ya *Ua la Faraja*, Sheikh Rajabu ambaye ni kiongozi wa dini hana tamaa ya mapenzi wala mali / pesa. Yeye na Musa wanatofautiana kama usiku na mchana. Rajabu anafanya mambo kulingana na kanuni ya dini yake. Kwa mfano, anafuata na kutekeleza wosia wa Mzee Ngoma namna umeandikwa.  Yeye si mzinzi, ana maadili.

### 2.5.3 Salome kama Mshiriki Mzinzi

Ni mshiriki wa kanisa anakohubiri Musa. Ni mshiriki mtiifu na mwimbaji hodari. Hulka hizi zote zinawafanya watu wengi kumpenda. Ni wa kuigwa kila wakati na washiriki wengine. Kwa mfano, anapoongoza wimbo, wote wanapata mhemko na uhondo wake. Urembo alio nao, sauti tamu kama ninga na maungo ya kuvutia, hayamweki pa kutenda maovu kama haya. Hata hivyo, tunatambua kwamba, tamaa ya kutaka mwana inamzuzua na kumfanya kukubali ushawishi kutoka kwa mhubiri wake. Tunaweza kusema kwamba, Musa alingamua udhaifu wake na hata kufahamu kuwa ni mhitaji sana.

Huenda Musa alifahamu haya alipokuwa anaulizwa aseme shida zake ndipo alisema ni mtoto. Musa kama mhubiri mnafiki na mlaghai, aliposikia haya, akatumia udhaifu huu kumnasa. Tumeweza kufasiri kwamba, huenda alimshawishi kuwa kupitia kwake Mungu angempa mtoto.

Ni katika hali ya kutekeleza kitendo hiki ndipo wanafumaniwa na kujeruhiwa na kusababisha siri kuwa si siri tena. Tamaa ya kutaka mtoto inazua mambo kama vile: kwanza, Musa kuzini na kupigwa na hata kudungwa kisu. Hali ambayo nusura imfishe. Pili, hata mwenyewe kupingwa na pia kujeruhiwa kwa kisu. Hali hii vilevile, inamfanya Kyalo kulipia bili ya matibabu ya hospitali. Tatu, kunakuwepo na soni kwa wote kwa mfano, mume wake kujulikana kuwa hana uwezo wa kuzaa. Wote kama washiriki wanaonekana si waaminifu mithalani, Musa kama mchungaji si mwaminifu kwa waumini. Nne, anachangia Musa kuacha kuwa mtumishi wa Mungu. Hii ni kwa sababu, hangeaminika tena kwani ni kosa kubwa ambalo kila mara hukemewa. Katika utafiti huu, tumeona kuwa mawimbi ya tamaa si mchezo; yanayumbisha hata waumini, wanaume kwa wanawake, waliyoolewa na hata walalahai. Wote wanajipata katika majaribio. Kunahitaji ustahimilivu ili mtu kuepuka majaribio ya tamaa. Salome anamshawishi mume wake: "Mume wangu nitakuruhusu uoe mke wa pili ili upate kizazi chako." (uk.59).

Wakati mwingine mwanamume anapompata mwanamke mrembo akizini, kumtaliki huwa gumu sana. Hii ndio maana, Kyalo anamwomba msamaha kwani angedhubutu kumuacha, angeolewa na mwanamume mwingine. Tumeona kuwa alikuwa akijaribu kumbembeleza na kumpumbaza mume wake tu aoe mke mwingine. Kilio chake kwamba alizini kwa kuwa anataka mwana, ni kisingizio tu. Mwandishi wa kazi hii amemtumia kuonyesha watu kwamba, ni vyema kujihadhari na watu wanaochukuliwa kuwa washiriki na washika dini kwani nao pia huyumbishwa na kuathiriwa na tamaa. Ni kupitia haya yote, dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa. Leo Tostoy (1960) katika nadharia ya maadili, anapendekeza sanaa iwe ya dini ili iweze kuwaelekeza watu wawe na tabia njema. Tunaweza kusema kwamba, Habwe ameweza kudhihirisha mawazo haya katika kazi yake jinsi watu wanafaa kuwa na tabia njema wakifuata dini bila udanganyifu. Kwa mfano, Musa na Salome. Hata hivyo, hakuna mshiriki wa kike wa dini ambaye ni mzinzi katika riwaya ya *Ua la Faraja*.

### 2.5.4 Washiriki wa Budalangi Church of God kama Walafi

Habwe anapiga vita tabia ya ulafi. Anawasuta watu walio na tabia ya tamaa ya ulafi hasa wakati wa matanga; kutaka kupewa pesa/ vitu vingi kupita kiasi. Vile tujuavyo, ulafi ni tabia hasi ndiposa watu wanastahili kutahadharishwa na kuonywa dhidi ya mwenendo kama huu. Nadharia ya maadili katika utafiti huu, inadhihirisha kwamba fasihi inafaa kuadilisha kwa kutahadharisha wanajamii dhidi ya maovu kama ulafi ndiposa katika riwaya hii, Habwe anawatahadharisha dhidi

ya kuitisha vitu vingi vya matumizi katika matanga. Kufanya hivyo inaonyesha tamaa / ulafi ni tabia mbaya na hukera. Hivyo basi, ni jambo la busara tena la kupendeza ikiwa watu watapuuzilia mbali. Selifa anaitisha: "Tungependa … utupe ng'ombe mmoja, sukari kilo ishirini, mafuta ya kupika kilo tano na shilingi elfu tano." (uk. 94).

Huu ni ulafi wa kiwango cha juu sana na unakusudia kuwaumiza wanajamii ambao tayari wana shida. Kutokana na mhimili wa nadharia ya maadili tuliotumia, umetuongoza kubaini kwamba dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga jamii kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii. Mawaidha ya Habwe kuhusu ulafi yanaweza kutumika kwa jamii yoyote ile kwa vile watu wengine hupenda kujitakia makuu na kutojali wengine. Watu kutaka vitu katika matanga na kuwaacha wengine wakihangaika katika ukata. Hii ndio tabia inayopigwa vita na kukemewa. Mwandishi, amewatumia wahusika hawa kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa. Wanafananishwa na Kassim na Mashaka katika riwaya ya Ua la Faraja kwenye matanga ya Ngoma. Wanataka maombolezi ya muda mrefu. Hii inatokana na msukumo wa tamaa unaolenga kuifilisi waliofiliwa.

### 2.5.5 Chifu Mohamed Owaki kama Mtumishi Mlafi

Yeye ni mtumishi wa umma. Anafaa kuhudumia jamii kuanzia mashinani. Anapowahudumia wananchi anafaa kuhakikisha kwamba haki ukweli inadumishwa. Lakini ana tamaa kwani anapotaka kitu huona ni lazima apewe. Hana soni kuitisha vya bure. Mfano wa kisa cha aina hii kinapatikana katika matanga ya Apondi ambapo Chifu Owaki akiwa mtumishi wa serikali ni mlafi. Inasikitisha kwamba, anatumia nguvu na vitisho ili waliopata msiba watoe ng'ombe. Ni ajabu kwani badala ya kuwahurumia na kuwasikitikia, anazidi kuwatwika mzigo mwingine. Tabia kama hii inafaa kukemewa kwani huwafanya waliofiliwa kupatwa na matatizo ya kisaikolojia. Tumemwona akimtisha Mango: "Hii ni mila. Lazima ufuate mila yetu hapa. Usipoifuata ikibidi tutakuchapa viboko …" (uk.93).

Kutokana na dondoo hii tunaona kuwa, ulafi humfanya kiongozi kukosa utu na tena kumtishia mtu wakati wa msiba. Ulafi humkosesha kiongozi maadili. Mwandishi amemtumia Owaki kuiendeleza na kuikuza dhamira ya tamaa kwa kumchora kama kiongozi anayeshindwa kuitetea na kuisaidia jamii yake hasa inapokumbwa na msiba. Hulka hii ameisawiri akidhamiria ipigwe msasa na kupingwa kwa vyovyote.

### *2.6* Matumizi ya Lugha-/ Mbinu za uandishi/ Kunga nyingine Katika *Ua la Faraja*

#### 2.6.1 Mbinu ya Majazi na suala la maadili

Meier (2008: 7) anasema kwamba, uwasilishaji mzuri unaopendeza ni lazima uwe na mali. Na pia uzuri unaofikiriwa lazima uwasilishe aina nyingi za vitu. Tumeweza kufasiri kuwa aina hii za vitu ni maudhui pamoja na mbinu za uandishi. Kati ya hizo ni mbinu ya majazi iliyotumika katika riwaya hii. Mbatiah (2016: 182) anaifafanua mbinu ya majazi kama majina ya wahusika ambayo yanaakisi tabia au sifa zao ambapo majina hayo pia yanawakilisha dhana maalumu. Wamitila (2003: 106- 107) katika ufafanuzi wake anaongezea kwamba, ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au yanatuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Kwa mfano, jina la mhusika linakuwa kielekezi cha tabia yake. Huhusisha pia majina ya mandhari, mahali na mengineo. Mbinu hii pia umuhimu wake ni kwamba, mwandishi anaweza kuitumia kuuchimuza mtazamo na pia mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. Mwandishi wa kazi hii ametumia mbinu hii kwa kuzingatia maelezo haya. Kwa mfano, jina Ngoma lina maana ya avumae sana au mtu mgumu. Mhusika huyu amepewa jina hili kufuatana na hulka yake. Alipenda kunywa pombe sana na pia kujihusisha na uzinzi. Alikuwa mtu wa majisifu na tena ufahari. Mwandishi anamsawiri kama: “Ngoma alikuwa mtu mwenye kutaka watu wamwone kila wakati kwamba yeye ni bora kuliko wao.” (uk.7-8).

Basi, mwandishi amempa jina hili kudhihirisha hulka yake ya majisifu. Hana maadili na anasifika kwa sababu hii. Jina ‘Ngoma’ linamaana, mtu asiyesikia ushauri au onyo. Tabu alimuonya kuhusu tamaa ya kufanya mapenzi na wanawake wengine lakini hakusikia. Mwandishi wa riwaya hii anampa jina hili kutokana na tabia yake mbaya. Anafanya familia yake kuwa na maisha magumu kwa kuitelekeza. Huu ni ukosefu wa maadili. Kwa vile jina hili limehusishwa na ukosefu wa maadili, limechangia kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa kwa vile ana tamaa ya kunywa pombe, kufanya mapenzi na wanawake.

Mhusika mwingine aliye na jina la kimajazi ni Tabu. Ana jina hili kuonyesha shida anazozipata. Ngoma anamwacha pasi na masurufu na anaamua kuuza genge ili kuikimu familia yake. Anapata tabu kufanya hivyo. Anapitia matatizo mengi kama mume kumtelekeza, kupewa talaka, kubaguliwa na jamaa ya mumewe na kuteseka anapougua. Isitoshe, mumewe anamwambukiza Ukimwi na kupata mateso ambayo hastahili kupata. Kupitia mbinu hii, msomaji anaweza kupata

taswira ya matukio kwa kuyaoanisha na majina ya majazi. Mbinu hii imemwezesha mwandishi kushughulikia dhamira ya tamaa kwa kutoa sifa za wahusika zilizohusishwa na tabia zao. Mbinu hii haijatumika katika riwaya ya *Paradiso* kwani hakuna yeyote aliye na jina la kimajazi aliye na tamaa.

### 2.6.2 Mbinu ya urudiaji na dhamira ya tamaa na maadili

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 302) urudiaji unaweza pia kuwa uradidi. Ni istilahi inayotumiwa kuelezea sifa za kurudiwarudiwa kwa neno au sehemu ya neno. Ni sifa ambayo hupatikana katika mnyambuliko wa maneno. Mbinu hii inapotumiwa huzua athari kubwa ya kihisia. Mwandishi wa riwaya hii ameitumia ili kutimiza maelezo haya ya uzuaji wa hisia katika kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa. Kwa mfano, Omolo alikataa kutawaliwa na tamaa ya mapenzi, Queen alipojaribu kumshawishi wafanye mapenzi ya mwili. Hii ilimfanya atoke na kwenda zake. Neno 'hapo' limerudiwa kusisitiza namna alivyokataa. Hakupoteza muda kukataa. Tunaelezwa: "Queen alipojaribu kumshawishi kwenye tendo lile, Omolo aliondoka hapo hapo na kuelekea kwake. "(uk. 53).

Dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa wakati Queen anatamani wafanye mapenzi na Omolo anakataa. Huenda Queen anayetamani wafanye mapenzi anajua kuwa ana Ukimwi. Naye Omolo anayekataa kushiriki tendo la ngono, anahisi hakuwa ameambukizwa. Omolo anakataa kufanya mapenzi ya mwili tena kwa sababu anajiheshimu. Kukataa huku kunadhihirisha kuwa ni maadili kukataa. Mwandishi anakemea tabia potovu ya Queen isiyo na maadili. Kila anapokutana na Omolo anataka wafanye mahaba. Kwa mujibu wa nadharia ya maadili, Queen alikosa maadili. Si wa kuigwa kuhusu tendo la ngono. Omolo ana maadili ya kupigiwa mfano kuhusu tendo la ngono kwa vile anagadhibika anapokumbuka walivyofanya mapenzi na Queen kisha mpira wa kondomu ukachanika. Anaonekana kutamauka na pia kuuchukia ugonjwa wa Ukimwi kwa kurudia neno 'Ukimwi'. Anarudia neno hili kuashiria jinsi ni ungonjwa hatari na wa kuogofya (uk.101).

Tena, uradidi umetumiwa katika riwaya hii kuonyesha athari itokanayo na tamaa. Tamaa inaathiri jamii. Kwa mfano, Grace anapoenda kumtembelea dadake, Tabu, anamwona akilia. Alikuwa na uchungu wa kuambukizwa Ukimwi. Anajuta na kulia. Anarudia neno 'Ooii'. Hii inaashiria amelemewa na mawazo na anajuta kuambukizwa Ukimwi. Kilio hiki kinamfanya Grace kuwa na huzuni kisha anamwita mara kadhaa. Anarudia neno 'dada' kumbembeleza na pia kuonyesha

uhusiano wa karibu kati yao na hisia zake kumhusu. Hali ya Grace kurudia kumwita huku anasalia kimya, inaashiria Tabu kutamauka. Hana furaha na anajuta. Hofu aliyo nayo inatokana na tamaa ya mumewe kufanya mapenzi ovyoovyo na wanawake wengine. Hii basi, ni ukosefu wa maadili (uk. 57).

Ni bayana kwamba, Ngoma hana maadili ndiyo sababu anamwambukiza mkewe, ugonjwa huu. Kama angekuwa na maadili na kuheshimu ndoa yao, basi huenda hangeambukizwa na kisha kumwambukiza mkewe ugonjwa wa ukimwi. Kwa vile Ngoma hana maadili, inaonyesha kwamba ana upungufu fulani, si wa kuigwa..

Tena, mwandishi ameweza kutumia mbinu hii kuelezea kifo cha Tabu ili kufikia malengo ya kusisimua hisia za hadhira ya wasomaji. Anasema:

> "Kifo hiki kilimkumbusha Mzee Loti msiba wa Bibi Helena, mke wake wa kwanza, ambaye aliyemzaa Tabu. Kilimkumbusha majonzi makubwa. (uk.340).

Katika dondoo hili, neno 'kilimkumbusha' limerudiwa kusisitiza hisia alizokuwa nazo Mzee Loti kuhusu kifo cha binti yake. Aliweza kutafakari majonzi aliyokuwa naye mkewe alipoaga. Tamaa ya Ngoma kufanya mapenzi na wanawake wangonjwa na kisha kumwambukiza Tabu, inagadhabisha. Mzee Loti anahuzunika sana Tabu anapokufa kutokana na ugonjwa ambao chanzo chake ni tamaa ya mapenzi. Kurudiwa kwa neno hili kuna maana kwamba, Mzee Loti ana majonzi sawa na wakati mkewe alipokufa. Ngoma alikosea kumwambukiza Tabu ugonjwa kwani asemavyo I. Kant, kila mtu ana wajibu wa kimaadili, ya kuheshimu hadhi na thamani yake na wenzake. Ngoma hakujiheshimu na pia kuheshimu Tabu. Ndiyo maana anajihusisha na mapenzi nje ya ndoa bila kujali na kupelekea kuambukizwa ugonjwa. Hii si maadili. Dhamira ya tamaa na athari zake imekuzwa na kuendelezwa kutumia mbinu hii kwani inasisimua hisia ya wasomaji kuhusu tukio hili.

Aidha, jina 'Ngoma' limerudiwa mara kadhaa wakati Mpemba anapoelezea uhusiano wa Ngoma na Queen. Anasema Queen ana *mkanda wa jeshi.* Anawaeleza wenzake namna Tabu alizozana na Ngoma kwa kumpata akistarehe na Queen katika *Kanga Moja Club* na kumwambukiza Ukimwi. Hii ilimliza Tabu nao watoto wakaanza kulia pia. Jina 'Ngoma' limekaririwa kusisitiza kwamba yeye ndiye alikuwa na tamaa na ndiye chanzo cha matatizo yote katika familia yake. Jina 'Ngoma' limerudiwa ili kusisimua na kuteka hisia kuhusu namna Ngoma alivyokosa maadili. Ngoma

alikosa uvumilivu na utoshelezaji wa kibinafsi, hakuwa na maadili; kama asemavyo Kant katika nadharia ya maadili kwamba, mtu asiye mvumilivu wala kutotosheka, hana maadili. Naye Tabu, kwa kuwa mvumilivu na kutosheka na mumewe, ana maadili. Dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa kupitia mbinu hii ya urudiaji kwa kuonyesha ukosefu wa uvumilivu na utoshelevu (uk.14).

Tabu amesawiriwa akikariri neno 'Acha' ili kusisitiza namna alivyomkataza Ngoma kujiepusha na mapenzi ya kiholela. Ngoma hakumsikiza, badala yake alijiona rijali akivamia kila aina ya mwanamke. Pia, neno 'tujadiliane' limerudiwarudiwa kusisitiza namna Tabu alivyokataa ombi la Ngoma la kuketi ili wazungumze, waelewane na watatue mzozo kuhusu uvumi wa kumwambukiza Ukimwi. Vilevile, 'Tujiadiliane' limerudiwa kumkejeli Ngoma kwamba, hapo mwanzo alikataa kumsikiza na tayari kosa limefanyika na sasa hapakuwa na haja ya kujadili lolote. Tabia ya kuwatamani wanawake wengi, inamfanya kuambukizwa Ukimwi kisha kumwambukiza Tabu. Hii si maadili. Kwa upande mwingine, Tabu kukataa kumsikiza Ngoma inakuwa ni maadili kwani Tabu ni mwaminifu, lakini mumewe anamtelekeza na kumwambukiza Ukimwi. Kwa vile chanzo cha maafa haya ni tamaa, neno 'Acha' limerudiwa ili kusisitiza namna Tabu anavyoonya mumewe kuhusu tabia hasi, na anakosa kusikia (uk. 27).

Pia neno 'tende' limekaririwa kuonyesha matokeo ya tamaa ya mapenzi yenye Ngoma alikuwa nayo. Neno hili limerudiwarudiwa kuashiria mateso au matatizo ambayo Ngoma anaanza kupitia kutokana na athari ya kuambukizwa Ukimwi. Urudiaji huu unasisitiza namna hali ya Ngoma ilivyo mbaya. Mwandishi amekariri neno 'tende' kusisitiza kwamba, kitu kizuri/ kitamu kikitumiwa vibaya kina madhara. Kwa mujibu wa Baumgarten katika nadharia ya maadili ni kwamba, hakuna kitu kinachoweza kuwa kizuri bila maadili. Ngoma kufanya mapenzi ambayo ni kitu kizuri bila tahadhari, ilikuwa si maadili na ndio sababu imemsababishia majuto (uk.33).

Isitoshe, mwandishi anakariri sehemu ya neno 'aliyelileta' ili kuonyesha na kutilia mkazo lawama anazolimbikiziwa Ngoma kwa kumwambukiza Tabu Ukimwi. Pia, inaonyesha kwamba, Tabu si salama tena. Mkufya amefanya hivyo ili kudhibitisha kwamba si mwingine bali ni Ngoma aliyemwambukiza Tabu Ukimwi. Tabia ya Ngoma kukosa maadili na kuheshimu ndoa yake, inampelekea Tabu kuambukizwa Ukimwi. Hali hii inazua chuki, huzuni na wasiwasi katika familia yake. Kwa mfano, Juma ambaye ni mtoto wao, analia kwa kuhuzunishwa na habari hii. Hampendi babake. Aidha, Tabu anatishia kuondoka na kwenda kwao. Mwandishi ametumia mbinu hii ya

urudiaji ili kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa kwa kuonyesha athari zake katika jamii (uk.37).

Vilevile, neno ‘kumi’ limerudiwa kuashiria namna Ngoma ana tamaa kubwa ya unywaji wa pombe. Unywaji wa pombe kiasi hiki si uadilifu. Tunaweza kusema kwamba, kunywa pombe kupita kiasi na kukosa nidhamu ameiga kutoka mtaa wa Tandika. Mawazo haya yanaweza kutiliwa mkazo kutoka kwa mawazo ya Jean Jacques Rousseau(1755) katika nadharia ya maadili kwamba, mtu huwa mzuri katika maisha ya kawaida isipokuwa huja kupotoshwa na jamii ambayo hufikiria kuwa imestaarabika. Ngoma anadhani akilewa sana na kucheza muziki katika baa ni ustaarabu. Hii ni kukosa maadili. Mwandishi wa riwaya hii, ameikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake katika jamii kupitia mbinu hii (uk.6 - 9).

Jina ‘Asha’ limerudiwa ili kutilia mkazo kwamba ni yeye Ngoma alikuwa akimgojea. Kwa mfano, Ngoma anamuuliza Rajabu ikiwa amemuona Asha kwani walikuwa wana miadi. Ngoma anakuwa na wasiwasi anapomkosa Asha kwa sababu ana tamaa ya kumpata. Ikiwa Asha angekosa kufika, Ngoma angemkosa. Tamaa ya Ngoma inamfanya akaidi onyo kutoka kwa Rajabu kwamba, Asha ana mume, Kisukuma. Rajabu akamtahadharisha kwamba, kuna siku Msafiri atakuja kumpiga. Lakini, ushauri wa Rajabu haumzuii Ngoma kumsubiri Asha. Anasema, yeye hufanya mahaba harakaharaka na kisha kuondoka. Kufanya hivi ni ukosefu wa maadili kwa vile Asha ana mume mwingine. Tunavyoona katika nadharia ya maadili ni kwamba, ili mtu aonekane mwema, ni lazima atende mema. Ngoma anafanya mapenzi na Asha ilhali ana mume na hii inadhihirisha kwamba, si mtu mwema (uk. 9).

Tena, neno ‘naumwa’ limerudiwa ili kusisitiza athari ya maumivu kwenye mwili wa Ngoma. Grace na Mashaka walipoenda hospitalini kumjulia hali, analalamika kwamba, alikuwa anahisi vibaya na afya yake inazidi kuzorota. Mwili ulikuwa kama mtu anayepigwapigwa. Uchungu aliokuwa nao, unatokana na athari ya tamaa. Neno hili limerudiwa ili kuonyesha makali ya ugonjwa huu. Mwandishi wa riwaya hii basi, anaikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa kwa kutumia mbinu hii ya urudiaji ili kurejelea anavyohisi Ngoma (uk. 274).

Sehemu ya maneno ‘wamchokoze’ na ‘wamfanyie’ yamerudiwarudiwa kuonyesha tabia ya Pendo na Chiku ya kumtamani Omolo. Wana tamaa ya mapenzi kwani wanatamani Omolo kufanya nao mahaba. Kiambishi ‘wa’ kinaashiria Pendo na Chiku na ‘m’ kinaashiria Omolo. Viambishi

vinaashiria jinsi Pendo na Chiku wanavyomtamani Omolo. Hali ya wawili hawa kumtaka Omolo kufanya nao mapenzi kwa wakati moja, si maadili. Ni bora kama mmoja wao anamwendea Omolo na kumshawishi wafanye naye mapenzi. Mkufya ameipiga vita tabia hii namna inavyodhihirishwa katika nadharia ya maadili kwamba, sanaa inafaa kuyafichua uozo katika jamii na kisha kuielekeza jamii kutenda mema kutumia njia za kulemea maovu. Hali ya mwandishi kurudiarudia sehemu ya maneno haya, ni kujaribu kuonyesha jinsi anavyokerwa na uozo huu na kutaka ukome. Kwa kutumia mbinu hii ya urudiaji wa maneno haya, dhamira ya tamaa na athari zake imekuzwa na kuendelezwa katika riwaya hii (uk. 6).

Tena, mwandishi amelikariri neno ‘hakujua’ kusisitiza kwamba Grace hakufahamu kuwa Ngoma ni mpenzi wa Queen. Aidha, neno hili limerudiwa kuonyesha kwamba, Grace hakuwa na habari kuwa Omolo alimfumania Ngoma kwa Queen. Urudiaji wa neno hili unasisitiza hali ya Grace kukosa kujua kuwepo uhusiano wa kimapenzi baina ya Queen na shemeji yake (Ngoma). Grace anachuliwa kuwa na maadili kwa vile, anamtahadharisha Omolo kuhusu Queen. Wazo kama hili linaungwa mkono katika nadharia ya maadili kwamba, kazi ya fasihi huwa na wahusika walio na mambo mema ambayo yanafaa kuigwa na pia wale wenye sifa mbaya za kuepukwa. Omolo alifaa kufuata ushauri wa Grace na kumwiga (uk.45).

Neno ‘mwenyewe’ limerudiwa wakati Chiku anazungumza na Omolo kuonyesha hisia na tamaa yake jinsi anavyotaka wafanye mapenzi na Omolo kwa vile yeye hula nyama yake. Anataka kulipa nyama aliyoila kutumia tendo la mapenzi. Tabia hii si maadili hata kidogo, kwa vile inasusha hadhi dhima ya ngono katika jamii. Mwandishi amesisitiza neno ‘mwenyewe’ ili kuadilisha jamii kuhusu ubaya wa wanawake kulipa chakula wanachokila kutumia ngono. Mwandishi ametumia mbinu hii kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa kwa kuonyesha namna watu wanavyochukulia ngono (uk. 75).

Vilevile, neno ‘alivyozidi’ limekaririwa ili kusisitiza namna Asha alivyoendelea kutazama picha ya ngono. Anazidi kutazama picha za ngono ambazo zinamsisimua na baadaye anaanza kumtekenya mzungu na kufanya naye mapenzi. Neno hili limerudiwa kuonyesha namna watu wengine huwa na tamaa ya kufanya mapenzi wanapotazama picha za tendo hilo. Mwandishi ametumia neno hili kuonyesha namna Asha anavyopata tamaa ya mapenzi. Tabia ya kumsisimua mzungu kwa kumtekenya ili wafanye mahaba na kisha alipwe, si maadili kwani inaathari zake katika jamii. Uozo huu umefichuliwa katika nadharia ya maadili inayosisitiza kwamba sanaa

inafaa kuyafichua uozo katika jamii na kisha kuielekeza jamii kutenda mema kutumia njia za kulemea maovu. Njia ya jamii  kuepuka uovu huu ni kuwa na maadili (uk. 89).

Hali ya Mashaka kuwa na tamaa ya mali ya Ngoma inatiliwa mkazo wakati neno ‘mirathi’ inaporudiwa. Kurudiwa huku kunaashiria kwamba kuna tatizo kubwa kati ya Ngoma na jamaa yake kuhusu mali. Mashaka anataka Ngoma afe kwanza ndipo wajadili na jamaa yake namna ya kurithi mali yake. Tabia hii si kubalifu kwani jamaa ya Ngoma wana tamaa ya kunyakua mali yake. Hii si maadili. Mwandishi ametumia mbinu ya urudiaji ili kusisitiza neno ‘mirathi’ kwa lengo la kuteka makini ya wasomaji kuhusu Mashaka na urithi na namna anavyotaka mali ya kakake. Kupitia mbinu hii, mwandishi ameweza kuikuza na kuiendeleza dhamira ya tamaa na athari zake katika jamii kwa kuipiga vita tamaa ya aina hii (uk.275). Mbinu hii haijatumiwa katika riwaya ya *Paradiso* ili kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa.

### 2.6.3 Uzungumzi nafsi

Queen anawaza na kujizungumzia kuhusu maisha na kifo. Anajisemea kwamba kifo hakina fumbo na kuamini kwamba, ni jambo la lazima kwani kila kiumbe kilicho na uhai kuna siku kitakufa. Anajielezea kwamba, mwanzo wa kifo huwa wakati mtu anapozaliwa na kuna siku lazima watu watakufa. Mtu anapokufa mapema au baadaye yote ni sawa kwani bado ni kifo. Hali ya kuwaza sana kuhusu kifo ni ishara kwamba, Queen ametamauka. Chanzo cha kupoteza matumaini kuhusu maisha ni tamaa ya ngono. Anajitoa uhai kwa kuchanganya pombe ya *Brandy* na maji ya machungwa kisha kumimina vidonge vyote kumi na tatu na kuvimeza. Hali ya kutamauka na kujitoa uhai si maadili. Kwa mujibu wa nadharia ya maadili, funzo ambayo msomaji anaweza kupata ni kwamba, tamaa si kitu kizuri kwa vile humfanya mtu kuhitimisha maisha yake (uk.170-171).

Vilevile, mbinu ya uzungumzi nafsia imetumiwa wakati mamake Queen, Bibi Kimaro anapolalamika kuhusu yaliyosemwa na Queen kuhusu mirathi kwa vile hayakuwa na umuhimu wowote kwake kwa vile watu wake wote wamekufa na kumwacha na Dadii peke yake. Kupitia mbinu hii, tunaona uchungu alio nao Bi. Kimaro kwa sababu ya kifo cha Queen. Bi. Kimaro hana tamaa ya mali. Hali hii inachukuliwa kuwa ana maadili kwani alichokuwa na haja nacho ni uhai wa Queen na mume wake. Tukirejelea mawazo ya Vaughn (2008) katika nadharia ya maadili kwamba, maadili husaidia kuongoza matendo, kufasili thamana ya mwanadamu na pia sheria

zinazomwongoza, tunaona matendo ya Bi. Kimaro yana thamani kwa vile anakataa kuongozwa na tamaa ya kurithi pesa / mali kwa sababu ana maadili. Dhamira ya tamaa, imekuzwa na kuendelezwa kutumia mbinu hii kwa vile Bi. Kimaro anajali uhai wa watu wake na wala si mali (uk. 179). Vilevile, mbinu hii imetumiwa lakini si sana katika riwaya ya *Paradiso* ili kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake.

### *2.7* Matumizi ya Mbinu za Uandishi -/ Lugha/ Kunga nyingine Katika *Paradiso*

#### 2.7.1 Mbinu ya urudiaji na dhamira ya tamaa na maadili

Wamitila (2003:307) anasema kwamba, urudiaji ni hali ya kulisema jambo mara kadha wa kadha. Hufanya hivyo, kimsingi kuhakikisha kuwa anayerudiarudia maneno anayakumbuka mambo fulani. Umuhimu wa mbinu hii ikitumiwa ni kule mwandishi kutaka kuliweka jambo wazi au kusisitiza jambo. Sawa na Mkufya, Habwe ameitumia mbinu hii kwa kurudia maneno fulani. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kutaka kusisitiza jambo fulani. Kwa mfano: "Kovu lake ni lake. Kwani ni la nani? Watu wengi wana makovu ati." (uk.65).

Mwandishi anaelezea namna Musa alikuwa akionyesha hali ya kutojali kuwa na kovu baada ya kujeruhiwa kwa sababu ya tamaa. Anaonyesha hali ya kutojali kuwa na kovu kwani hata kama imepatikana kwa kupigwa au namna ingine, bado ni sawa tu. Urudiaji pia umetumiwa hapa kusisitiza jambo hasa la kukataa. Mathalan: "… Hatutaki utangetange kama mwehu. Mara utaenda na wazungu, mara Waafrika, mara Wahindi…" (uk.73).

Neno 'mara' limerudiwa ili kusisitiza hali ya Joshua kuchukizwa na mienendo ya binti yake. 'Mara' limetumiwa hapa, kuonyesha wakati mwingine. Mbinu hii imetumiwa kuelezea namna ya kuchukizwa na tamaa ya Nice kwa vile si maadili kwa Nice kufanya hivyo.

Habwe amerudia jina kama Zuhra. Ametumia mbinu hii ili kuteka fikra za wasomaji kuhusu wake wa Mango. Ni bayana kwamba, Mango ana wake wengi kama tano na hawara mmoja, Sakina. Ni tamaa kubwa, mtu mmoja kuwa na wake wengi kiasi hicho na hawezi kuwakimu. Ni ukosefu wa maadili. Gitobu (2014: 9) katika nadharia ya maadili anasema kwamba, nadharia ya maadili huchanganua kilichomo katika vitendo ambavyo huvifanya vitendo hivyo kuwa sawa ama kutokuwa sawa. Kitendo cha Mango kuwa na wake wengi ni tamaa, na si sawa (uk. 1).

Isitoshe, neno ‘wewe’ limerudiwa kuonyesha namna Sakina na Zuhra wanavyotoleana vitisho. Neno hili vilevile limekaririwa kusisitiza jinsi walivyo na msimamo mkali. Hii ni kwa sababu ya tamaa ya kunyanganyana mwanamume (Mango). Tamaa kati ya wawili hawa imekuzwa na kuendelezwa kutumia neno ‘wewe’ ambalo pia linaonyesha madharau kati yao. Hali ya wanawake kuishi wakichukiana si maadili. Watu wanapaswa kuishi maisha ya maadili kama wasemavyo, Plato na Tolstoy katika nadharia ya maadili (uk. 10).

Pia, kuna kurudiwa kwa jina ‘Zuhra’ ili kuonyesha maovu anayotenda. Tamaa ya Zuhra kuolewa na Mango inamfanya Apondi ambaye ni mke wa kwanza wa Mango kuhisi kwamba Zuhra amemnyanganya bwana. Kurudiwa kwa jina ‘Zuhra’ inasisitiza kwamba ni yeye aliye na makosa kuruhusu Mango kumuoa. Kitendo hiki kinaonekana kumkera Apondi kwani anahisi kuwa amempokonya mume. Kama tunavyoona katika nadharia ya maadili ni kwamba, mtu mwema anapaswa kutenda mema. Zuhra hakumtendea Apondi vizuri, basi yeye si mwema tena hana maadili. Habwe ameikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake katika jamii kutumia mbinu hii ya urudiaji wa jina ‘Zuhra’ (uk. 13).

Mwandishi ametumia neno ‘huo’ sana ili kusisitiza aina ya chakula walacho Apondi na wanawe kule Bunyala. Kurudia kwa neno hili kunasisitiza namna kunasinya kula chakula cha aina moja. Apondi anamlaumu mumewe, kwa kosa la kujilimbikizia wanawake ilhali hana uwezo wa kuwatunza. Kwa mfano, ana wanawake Bunyala na wengine Mombasa. Tabia hii inamuudhi sana Apondi na hata anatishia kumtia Mango adabu. Njogu na Chimerah wanasema kwamba, katika nadharia ya maadili, kuna aina mbili za tabia: tabia chanya na tabia hasi. Mtu ataiga tabia mzuri endapo atampata yule wa kumwelekeza kutenda mema ikiwa angali mchanga. Kulingana na fasiri yetu, Mango alikuwa na tabia hasi kuwaoa wake wengi pasi na uwezo wa kuwakimu kwa sababu alikosa mtu wa kumwelekeza. Na hii si maadili (uk. 15).

Neno ‘linawezekana’ pia limerudiwa kuonyesha hali ya uwezekano wa jambo fulani (tiba) kutendwa. Kabwere anakubali kwamba tiba ya mgonjwa husika inaweza kufanyika na apone mradi walipe damu ya mtu, ng’ombe wawili na shilingi elfu ishirini. Hii ni tamaa kubwa ya kutaka kujinufaisha na vitu vya watu wengine na pia kuharibu uhai kwa kutaka damu ya mtu. Hivyo basi, si maadili. Mwandishi anadhamiria kuonyesha namna tamaa inapelekea mtu kutaka pesa / mali kutumia kila njia

Hough katika nadharia ya maadili anasema kwamba, fasihi ina mchango mkubwa katika matendo pia thamani ya binadamu. Mawazo ya Hough yatatusaidia kuwa macho tunapohitaji usaidizi kutoka kwa waganga kwa vile wengi wao ni waongo na tusipochukua tahadhari tunaweza kupata hasara kama kuua mtu ili tukidhi mahitaji yatu. Matendo yetu yanafaa kuwa mema na muhimu (uk. 18).

Vilevile, kuna urudiaji wa sehemu ya neno 'asi-'kwa mfano, 'asioe' na 'asiweke'. Mwandishi ametumia mbinu hii kuonyesha msisitizo wa wazee wa kanisa kupinga hali ya Mango kuwa na wanawake wengi kwa sababu ya tamaa. Kama kiongozi wa kanisa, tabia ya Mango kuwa na wanawake wengi, hairidhishi na pia si adilifu kwa jamii. Wazee wanamtaka kuwaacha wake wengine na kusalia na mmoja kwa sababu, ndoa ya mke mmoja na mume mmoja ina mapezi kamili, na hii ndiyo maadili ya kanisa (uk.20).

Kuna urudiaji wa neno 'wako' ili kusisitiza tamaa ya Mango ya kuwa na wake wengi. Zuhra anarudia neno hili ili kuonyesha namna inasikitisha Mango kuwa na wake wengi ambao haieleweki yupi ni mke wake halali. Hali hii inaweza kuchukuliwa kuwa si maadili kwani atawafunza watu wengine tabia hasi (uk. 22).

Tena, neno 'bila' limekaririwa ili kusisitiza na kuonyesha namna Joshua alivyokuwa alipokutana na Lona. Joshua akiwa anasaka kazi mjini, alikuwa hana chochote. Hali hii ya umaskini inamfanya Lona kushauriana na mumewe (Mganga) ili waweze kumsaidia Joshua. Wanafikiana kuishi naye katika boma moja. Baadaye, tamaa inawafanya kujihusisha na mapenzi kwa njia ya siri. Tendo hili linaendelea kwa muda bila Mganga kujua. Aidha, kukariri kwa neno hili linasisitiza hali ya kusikitisha kuhusu maisha ya awali ya Joshua. Alikuwa maskini. Hali ya kufanya mapenzi na Lona ilhali Lona ni mke wa Mganga, si maadili. Uamuzi wa Mganga kumuacha Lona aolewe na Joshua ni adilifu. Uamuzi kama huu ni sawa kwa vile anachotaka ni waishi kwa upendo kwa vile ni muhimu kama asemavyo, J. J. Rousseau katika nadharia ya maadili. Kwa upande mwingine, Lona kukataa ndoa yao na Mganga bila kukosewa, si adilifu na hii inaonyesha kwamba, yeye si mtu mwema (uk. 33).

Zuhra anapoulizwa na Michael kutoa habari zaidi kuhusu Tonje, anakariri jina 'Tonje'. Anasema alianzisha kanisa lake. Lengo kuu la kufanya hivyo ni tamaa ya kutaka awe kiongozi. Kurudiwa kwa jina hili inaweza kufasiriwa kwamba, Tonje alibadilika na kutenda kinyume na matarajio.

Zuhra anadokeza kwamba Mango na Tonje wanazozania washiriki. Badala ya kuifanya kanisa kuwa kitu kimoja, wanaigawanya kwa manufaa yao wenyewe. Kufanya hivyo si vizuri kwani kanisa inafaa kuwa mfano mwema wa kuleta watu pamoja. Wawili hawa hawana maadili kwa hivyo si watu wema. Kwa mujibu wa Rousseau, katika kitabu chake *Moral Education* (1762), mtu anaonekana mwema ikiwa anatenda mema. Kwa vile wawili hawa waliisambaratisha kanisa, hawakutenda mema, pia si wema (uk. 45).

Dhamira ya tamaa imeangaziwa sana wakati neno 'ndugu' linaporudiwa. Hii inaashiria namna tamaa ilivyo na madhara. Kurudiwa huku kunasisitiza jinsi uovu wa tamaa ulivyokita mizizi katika jamii hadi ndugu analala na ndugu. Tabia ya ndugu kufanya mapenzi na ndugu yake, si maadili na haikubaliwi katika jamii nyingi (uk. 123).

Pia, neno 'hana' limerudiwa kuonyesha bila. Baada ya Lona na Joshua kuhusika katika ajali ya barabarani, wanaaga dunia. Walipokuwa hai, walikuwa na tamaa ya kunyakua mali nyingi ya kanisa. Wanapoaga, wanaacha mali / pesa. Urudiaji wa neno hili 'hana' lina maana kwamba, ilikuwa kazi bure kujisumbua kuchukua vitu vya kanisa na sasa amekufa na kuviacha vyote katika ulimwengu. Tunaweza kusema kwamba, tamaa humfanya mtu kutaka vitu hata vile havitamfaa kwani aagapo, huviachia watu wasioweza kuvitunza (uk.134).

Lona ana tamaa ya kufanya mapenzi baada ya Joshua kumkataa. Anamwendea Boribori. Neno 'alimkatalia' limerudiwa kusisitiza msimamo mkali wa Boribori kukataa kufanya naye mapenzi ya mwili. Hatua ya Boribori inamkasirisha Lona na kisha anaende kumsingizia Boribori kwa Joshua kwamba anataka kumbaka. Tamaa ya mapenzi inaathiri uhusiano wao wakati Jushua anapomchukia binamuye, Boribori. Tendo la Lona kutaka kufanya mapenzi na Boribori kwa sababu ya tamaa, si vizuri wala adilifu kwa vile ni mke wa watu.

Kwa upande mwingine, ni adilifu kwa Boribori kukataa kufanya mapenzi na Lona ambaye ni mke wa askofu wake tena jamaa yake. Kulingana na msimamo wake, Boribori anachukuliwa kuwa mtu mwema. Hii ni maadili. Asemavyo Rousseau kwamba, nadharia ya maadili inasema ili mtu aonekane mwema, ni lazima atende mema. Boribori anatenda vyema kumkataa Lona (uk.135).

Neno 'alianza' limerudiwa kusisitiza hali ya Michael kuacha kumshughulikia Lydia. Mathalan, kwenda naye safarini hata kumletea zawadi. Michael alianza kumsusia Lydia kwa sababu alikuwa anamtamani Patricia. Tamaa yake inamfanya kujuta kwa nini akamuoa Lydia. Tunaweza kusema

kwamba, kitendo hiki cha kuanza kumkataa na kumnyima Lydia mapenzi kwa sababu ya kumtamani Patricia ni kukosa maadili. Baada ya Michael kufunga ndoa na Lydia, hakufaa kuwazia jambo kama hilo (uk. 150).

Habwe ametumia mbinu hii ya urudiaji kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake katika jamii kwa kurudia maneno anuwai sawa na alivyofanya Mkufya katika riwaya ya *Ua la Faraja*

**2.7.2 Matumizi ya Uzungumzi nafsi**

Mbinu hii imetumiwa kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa katika riwaya hii. Uzungumzi nafsi unatokea wakati wazee wa kanisa wanapomtaka Mango kuwa na mke mmoja wa ndoa na kuacha kuwa na kimada. Mango kujizugumzia ni dhihirisho kwamba, hayuko tayari kuacha tamaa ya kuwa na wake wengi. Jinsi anavyolalamika inaonyesha namna tamaa na athari zake ilivyoendelezwa. Kulingana na Mango si kosa kuwa na wake wengi. Kumwekea masharti ya kuwa na mke mmoja inamfanya kuwa tayari kuacha kulitumikia kanisa. Anajizungumzia na kushangazwa ikiwa wanawake hao hawahitaji waume. Anajiuliza wataenda wapi akiwataliki. Tunaona kwamba, hata wanawake wana tamaa na hii ni adilifu kwa vile, hataki kuwakosesha furaha. kwa mujibu wa Rousseau katika nadharia ya maadili anasema kwamba, jambo la maana katika maisha ya mwanadamu ni furaha ambayo msingi wake ni upendo. Mango anataka waishi kwa furaha na wake zake (uk.20).

Vilevile, mbinu hii inajitokeza wakati Patricia anajisemeza. Ana tamaa ya mapenzi ya kutaka Michael amuoe. Anawazia na kujiuliza maswali kwa nini anakosa kumpata mume mzuri wa kumuoa. Anashangaa kwa nini ni Lydia tu aliyebarikiwa kumpata mume mzuri na wala siye. Uzungumzi nafsi huu unaashiria ana tamaa ya kumpata mume mzuri. Tunaweza kusema kwamba, kuwaza na kutamani mume wa watu, si maadili. (uk. 145).

Tamaa inamfanya Lona kukosa kujali maisha ya washiriki wenzake na hata mwanawe, Nice, anayeharibikia kule ng’ambo. Anasema, kama Nice ameharibika hiyo haitamtatiza kwani kila mtu anaishi maisha yake. Kinachomfanya kuwa na mawazo kama haya ni kuwa na pesa nyingi na tamaa ya anasa. Anataka kujistarehesha na kutowajibika kwa sababu akiwa mzazi anawajibu wa kuhakikisha afanyacho mtoto wake. Lakini kukosa kufanya hivi ni ubinafsi na si maadili. Dhamira

ya tamaa imekuzwa kwa kuonyesha namna tamaa imemtawala Lona kiasi kwamba anajisahau (uk.131).

Michael ana tamaa ya mapenzi inayomsababishia mawazo mengi. Baada ya kufanya mahaba na Patricia na kumpachika mimba, anakosa kutulia. Anakumbwa na matatizo ya kiakili. Anajizungumzia huku akimlaumu Patricia kwamba, anajilazimisha kwake ilhali anajua alikuwa ameoa. Michael na Patricia hawaheshimu ndoa na hii si maadili hata kidogo. Tena, Michael kunuia kumwacha Patricia akiwa mja mzito si utu. Anapaswa kumsaidia Patricia kubeba mzigo wake. Dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa kutumia mbinu hii kwa vile inatuonyesha namna Michael alivyowaza kumshughulikia Patricia (uk. 170).

Tumeona kwamba, Habwe ameitumia mbinu hii kwa kiasi sawa na alivyofanya Mkufya ili kukuza na kuendeleza dhamira ya tamaa.

### 2.7.3 Matumizi ya Ishara

Katika riwaya hii, msitu umetumika kuashiria hali ya hatari au ubaya. Katika mkabala huu, neno 'msitu' katika *Paradiso* limetumiwa kunasibisha mazingira ya hatari likitazamwa katika muktadha wa tamaa na athari zake. Msitu umesawiri hali ya giza anamokuwa Joshua kuhusu maisha yake. Tamaa inamfanya kuchukuwa vitu vya kanisa na kuvifanya vyake. Anatumia pesa za kanisa kununulia shamba kubwa na pia kujenga nyumba ya kifahari. Anafanya yote haya kwa lengo la kuwawekea watoto wake msingi mzuri wa maisha. Baadaye, anagundua kwamba yote anayofanya ni kazi bure. Tunaarifiwa kwamba: "Aliingia msitu wa Langata akapata nafasi ya uga akakaa na kuanza kusikiliza nafsi yake kwa undani." (uk. 102-103). Katika dondoo hii, tunaona Joshua anagundua kwamba tamaa haina maana. Mwandishi ametumia mbinu hii ili kuweka wazi ukweli wa mambo kuhusu tamaa aliyokuwa nayo Joshua, "… dunia si chochote." (uk. 104). Msemo huu unadokeza kwamba, mtu asiwe na tamaa ya vitu vya ulimwengu kwani havina maana. Kutawaliwa na tamaa si maadili. Mbinu hii haijatumiwa na Mkufya, hasa kuendeleza dhamira ya tamaa na athari zake.

## 2.8 Hitimisho

Katika sehemu hii, tumeshughulikia jinsi dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Ili kuweka kila jambo wazi, tumechunguza suala hili kwa kutumia mada ndogo ndogo. Uchunguzi huu umetuwezesha kufafanua aina ya wahusika na sifa

zao, waovu na wema. Tumeonyesha jinsi wametumiwa ili kufanikisha dhamira ya tamaa katika kazi hizi. Tumekemea na kutweza matendo ya walio waovu huku tukiwapongeza na kukweza walio wema. Tumerejelea japo kwa ufupi, matumizi ya lugha, mbinu za uandishi na kunga zinginezo kwa vile hakuna jinsi mtu anaweza kushughulikia ukuzaji na uendelezaji wa dhamira ya tamaa pasi na kutaja viungo hivi. Kila mbinu imeshughulikiwa kwa kuitengea kila riwaya sehemu yake na kisha kulinganisha kwa ufupi namna mbinu hiyo imetumiwa na Mkufya na Habwe kuikuza na kuendeleza dhamira ya tamaa. Tumefanya hivyo ili kuweka wazi baadhi za njia ambazo waandishi hawa wawili wamezitumia kukuza na kuendeleza suala la tamaa katika riwaya zao. Tumeona kwamba, yaliyoangaziwa katika sehemu hii yanafanana na kutofautiana kwa kiwango kikubwa na katika riwaya zote mbili. Ufananishaji na utofautishaji huu umeshughulikiwa kwa kuipa kila riwaya sehemu yake.

# SURA YA TATU

# MATATIZO YANAYOSABABISHWA NA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia matatizo yanayotokana na tamaa katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*. Tumeeleza matatizo hayo yanasababishwa na nini na yanaiathiri jamii vipi katika kazi hizi. Kati ya matatizo tumeyaangazia ni ulevi katika familia, uongo na kusambaratika kwa familia, ulafi, uzinzi, magonjwa katika jamii na nyinginezo. Tumechagua, kueleza na kulinganisha baadhi ya matatizo haya kwa kushughulikia kazi zote pamoja. Vilevile, tumebaini uwiano na tofauti uliyo katika matatizo haya. Tumeweza kutumia nadharia ya maadili hasa mihimili zake na kuonyesha namna tamaa inavyoathiri wahusika katika riwaya hizi.

## *3.1* Tamaa na Matatizo yake katika *Ua la Faraja* na *Paradiso*

### 3.1.1 Matatizo ya Ulevi katika Familia

Ulevi, katika muktadha huu umechukuliwa kuwa ni matumizi ya kileo kinacholewesha kama pombe. Katika kazi ya *Ua la Faraja,* kuna wahusika kadhaa ambao wamejitumbukiza katika lindi la ulevi na kisha kujipata katika shida pamoja na aila yao. Wahusika hawa, kwa mfano ni Ngoma, Queen, Asha, Msafiri, Chiku na Pendo. Ngoma ni mfanyibiashara anayemiliki daladala tano za kuwasafirisha abiria. Licha ya kupata pesa nyingi kila siku kutokana na biashara hii ya magari anazitumia pesa hizo vibaya kushiriki anasa kama kuenda katika majumba ya ulevi na starehe. Katika sehemu hizi za burudani anatumia kiasi kikubwa cha pesa kujinunulia bia na hata kuwanunulia marafiki wake wanawake. Wanaosherehekea pesa zake ni Pendo, Chiku, Asha na Queen. Pendo na Chiku wakiwa kama wahudumu wa pale *Malaika bar,* wana mazoea ya kumhadaa punde anapowasili *Malaika bar*. Ngoma anatumia pesa zake nyingi kuwanunulia pombe na nyama na kuitelekeza familia yake. Mara nyingi anakunywa zaidi ya chupa sita ya bia kila siku. Tabu, mkewe, anasalia nyumbani bila pesa za masurufu na hata za kununulia nguo safi za kuvaa. Hali hii inamlazimisha Tabu kuanzisha biashara kidogo ya kuuza vitu vya matumizi kama vile vitunguu, mboga na viazi ili kupata pesa ya kuitunza familia yake. Katika mazungumzo haya tunapata taswira namna Ngoma anavyojihusisha na wanawake:

Ngoma alimuuliza Rajabu, "E- bwana hujamwona Asha leo?"

"Asha yupi?"

"Asha kibonge."

"Hapana. Kwani vipi?" Rajabu aliuliza.

"Nilikuwa na ahadi naye tukutane hapa. Sijui vipi kuchelewa…!" (uk.8).

Kulingana na dondoo hili, Mzee Ngoma ana miadi ya kukutana na Asha katika ukumbi wa *Malaika bar*. Ni katika maeneo kama haya anatumia pesa zake kwa wingi kununua pombe na hata chakula. Baada ya kunywa pombe, kula na kuzungumza, mengine yangefuata kama vile kushiriki ngono. Anasalia mlevi huku anazini na wanawake wagonjwa wa Ukimwi kama Queen anayemwambukiza virusi vya Ukimwi. Hali hii inazua mgogoro mkubwa katika ndoa yao. Hii ni baada ya kujulikana bayana kuwa Ngoma anaugua Ukimwi na kamwambukiza Tabu. Hali hii inawaathiri watoto wao. Kwa mfano, Juma na Aisha ambao walisikia wakizozana usiku kuhusu uambukizwaji wa ugonjwa huu. Familia ya Ngoma inakumbwa na ukosefu wa furaha kwa sababu ya yeye kukosa kuwa muadilifu maishani. Hili linafaa kuwa funzo chanya kwetu sote; kuwa tunapaswa kujiepusha kujihusisha na aina hii ya maisha ili familia isipate athari hasi. Aidha, kutokana na mlevi mvumi, Mpemba, tunapata mambo mengi kuhusu afya ya Queen na Ngoma:

"E jama ee! Mwajua kwamba Queen amepatwa na *mkanda wa jeshi*…

jana mke wangu alihadithiwa na mke wa jirani yake Ngoma…" (uk. 14).

Tueleavyo, Ugonjwa wa virusi vya Ukimwi ni tishio kubwa kwa maisha ya binadamu ulimwengu mzima. Kwa mujibu wa Serwadda (1985) maradhi ya UKIMWI yalipata kutambulika katika eneo la Afrika Mashariki katika miaka ya 1980. Nchini Uganda kwa mfano, ulitambuliwa mnamo mwaka wa 1982, Tanzania mwaka wa 1983, nayo nchini Kenya mwaka wa 1984. Kufikia mwaka wa 1999, ungonjwa wa Ukimwi ulikuwa umeangamiza watu wengi na kupelekea kutangazwa kuwa janga hatari la kitaifa.

Kwa mujibu wa UNAIDS (2014), takribani watu milioni 35 ulimwenguni walikuwa wanaishi na virusi vya ugonjwa huu hatari. Kutoka mwaka wa 2001, kumekuwa na ongezeko la idadi ya waathiriwa kufikia kiwango cha watu milioni 29.8. Kati ya ongezeko hili, asilimia 68 ya wanaoambukizwa ni watu wa bara la Afrika. Asilimia 40 ya wale wanaoambukizwa wakiwa ni vijana wenye umri wa miaka 25.

Kuna changamoto chungu nzima zinazoambatana na maradhi ya UKIMWI. Mtu anapopatikana na virusi vya ugonjwa huu huwa ni jambo la kusikitisha. Watu wengine wanakataa kukubali hali yao na kisha kuendelea kufanya mapenzi pasipo na kinga huku wakiwaambukizia wenzao. Kwa mfano, Queen anamwambukizia Ngoma, naye Mzee Ngoma akamwambukiza mkewe na Asha. Mwandishi wa kazi hii, anatumia barua ya Queen kutuonyesha athari ya makali wa ugonjwa huu. Queen anamwandikia Omolo, akimweleza jinsi mhanga wa Ukimwi hukumbwa na upweke. Mtu akiwa anaugua ugonjwa huu, watu humtoroka na kumwacha peke yake. Mgonjwa huona ugumu kuendelea kuishi na mwisho hujitoa uhai. Tumeona katika barua hii kwamba, Queen anajitoa uhai na kusema, "Nimeamua kuumaliza huu mchezo." (uk.177).

Aidha, mgonjwa huipa jamaa yake shida na uchungu wa muda mrefu kama wanavyofanya Queen, Ngoma na hata Tabu. Ngoma ana mazoea ya kurejea nyumbani huku akiwa mlevi. Watoto wake wachanga hawapati nafasi ya kumwona. Ulevi unamfanya mkali kiasi cha kumnyima Tabu haki ya mapenzi. Hali hii inapelekea Tabu kwenda kwao kwa wazazi wake na hata kutalikiwa. Juma naye anaenda kwa babuye ili aweze kusomea huko kwani ako tayari kakosana na babake kwa kukosa kufuata kanuni za dini ya Kiislamu.

Tumeona kwamba ulevi umeifanya familia ya Ngoma kukosa kupata mahitaji muhimu ya kujikimu katika maisha kama vile, nguo, vyakula na hata mapenzi. Tamaa ya ulevi inamfanya kutumia pesa nyingi kiholela kununua pombe na ndipo anaisahau familia yake. Matokeo ya hali hii ni kuwa anadharauliwa na watoto wake na hata watu wengine katika jamii. Ulevi unamsukuma kuwa na uchu wa wanawake na kuonana nao kimwili pasi na kinga. Mwishowe, anamwambukiza mkewe virusi vya ugonjwa hatari wa ukimwi. Kitendo hiki kinapojulikana, kinasababisha majonzi na kutoelewana katika familia. Anasa za Ngoma zinazua vifo; naye anaaga dunia, wakati Tabu anafuata baadaye watoto wao wakisalia mayatima.

Queen pia ni mlevi hali inayomfanya kushiriki ngono na wanaume bila kinga. Kitendo hiki kinamweka katika hali hatari ya kuambukizwa virusi vya Ukimwi. Katika utafiti huu tulibaini kuwa alipokuwa mzima, hakuweza kuwasaidia mamake wala jamaa zake. Hii ni kwa sababu aliikumbatia anasa; hata akasahau kuolewa. Anaugua, na kumwia mamake mzigo mzito kama nanga na baada ya kifo chake, mamake anakumbwa na simanzi si haba:

> Bibi Kimaro akaanza tena kulia akila, "Nyumba itasaidia nini? Pesa za nini?

Mimi namtaka mwanangu jamani miimi ee - Uuuwi!” (uk. 179).

Kulingana na dondoo hili, ni bayana kwamba Queen, alikuwa amekaa muda bila kukutana na mamake. Kifo chake kinamwacha mamake na upweke mkubwa. Kwa mujibu wa Rono (2013), ulevi humfanya mtu kukosa kuelewana na wenzake, kukosa heshima, kutowajibika na pia kuonekana zuzu na juha katika jamii. Tumeona kwamba mtu yeyote anayeshiriki ulevi wa kupindukia, huwa katika hatari ya kuhusishwa na sifa hizi hasi kwani mara nyingi walevi hushindwa kutekeleza wajibu wao na hatimaye, kurudisha maendeleo ya jamii nyuma. Kwa mfano, Ngoma anashindwa kutekeleza wajibu wake kuwafunza wana wake maadili ya kushika dini wakiwa wachanga, kuwanunulia nguo nzuri na hata kumpa mkewe pesa za masurufu. Hii ni kwa sababu anatumia pesa zake nyingi na muda wake mwingi kushiriki ulevi.

Katika *Paradiso,* Lydia anakuwa mlevi na kumjibu Micheal vibaya na kwa madharau. Michael si mnywaji wa pombe, si mlevi. Anapomkaribia Lydia na kuhisi harufu ya kileo, anashangazwa si haba. Anapotaka kujua akiwa amelewa, anaitika kwa bezo kwamba amekunywa na wala hakuwa mlevi (uk. 164 -165).

Ulevi humfanya mtu amkosee mwenzake heshima hasa ikiwa mwenzake hajalewa. Kwa mfano, Lydia anamkosea Machael na kumweleza kwa dharau afanye alitakalo. Hii ni kama kumdunisha. Aidha tunaona ulevi ukimtawala Lydia na kumchochea Michael kutenda asichotaka kutenda. Kwa mfano, anamzindua hadi wanagombana. Habwe anatoa taswira inayotisha ya Lydia kuzua vurugu kwa kumshika Michael ukosi:

> “Alipoona Michael hamsikilizi alikwenda kumshika ukosi. Michael
> alijaribu kujitoa mikononi mwake asiweze…” (uk. 165).

Tumeona namna ulevi unaweza kumfanya mtu kuua bila kutarajia. Ulevi wa Lydia unamfanya, mumewe kupandwa na hasira kisha kumsukuma ukutani na kugota. Anakigota kichwa chake kama avunjaye kile cha nyoka. Anamwinua juu na kisha kumrusha chini na mara kumputa chini. Kisha Lydia anashindwa hata kulia. Hatimaye, tunapata taswira ya kusikitisha sana kuhusu majuto anayopata Michael kufuatia matokeo ya ugomvi baina yake na Lydia ambayo chanzo chake ni ulevi. Anajuta na kulia, “*Mungu wangu nisamehe nimemuua mke wangu*.” (uk.161). Anashikwa na kiwewe baada ya Lydia kuzirai. Tena, ugomvi ambao chimbukole ni ulevi unampa shughuli ambazo hakuwa amenuia kuwa nazo kama vile kuzirai kwa Lydia kunamlazimu kumpeleka

hospitali akisaidiwa na majirani. Hata baada ya kurudi nyumbani, anachukuliwa na askari polisi na kupelekwa katika msitu wa Ngong inayoashiria mahali hatari na kuhojiwa kuhusu yaliyopelekea kitendo hicho.

Vilevile katika matanga ya Apondi, tunamshuhudia Mango akilazimishwa kufika katika kikao cha wazee ili atangulize kunywa pombe kidogo kama ishara ya kutimiza mila na desturi za Wanyala. Anatatizika kuhusu jambo hili kwani ilikuwa kinyume na imani ya dini yake; lakini wazee wanashikilia kwamba ni sharti atekeleze. Tunaambiwa kwamba: "Lakini walimwambia afungue kwa kuonja ili wazee wa rika lake waendelee kunywa…" (uk. 93).

Imani ya dini ya Mango inamzuia kushiriki katika kikao cha kubugia kileo na wazee wenzake kwani ni mkristo na hivyo basi anatengwa na wenzake. Kutokana na tabia na hulka ya Mango, tunaona kwamba, anatatizika kisaikolojia anaposhurutishwa kuonja pombe huku wazee wanajua fika kwamba ni haramu kufanya hivyo. Kutoshiriki kunywa pombe kunamtenganisha na wazee wenzake. Tulichukulia kwamba, kutoshiriki katika kikao hiki na wazee wenzake kunamfanya kuonekana kama mwanajamii aliye na upungufu fulani. Kwa mujibu wa Vaughn (2008), nadharia ya maadili inahusu kinachofanya tendo lolote lionekane zuri au baya. Tumeona unywaji wa pombe kupita kiasi kama tendo baya linalofaa kupigwa vita. Namna imesawiriwa katika riwaya zote mbili, athari ya ulevi ni sawa. Kwa mfano, inasababisha mafarakano, madharau, kutowajibika, matatizo ya kisaikolojia na mengineo.

### 3.1.2 Matatizo ya Udanganyifu na Kusambaratika kwa familia

Katika *Ua la Faraja*, baadhi ya wahusika ni wanadanganyifu. Mhusika Ngoma anasema uongo ili kutimiza haja yake kwa mkewe, Tabu. Anasema kwamba, walipoonana na Queen kimwili walitumia mpira wa kinga. Udanganyifu wa namna hii ni changamoto kuu katika ndoa kwani una athari hasi katika familia. Hali kama hii ni upotovu wa maadili katika jamii. Anasema uongo huku akifahamu fika kwamba alishiriki ngono na Queen pasi na mpira wa kuzuia virusi vya ugonjwa hatari wa Ukimwi:

> "Ngoma alipoulizwa vipi, akaambiwa hawara yake. Queen amepatwa na *mkanda wa jeshi.* Ndugu yetu , Ngoma, alijitetea lakini wapi! Mkewe alizidi kumshtumu na kumwaga chozi mpaka hata watoto wakaingilia kulia." (uk. 14).

Uongo wake unadhihirika wazi Queen anapoanza kuumwa. Anashikwa na kiwewe kisha anabadili mtindo wake wa maisha kama kuanza kufika nyumbani kwake mapema, kuasi kuenda katika sehemu za burudani na starehe, kunywa pombe, kuvuta sigara na hata kujihusisha na vimada wake wa awali, akawa mswalihina na kwenda msikitini mara kwa mara kusali. Si kama hapo mwanzoni Tabu, anapomuuliza sababu ya kuchelewa kufika nyumbani mapema, anatoa visingizio kwamba, walikuwa na jirani yake, Jaluo, wakinywa huku wakijadili biashara; hali inayopelekea kujisahau (uk. 24).

Tunaelewa fika kwamba, huu ni uongo kwani Ngoma hampendi Omolo kwa sababu yeye Omolo alimfumania na Queen. Kutokana na sababu hii, hakuna siku wanakaa katika meza moja wakinywa huku wakijadili lolote hasa kuhusu biashara. Ngoma anapenda sana kunywa pombe na rafikiye, Rajabu huku akijishughulisha na wanawake kama Queen, Asha, Pendo na Chiku.

Vilevile, uongo unamfanya kuzozana na mkewe, hatimaye ndoa yao inayumbishwa na kusambaratika. Tabu ni mstaarabu na ndiye anawalea watoto wao. Ni mke aliye na adabu kinyume na mumewe ambaye analewa chopi pamoja na kipusa wake, Queen hadi saa nne za usiku. Tulivyosoma:

> ‘Rajabu akachukua glasi. Akaijaza na kuinywa… kisha akasema, “Hapana ninamskitikia mke wake Ngoma. Yule mama ni mstaarabu sana. Ingawaje Mume ni mlevi wa kutupwa, yeye anawalea wanawe kwa adabu...” (uk. 15).

Ngoma hana heshima. Ndiye anasababisha matatizo yanayoikumba familia yake. Anakwenda kinyume na matakwa ya maadili ya kusema ukweli na kutenda haki. Mkewe anamuonya kila wakati ajiepushe na kuvamia kila mzoga wa kike anaoupata lakini masikioni ametia nta. Ni mwasherati aliyetambuliwa na kila mtu. Ni jambo la kusikitisha kwamba, anamwambukiza Tabu ugonjwa hatari wa Ukimwi ambao uliwafanya Nuru, Rahma, Juma, Aisha na Abu kusalia mayatima mapema. Mkewe mara nyingi aliteta kuhusu hulka yake hii (uk. 27).

Hata wanawe wanaufahamu uongo wake. Juma kwa mfano, anamchukia babake kwa sababu ya uongo. Anawatelekeza, huku akijihusisha na ulevi, uvutaji sigara, wanawake wengi na mzozo wa mara kwa mara, kutomjali Tabu na kupelekea afanye biashara za kupika vitumbua na chapati na pia kuuza genge la mboga ili waweze kujikimu. Hali hii inamfanya Juma kulia sana anaposikia kuwa babake amemwambukiza mamake Ukimwi.

Hatimaye, Juma anatawaliwa na mawazo mengi, chuki, hofu na hata hamu ya kulipiza kisasi kwa babake. Hali ya Tabu kuambukizwa ugonjwa wa Ukimwi, unamvunja Juma moyo kwani anajua fika kuwa hawezi kutimiza ndoto yake ya kumpa mamake maisha mazuri, kuona tabasamu yake na pia kupanguza machozi yake (uk. 34).

Tumeona kwamba mtu anaweza kulazimika kutumia uongo akiwa na lengo la kudumisha utulivu na mshikamano katika familia. Kwa mfano, Tabu anawadanganya wanawe kwamba mambo yote wanayoyasikia wanapokuwa wakizozana na mumewe huwa si ugomvi bali ni malumbano ya kawaida. Vilevile uongo unaweza kutumiwa ili kuleta maadili katika familia, hii inadhihirika tunapoelezwa kwamba:

> "Mama yao alikuja kuwatuliza na kuwadanganya kwamba yale waliyoyasikia hayakuwa kweli ila yalikuwa malumbano ya kawaida waliyozoea kati yake na baba yao. Watoto wakamwamini mama yao." (uk. 36).

Katika utafiti huu tunaweza kusema kwamba, udanganyifu unaweza kutumiwa ukiwa unalengo nzuri kama vile Tabu alivyodhamiria kuutumia. Hali ya kuwadanganya wanawe kwamba waliyoyasikia yalikuwa ni ugomvi wa kawaida ilinuia kuwatuliza na wamwamini ili kuwaondolea hofu na huzuni. Hali ya namna hii inaweza kuipa familia yake matumaini na vilevile furaha. Hata hivyo, si maadili mema uongo kutumiwa kama mazoea. Maoni yetu yanaweza kuungwa mkono na mhimili wa nadharia ya maadili kwamba, dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii. Mkufya kuitaka jamii kuishi kwa furaha alidhamiria kuijenga kimaadili. Katika riwaya ya *Paradiso*, Lona anatumia uongo kumsingizia Borobori kutaka kumbaka. Uongo huu unasababisha chuki kati ya Joshua na Boribori. Tatizo hili la uongo limetumiwa na Mkufya na Habwe kurejelea dhamira ya tamaa katika kazi zao.

### 3.1.3 Matatizo yanayotokana na Ulafi

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* kuna wahusika kadha wenye tabia ya ulafi. Hawa ni Ngoma, Pendo, Chiku, Mashaka, Kassim, Asha, Queen na Zito. Kila mmoja wao ni mlafi kwa namna yake.

Mhusika Ngoma ni mlafi wa kula chakula kingi na kupenda wanawake. Anapenda kula nyama na kunywa bia katika sehemu za burudani huku familia yake ikisalia kutaabika nyumbani.

Anafahamika kuwa na tabia ya kupenda ufahari kwani kila mara anataka kuonekana kuwa yeye ni bora kuliko watu wengine. Ili kutimiza ufahari wake, daima anaagiza bia kumi kwa kumaanisha bia moja na ishirini, kumaanisha mbili. Anapofika *Malaika Bar,* wachoma nyama wanamuuliza kiasi anachopenda kuchomewa. Hii ina maana kuwa ana mazoea ya kula nyama akinywa pombe na pia uwezo wa kulipa kiasi chenye angechomewa. Ulaji na unywaji wa bia kupita kiasi unakiuka maadili ya mtu mstaarabu kwa vile mtu hutumia pesa nyingi. Vitendo kama hivi humfanya mtu kuzembea kutekeleza majukumu na pia wajibu wake muhimu katika familia kama Ngoma anavyoshindwa.

Wahusika wengine walio na tabia ya ulafi japo hawana uwezo wa kununua vya kuliwa na kunyiwa, ni Pendo na Chiku. Wawili hawa wanajiegemeza kwa wateja wa *Malaika Bar* ili wapate kukidhi ulafi wao wa kula, kunywa na uchu wa kufanya ngono. Wakati Omolo anapoagiza chakula, wao pia wanajitia katika hesabu. Tabia kama hii ni kero kwa wateja (uk. 70).

Tunaweza kuchukulia kwamba, tabia ya Omolo ya kunyamaza na kutotaka mzaha kutoka kwa wanawake siku hiyo, ni kama amechoshwa na ulafi wa Pendo na Chiku. Tabia ya kuwaombaomba wateja chakula na kutaka kufanya ngono nao ni ulafi ambao unaenda kinyume na maadili ya jamii kwani unamfanya muombaji kuwa mzigo kwa anayeombwa (uk. 70).

Tumebaini kwamba, wateja wanapoombwa, hulazimika kugharamia chakula ambacho hawajapangia. Kwa mfano, Pendo anapomuuliza Omolo kuhusu nyama, Omolo analazimika kumweleza Yakobo kuwapa mishikaki ambayo angelipia yeye. Tumechukulia kwamba, ulafi wa namna hii, unaondoa ustaarabu na kupalilia ukosefu wa maadili katika jamii.

Vilevile tumeweza kuona kuwa tabia ya ulafi imekita mizizi sana katika jamii ya riwaya hii. Mashaka mathalan, pia ana tamaa ya chakula. Kitendo chake cha uroho kinaonekana katika matanga ya kakake, Ngoma anapoalika maombolezi ya siku tatu; yeye ni mlafi. Dosari ya kufanya hivi ni kwamba, ingewalazimu waliofiliwa kupata hasara zaidi kama vile kutumia pesa zaidi katika kununua vyakula vya kuwalisha waombolezaji. Kuongeza muda wa kuomboleza ni kuitwika familia imefiliwa mzigo wa gharama. Kama tunavyoona:

> "Mashaka alialika matanga ya siku tatu. Hayo hayakumsumbua Juma na hakutaka kujihusisha na uamuzi wa mahitaji au ununuzi." (uk. 303).

Tunaweza kuamba kuwa, tabia ya ulafi imekita mizizi hadi kwenye matanga na kuifanya jamii kupoteza maadili kwani palipo na majonzi, hapapaswi kuwa mahali pa kustarehe.

Vilevile, wanaume na wanawake ni walafi wa mapenzi. Ngoma, Queen, Pendo na Chiku wanapenda mapenzi. Ngoma ana wanawake marafiki kama Queen na Asha. Naye, Asha ana wengine kama Msafiri.

Vilevile, katika riwaya ya *Paradiso,* Habwe ameangazia aina tofauti tofauti za ulafi. Uroho wa namna hii unakinzana na matakwa ya dini. Kwa mfano, Apondi anapokufa, kunakuwepo na matanga. Mzee Okoth anamshurutisha Mango kuwapa ng’ombe wa kike wamchinje ili waombolezaji wapate kumla. Hata baada ya Mango kukataa na kuwashauri kwamba ana pesa zinazotosha kununua nyama ya kuwalisha, Chifu Mohamed Owaki anadinda kukubaliana na maoni yake. Chifu anasema kwamba, mila haikupaswa kufanywa hivyo. Kisha anatishia kumwadhibu kwa kumchapa viboko na hata kumwachia maiti ya marehemu mkewe kuizika mwenyewe. Anamkumbusha kuwa hata yeye, ni muumini Mwislamu na anafuata mila. Kwa sababu ya ulafi, Mango anatwikwa mzigo mwingine usiokubalika na dini yake. Ananunua ng’ombe wa kuchinja na mbuzi wa kumpa baba mzazi aliyemzaa Apondi. Hata baada ya kutekeleza haya, Mama Selifa mchungaji wa Budalangi Church of God alikoshiriki Apondi, anataka wapewe vitu ambavyo vingewawezesha kuendeshwa kwa mazishi. Anataka ng’ombe wa kuchinja usiku huo; tofauti na yule Mango amekwishawapa wazee wanaosimamia matanga.

Zaidi ya hii, anataka, sukari kilo ishirini, mafuta ya kupika kama kilo tano na pesa kiasi cha shilingi elfu tano. Anavyosema, pesa hizi zingewalipa watu ambao wangeshughulikia mazishi ya mwenda zake. Kutokana na mahitaji haya, ni bayana kwamba dini imekuwa ni biashara. Badala ya kumfariji na kumsaidia mfiwa, tamaa ya waumini pamoja na viongozi imepata mwanya wa kumfyonza kwa kila hali. Hali kama hii ni kama kutia msumari wa moto juu ya jeraha. Mwandishi ameonyesha jinsi kanisa limeenda bendi na panapopaswa kunyooshwa na kuitumikia jamii, panaendelea kupinda. Ameonyesha pia, namna ulafi umekita mizizi kote bila kusaza madhehebu na hata viongozi wa madhehebu haya kuathirika punde wapatapo mkasa. Mango kama kinara wa kanisa, anatwikwa mizigo bila hisia za huruma huku akiwa amefiliwa. Wanampuuza anapojaribu kuwakumbusha kwamba hata yeye, anamhudumia Mungu na maadili ni kwamba, mtu afiwapo, bili huwa juu ya viongozi wa dini na wala si kwa wamekumbwa na msiba. Ni jambo la kushangaza kuwa matanga yamekuwa njia ya kujipatia pesa. Tamaa ya namna hii vilevile,

imemshangaza Michael ambaye, pia ni mhudumu wa kanisa ambapo anainukuu Bibilia ikisema kwamba, “Ukienda mahali pa msiba ni vyema kushiriki katika msiba na kuwapoza walioathiriwa…” (uk. 95).

Tumeona namna ulafi umeyatenganisha makanisa kwani viongozi wake na waumini wanazozana kufuata mali na uongozi wa kanisa. Kwa mfano, Tonje na Mango wanatengana kufuatia tamaa ya uongozi na zaka wanazotaka na kisha kila mmoja akajiendea zake baada ya mafarakano. Mawazo ya Habwe kupinga uovu wa namna hii unajitokeza katika mhimili wa nadharia ya maadili unaosema kwamba, dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga kimaadili na kukemea yanayopotosha jamii. Pia, Mkufya amekemea uozo huu wa tamaa kwa vile unapotosha jamii.

### 3.1.4 Matatizo ya Uzinzi katika familia na jamii

Ngoma ni mzinzi kisha anaambukizwa Ukimwi. Ni mzinzi kwa sababu ana pesa nyingi zinazomfanya apende anasa. Analewa pombe, anavuta sigara, kucheza densi katika ukumbi wa starehe na kuwatongoza wanawake wengi kama Queen na Asha. Yeye ni mzee aliye na mke na watoto lakini anazini na Queen na Asha bila kinga. Mkewe amemwuonya aache kujihusisha na kila mzoga wa mwanamke lakini hakusikia. Ni kutokana na uzinzi wake anaambukizwa Ukimwi na kisha kumwambukiza mkewe. Tabia hii inazua mgogoro baina yao na familia kwa jumla. Tumeona kwamba Ngoma anarudi nyumbani kwake akiwa amelewa chakari na amechelewa. Tunadhihirishiwa kwamba:

> “Ngoma alijikokota kwa kuyumba, kuelekea sebuleni. Alijisikia vibaya kwa ile hali ya kujiona mwenye hatia kwani kila alipovuta pumzi, pua zake zilimkumbusha marashi ya Asha na harufu ya kushiriki ngono...” (uk. 24- 25).

Kutokana na dondoo hili, tunaelewa tosha kwamba, Tabu amechoshwa na tabia ya Ngoma kujihusisha na uzinzi. Tabia hii imemkera na suluhu ni kuondoka na kurudi kwao kwa wazazi wake. Hatua anayochukua itamfanya kusalia na watoto, huku watu wakimsema na pia kumcheka.

Athari ya uzinzi wake ni kukosekana kwa furaha na mapenzi katika familia. Aidha, kunakuwa na chuki baina yao. Vilevile, inamfanya Tabu kutelekeza chakula ovyo mezani na kumtaarifu kwamba hatakuwa anamwandalia chakula mezani ikiwa angechelewa kurudi. Wanapolala

kitandani, mkewe analala na kugeukia ukutani huku akimpa mgongo; hata anapotaka wajifunike shuka moja, anakataa kwa kuirusha pembeni na hata anaponyoosha mkono na kumgusa kiunoni, Tabu ananyanyuka na kumuonya akome kufanya hivyo, "Usiniguse tafadhali sana!" (uk. 27).

Utafiti huu, umetuonyesha kwamba, maisha ya ndoa kati ya wawili hawa yamekosa maadili na pia mapenzi. Queen naye amesawiriwa kuwa mzinzi kwani anashiriki ngono na mume wa mtu - Ngoma na kisha kumwambukiza Ukimwi. Hapendwi na wanawake wengi kwa sababu ya urembo wake, kisomo na kazi nzuri anayofanya. Ana pesa chungu nzima na hii ndiyo sababu ya kujitoma katika uwanja wa anasa. Hana jiko na pia mwana lakini anaambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Analaumiwa kumwambukiza Ngoma virusi vya Ukimwi na kukitia kitumbua chake mchanga. Ngoma naye anaenda kumwambukiza mkewe. -Tendo linalosababisha ugomvi na uhasama baina ya mtu na mkewe na kisha kusambaratisha mapenzi na furaha ya familia na jamii.

Tunaona hali ya watu kukosa maadili na kuheshimu tendo la ngono kunasababisha matokeo hasi maishani. Mwaandishi anatuonyesha namna uzinifu unavyoweza kusababisha matatizo makubwa katika familia na jamii kwa ujumla. Kwa mfano, Queen anaambukizwa Ukimwi kabla ya kuolewa hata kuzaa, akamwambukiza mume wa watu, Ngoma, na kisha anamwambukiza mkewe na pia Asha. Asha naye anamwambukiza Msafiri anayemwambukiza mkewe kule kwao. Katika utafiti huu tumepata kuona kuwa uzinzi unaleta majonzi katika familia na jamii; hii ni kwa sababu ya ukosefu wa maadili. Mwandishi anadhamiria kutuhimiza kujiepusha na uozo huu kwani walio na ugonjwa huu, wanasalia wakilaumiana, wakifedheheka, wakijuta, wakiteseka kwa maumivu, wakisengenywa na hatimaye kufa. Hata hivyo, katika riwaya ya *Paradiso*, unzinzi haujamuambukiza mhusika yeyote na ugonjwa wa zinaa kama vile Ukimwi.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Paradiso* imesawiri tendo hili kwa kuwatumia wahusika kadha. Uzinzi unasemekana kusababishwa na tamaa na hisia za kimwili. Mara nyingi linapotekelezwa huwa na athari hasi. Musa kwa mfano, kama mtumishi wa Mungu, hakupaswa kufanya ngono na muumini wake, Salome anayeonekana mzuri kiasi kwamba wanaume wengi wanammezea mate kwa vile uvaaji wake ni wa kipekee. Taswira inayojitokeza ni kwamba, anapovaa nguo zake anaonekana kama ua la mwasumini. Musa anamwona kapendeza kiasi kwamba hawezi kudhibiti hisia zake na hatimaye kumshawishi wafanye mapenzi. Wawili hawa wanashinikizwa na tamaa na kuishia kutekeleza tendo la uzinzi katika nyumba ya Kyalo. Wanapata nafasi wakati Kyalo, mumewe, anaelekea matangani ya rafiki yake kule Kisiwa cha Rusinga lakini kwa bahati mbaya,

gari wanalosafiria, linahusika katika ajali na kujeruhiwa. Akiwa mmoja wa majeruhi, anaamua kurejea nyumbani ili amsimulie mkewe yaliyojiri. Kwa bahati mbaya, anawafumania kitandani katika chumba chake cha kulala wakiwa wanafurahia uhondo wa uroda. Anaishia kuwajeruhi kwa kisu cha Kisomali. Baadaye, wawili hawa wanaokolewa na majirani baada ya Kyalo kubembelezwa kutowafanyia unyama. Kwa uchanganuzi wetu, tuliona kwamba wawili hawa walitawaliwa na tamaa, wakakosa heshima na kisha kushiriki tendo la ngono katika chumba cha Kyalo. Ni kutokana na tukio hili la kukosa maadili ambapo, kunapatikana majeraha, soni, gharama shaghalabaghala ya matibabu kisha Musa kuasi ukasisi pamoja na kanisa (uk. 51-52).

Kyalo ananuia kumua Musa lakini anabadili nia baada ya watu kumsihi amwache. Tena mkewe anapokuwa hospitalini anamwendea na kumwomba msamaha. Vilevile anamhimiza aendelee kusali katika kanisa anapokuwa akisali hapo awali na Musa. Isitoshe, anamhurumia Musa pia kwa yote yaliyotendeka.

Aidha, uzinzi unajitokeza baina ya Mtumishi wa Mungu, Michael na Patricia. Tendo hili la mapenzi ya kimwili baina ya wawili hawa linatokana na msukumo wa tamaa inayojengeka wakati Michael anapomtembelea Patricia nyumbani kwake naye Patricia anapozuru ofisi ya Michael. Wanapokezana busu kwa njia inayoamsha na kuchochea hisia za mapenzi kati yao (uk. 150).

Daima Michael anamuwaza Patricia, hali ambayo, inazima joto la uhusiano baina yake na Lydia. Kwa mfano, anapokuwa na safari muhimu, anachanganyikiwa na kumsahau. Isitoshe, anaacha kumletea zawadi kama hapo awali na furaha yake kudorora pia. Mara kukawa na uvumi kwamba walionekana wakiwa katika hoteli maarufu na ya kifahari ya Sunset Kisumu. Kwa msingi wa uchunguzi wetu, tuliweza kuona jinsi tamaa ya uzinzi inavyosambaratisha uhusiano katika familia. Aina hii ya tamaa inaharibu mapenzi kati ya mume na mke kwani mapenzi hupungua na kuzusha wasiwasi. Hatimaye uongo huanza kusemwa na kutawala maisha ya wanandoa.

Kando na mtoto Mango (mdogo), Patricia ana watoto wengine watatu aliowazaa hapo awali. Hili ni zao la kuchezewa shere na wanaume wa hapo awali. Tunapata ujumbe kuwa:

> "Patricia alikuwa ashamtajia Mike kuwa haoni damu yake ya hedhi katika miezi mitatu. Hali hiyo ilimpa Patricia taharuki. Michael alimweleza asijali… alionekana mtu wa imani." (uk. 162).

Kulingana na dondoo hii, tulibaini kwamba watu wengi wamekuwa wajanja na wazinzi. Tena ni bayana kwamba, Patricia ana tamaa ya kuolewa isipokuwa wanaume wanamdanganya, kumpachika mimba na kumhepa. Vilevile, ni bayana kama mchana kwamba, uja uzito wa Patricia unawasababishia Michael na Lydia matatizo mengi na magumu ya kisaikolojia; Michael anatatizika kupata suluhu kuhusu namna angeligharamia matibabu ya hospitali. Aidha, anabughudhika kuhusu malezi ya mtoto ambaye angezaliwa na kuishia kugharamia malipo ya hospitali anakojifungulia Patricia. Lydia naye ameolewa lakini kawa na jicho la nje.

Kwa mujibu wa utafiti huu, uzinzi unaonekana kukita mizizi katika sehemu nyingi za riwaya hii. Tunaelezwa kuwa Askofu Joshua pia ni mzinzi. Kabla ya kuwa kasisi, anaishi na Mganga, bwanake Lona na Lona. Kwa muda, Mganga hakufahamu kwamba anaendewa kinyume na Joshua. Mwishowe, Lona anamwacha Mganga na kuolewa na Joshua. Ukweli ni kwamba, uzinzi unasambaratisha ndoa kati ya Mganga na Lona kisha hapo baadaye, Lona anaolewa na Joshua bila jasho. Yote haya yanatokea kwa sababu ya tamaa.

> "… Lona hakujua amfuate Joshua au yule mume mwingine. Lona alielea kati ya wanaume hao wawili." (uk. 136).

Maelezo haya yanatoa na kukoleza ushahidi kwamba, Lona ni mzinzi kwani watoto alionao hakuwazaa na Joshua. Kwa mfano, Nice ambaye hataki kusikiliza ushauri wowote kutoka kwa Joshua. Anampuuza eti kwa sababu anamsumbua ilhali si babake. Joshua anapousikia utetezi huu anatamauka, anajisaka na kutaka kujua hali ya ukweli kuhusu matamshi ya Nice. Anaathirika kiasi kwamba anaamua kwenda katika msitu wa Ngong mahala patulivu ili kuyatalii maisha yake kisha apate suluhisho kuhusu anakokosea katika ndoa yake. Kwenda katika msitu inaashiria kuhatarisha maisha yake. Pia ni ishara tosha kwamba anakuwa tayari kwa tukio lolote maishani.

Vilevile, katika utafiti huu tuliona jinsi Lona anaendeleza uzinzi wake. Anapanda mbegu ya chuki kati yake na Boribori kwani tamaa ya ngono inampeleka kwake na kumtaka mahaba; jambo ambalo anakataa katakata. Kinachomfanya kutokubali kuwa na mahusiano ya mapenzi na Lona ni kwamba ni mkewe Askofu, rafiki na tena ni binamuye. Msimamo wake kwamba, maadili hayakumkubalia kujihusisha katika tendo hili. Tunaelezwa: "Boribori alipomkatalia, Lona alienda nyumbani huku amefura kama paka aliyeshambuliwa na mbwa." (uk. 138).

Tamaa ya kujihusisha na tendo la uzinzi linamfanya Lona kusema uongo. Anamsingizia Boribori kwamba alidhamiria kumnajisi. Tunadokezewa kusema:

> "Yule Boribori ni binamu yako?"
>
> Joshua aliulizwa kwa wingi wa kuchanganyikiwa.
>
> "Mimi sidhani. Kwa nini basi akataka kuni…,"
>
> "Alininajisi", Lona alidai. (uk.139).

Kusema uongo na kisingizio cha aina hii, ni hatari kwa usalama. Uongo huu unamfanya Joshua kughadhabika na kunuia kumtendea Boribori uhuni kama vile kumuua kwani shtaka la uongo kutoka kwa mkewe linachochea hisia za hasira na chuki.

Inabainika wazi kuwa lawama ya uzinzi, haimuegemei Lona tu. Joshua kama mkewe anazini pia. Hali hii inamuathiri mkewe na kumshinikiza kwenda kwa mganga anayeumaliza uzinifu wake. Naye mhusika Agripina pia anajifungua akiwa hajapata jiko. Hii nayo ni ishara kwamba, ni mzinifu. Hawezi kuidhibiti tamaa ya hisia ya mwili wake hivi kwamba anaishia kuizima kwa kufanya mapenzi kabla ya kuolewa. Tumeona akimweleza Michael kwamba aliyafanya haya kwa kuwa alikuwa na tamaa ya kupata mtoto. Agripina anasema:

> "Mimi naona mume wangu ana dosari." Agripina alisema bila kificho.
>
> "Kwa nini?" Michael aliuliza…
>
> "Mimi nilizaa mtoto kabla kuolewa naye." (uk. 99).

Kulingana na maongezi haya, tulifikia uamuzi kwamba, uzinzi katika kazi hii, umewachafulia maisha wahusika wengi na unaonekana kuwa kama jambo la kawaida katika maisha ndiyo maana Agripina hana haya kumtobolea mtumishi wa Mungu namna alivyozini na kupata mtoto. Kutokana na tendo hili, alipata fursa ya kumlaumu mumewe kadamnasi ya kuwa ndiye hakuwa na uwezo wa kuzaa. Tukirejelea mhimili wa nadharia ya maadili inayosema kwamba, uzuri au ubaya wa kitendo inalingana na jamii, Agripina aliona ilikuwa jambo la kawaida kuzini. Ndiyo maana haikuwa soni kwake kumfichulia Michael uzinzi wake. Hakika ukweli upo katika usemi huu kwa sababu jamii ya *Paradiso* imeichukulia tendo la kuzini kama jambo la kwaida. Hii si maadili. Sawa na *Ua la Faraja*, uzinzi ambao umesababishwa na tamaa umekita mizizi kote katika jamii. Tumeona inafanywa na watu wa jinsia zote. Kwa mfano, Ngoma, Queen, Asha na wengineo ni wazinzi.

Athari ya uzinzi hairidhishi. Wahusika wanapata ugonjwa, kuteseka na kuaga dunia na famila kusambaratika. Tofauti ya athari inayotokana na uzinzi katika riwaya hizi mbili ni kuwa, hapana uambukizo wa Ukimwi kati ya wahusika wa riwaya ya *Paradiso*.

### 3.1.5 Matatizo ya Pesa na Anasa

Watu wengine hujihusisha na uozo kama ulevi, ukahaba na anasa kwa sababu ya kuwa na pesa wanazoweza kuzitumia. Hivi ndivyo ilivyo katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Katika kazi hii, Mkufya alidhamiria kuonyesha namna pesa inavyowafanya watu kupenda anasa. Ngoma ana pesa nyingi anazotumia katika anasa ya ulevi, wanawake wengi, uraibu wa kuvuta sigara na ulaji wa nyama. Anasa inamfanya kuchelewa kufika nyumbani mapema na kuwafanya watoto wake kukosa nafasi ya kujumuika naye. Ni mkali kiasi kwamba watoto wake wanamwogopa. Anatumia pesa zake vibaya huku famila yake ikisalia bila masurufu. Matokeo ya pesa nyingi yanamzuzua kunywa pombe kupindukia, kuwa mkali na kuwa na mazoea ya kugombana. Pesa zinamfanya kuwa mjeuri, kujifahari na pia kuwa mtu mwenye dharau. Hali hii inampelekea kuchukiwa na watu wengi, mmoja wao akiwa ni mwanawe, Juma.

Mwandishi ametuonyesha kwamba, pesa haziwezi kuwa kila kitu kama vile kivutio au nyenzo ya furaha maishani. Mtu asipotumia pesa zake vizuri, basi hupata matatizo mengi baadaye. Katika riwaya hii, Ngoma ana pesa nyingi lakini zimekuwa chimbuko na chemchemi ya majuto katika aushi yake. Ana uwezo wa kutangamana na wanawake warembo walio na pesa kama vile Queen na Asha katika majumba ya burudani (uk. 9).

Queen ni msomi, mrembo anayesifika katika mtaaa wa Tandika. Ni mwanasheria aliyeajiriwa na kuhodhi pesa nyingi. Kila mara walikunywa pombe pamoja hadi usiku. Mazoea haya yanawafanya wajuaji kumdokezea Tabu anayewafumania wakinywa pombe pale *Kanga Moja Club*. Pia, mazoea haya yanaishia wao kushiriki ngono hasa katika nyumba ya Queen na hatimaye, kuambukizwa ugonjwa wa Ukimwi. Msimulizi anatueleza kwamba:

> "Muda mrefu ulikuwa umepita tangu uhusiano na mawasiliano baina yake
> na Queen uishe. Kwa nini apige simu? Omolo alikwishakataa kuendelea
> kuhusiana naye toka siku ulipotokea mzozo ..." (uk. 43).

Asha naye ana pesa nyingi kwani anamiliki hoteli ya kifahari *Hotel Victoria* anayojengewa na Bwana Hastings. Hajaolewa kwa sababu anachukulia ndoa kuwa ni utumwa na pia ana uwezo wa

kumlisha mwanamume. Kwa mfano, anamnunulia Msafiri kuku na bia. Anawapenda wanaume wenye pesa kama Msafiri, Ngoma na Hastings. Kuwa na pesa kunamfanya kupenda anasa, kama vile kunywa pombe, kucheza densi na kushiriki ngono. Ni kutokana na aina hii ya maisha kunamfanya kuambukizwa ugonjwa ambao unamfanya kujuta, kugombana na kumchukia Ngoma. Tamaa ya pesa inamsukuma kumfuata Msafiri na kumwambukiza ugonjwa huu. Ni kutokana na utafiti huu tunashuhudia kwamba, pesa na anasa husababisha majonzi, kwani baada ya raha ni kilio (uk. 83).

Aidha, katika riwaya ya *Paradiso*, matatizo ya pesa na anasa yanawiana na ya riwaya ya *Ua la Faraja*. Wahusika kama Loana, Joshua, Michael na Boribori wana tamaa ya pesa na anasa. Joshua anachukua gari la kanisa na kufanya lake. Boribori anajihusisha na biashara ya ulanguzi wa madawa ya kulevya ili apate pesa nyingi za starehe, mwishowe anashikwa, anashtakiwa na kufungwa. Michael anamchukua Patricia na kumpeleka katika hoteli ya kifahari ya Sunset Kisumu na habari inamfikia Lydia anayezua tetezi kuihusu. Tofauti baina ya riwaya hizi ni kwamba, anasa katika *Ua la Faraja* imekumbwa na athari kama maambukizi ya Ukimwi na vifo.

Mwandishi anatutahadharisha kwamba, tukiwa na pesa tunapaswa kumakinika tunapozitumia ili tusije tukajuta jinsi anavyojuta Asha kwa kuwa na tamaa ya pesa na baada ya kuzipata, anajihusisha katika anasa inayomletea maisha ya tanzia. Utafiti huu unaungwa mkono na nadharia ya maadili inaeleza sanaa ya fasihi kama inayotoa mifano bora ya kuigwa na kuziacha potovu. Nadharia hii imetufaa sana katika kutuelekeza na kutambua maovu ya anasa katika jamii kama tuliyoyarejelea.

### 3.1.6 Matatizo Katika Ndoa

Asasi ya ndoa inachukuliwa kuwa muhimu sana katika jamii kwani, uthabiti wake huwa chanzo cha uthabiti wa asasi zingine za jamii. Siku hizi hata hivyo, ndoa nyingi zimevunjika. Watoto katika familia ndio huathirika zaidi wakati ndoa zinapokumbwa na matatizo makubwa. Vilevile migogoro katika ndoa, husababishwa na mambo mengi kama kutokuwepo na mawasiliano baina ya mume na mke. Ili ndoa ipate kudumu na kustawi, inawalazimu wanandoa kuongea ili kuweza kutatua matatizo yao. Tatizo la pili ni kuingiwa na jamaa na marafiki. Mara nyingi baadhi ya hawa hawawatakii walio katika ndoa ufanisi. Huenda ni kwa sababu ya wivu au mashindano. Kulingana na jamii za kiafrika, ndoa inachukuliwa kuwa na thamani maalumu. Kukosekana kwa watoto

kuchukuliwa kuwa ndoa haijakamilika. Wanandoa hawapaswi kutalikiana kama kuna suitafahamu katika ndoa yao. Waathiriwa wanapaswa kutafuta ushauri kutoka kwa watu wenye hekima, kama vile wazee, wazazi na hata viongozi wa dini, ilmuradi tu ndoa isisambaratike.

Ndoa ya Ngoma na Tabu inakumbwa na matatizo chungu nzima kwa sababu ya anasa kama vile ulevi na uasherati wa Ngoma. Ngoma anatumia muda wake mwingi kunywa pombe katika baa hadi usiku. Hali hii inamfanya kusahau majukumu yake ya nyumba kama vile kuikimu familia yake. Anafanya mapenzi kule nje na hata anapofika kwake nyumbani, anakosa kumwonyesha Tabu mahaba. Queen anamwambukiza virusi vya ugonjwa wa Ukimwi, naye akamwambukiza mkewe. Inapojulikana kwamba Queen ana dalili ya ugonjwa huu na ana uhusiano wa kimapenzi, mkewe anaanza kumlaumu mumewe kwa kumwambukiza ungonjwa utakaomuua hatimaye. Mara kunakuwa na chuki katika ndoa ya wawili hawa; Ngoma anachukiwa na wanawe na jamaa ya Tabu kama Grace. Mwisho kuna talaka kama mwandishi aelezavyo:

> "Grace alimpenda dada yake …. Kilio hiki kilimshtua na kumchoma moyoni.
> Kuna nini? Alijua dada yake alikuwa na matatizo… hayo dadayake
> alikwishayazoea… Kwa nini dada yake amekuwa mkiwa kiasi kile? (uk. 57).

Mwandishi alidhamiria kutuonyesha matatizo ambayo yako katika ndoa ya Ngoma na Tabu. Ametuonyesha namna Tabu amevumilia na kutafuta mbinu mbadala ili kukabiliana na hali ngumu katika ndoa yao. Kuna jambo moja tu ambalo linamtisha na kumkosesha furaha, nalo ni kuambukizwa ugonjwa usiotibika wa Ukimwi. Mwandishi anaweka wazi taswira ya Tabu kuhuzunika kwa kuangazia mazungumzo kati yake dadaye:

> "Dada, kuna nini?"
> "Aaii! Ooii! Mungu wangu n'tamwachia nani miee? Ooii…"
> . Akaendelea kulia huku akisema, "UKIMWI, Grace, UKIMWI!
> Shemeji yako kaniletea UKIMWI." (uk. 57-59).

Ni bayana kwamba, mwandishi amelenga kuonyesha umuhimu wa kutambua faida ya uaminifu katika ndoa. Anatuhamasisha kwamba, ukosefu wa elementi hii katika ndoa huzua ukosefu wa furaha. Mume asipokuwa mwaminifu kuhusu tendo la ndoa, anaweza kumletea mkewe ugonjwa hatari unaoweza kumkosesha furaha na kisha kusambaratisha familia yao.

Vilevile, tofauti za dini kati ya wanandoa imeonyeshwa kuwa chanzo cha matatizo katika ndoa. Hii hutokea ikiwa wanandoa ni waumini wa dini tofauti. Kwa mfano, mume akiwa ni Mwisilamu, naye mke awe Mkristo. Tofauti wa namna hii wakati mwingine, huzua vuta nikuvute kuhusu ni nani atakayeasi dini yake na kujiunga na ya mwenzake. Mara nyingi mume humtaka mke kufuata dini yake. Swala hili hulenga urahisishwaji wa uleaji wa watoto wao. Mawazo kama haya ndiyo yanamlazimu Tabu kuacha Ukristo na kuwa Mwisilamu. Uamuzi wa aina hii unaweza kuifanya jamaa kumtenga mhusika, namna Tabu anavyotengwa hadi anaenda kuomba msamaha; kama asemavyo mwamdishi:

> "Mazishi yake yalifuata taratibu za mazishi ya Kikristo. Kufuta
> talaka alikokufanya Ngoma kulisaidia sana katika kesi ya mirathi….
> Ndugu wa mume, ambao walijua kwamba Tabu alikuwa ametalikiwa,
> Walishangazwa …" (uk.339).

Tumeona kwamba, ni vigumu kwa wanandoa kuasi dini yao na kuishiriki ingine iliyotofauti. Tabu anaendelea kuwa Mkristo naye mumewe Mwislamu. Hata hivyo, hatua ya Tabu kumridhia mumewe na kupewa mafundisho ya Uisilamu na baadaye kusilimu, kunamletea matatizo mengi kutoka kwa jamaa zake. Tena ndoa hukumbwa na matatizo yanayoletwa na tamaa ya mali. Katika ndoa, mali humezewa mate sana na watu wengi wa familia. Kwa mfano, nduguye Ngoma, Mashaka, anamtaka Juma aeleze mahali magari ya marehemu babake yamepelekwa. Pia wanamshurutisha Omolo awape wosia na kutishia kutoutambua. Bila soni wanalalamika na kutaka kujua ni kwa nini Omolo anawaachiwa wosia ilhali yeye hakuwa jamaa wao wala Mwisilamu. Tuliona kwamba, kwa vile hawakutajwa popote katika wosia kuhusu mirathi, wanakasirika na kisha kuitenga aila ya Ngoma. Kwa hakika ni tamaa ya ajabu. Tumeona kwamba, watu wengi katika jamii huwa na tamaa ya mali. Hata mtu anapougua na kisha kufa, jamaa zake huwa na tamaa ya kurithi mali yake. Huwa hawana haja hata kidogo na masilahi ya familia ya marehemu kwani wanachongoja kupata ni mali ya marehemu. Wanapokosa kufikia malengo yao, wanaamua kuitenga familia ya marehemu na pia kususia kuisaidia panapohitaji msaada. Mwandishi anatuonyesha namna tamaa ya aina hii inavyoathiri jamii yetu. Anatutahadharisha kwamba, tusipende mali sana kuliko kutoa msaada katika jamii.

Aidha, tumeshuhudia kwamba, dharau ni kati ya matatizo makubwa katika ndoa. Katika dondoo tulioona hapo awali, dharau ni tabia ya kupuuza na pia kutowaheshimu watu. Kudharauliwa katika

ndoa kunaonyesha kutothaminiwa, kuaibishwa na kuvunjiwa heshima kupitia vitendo vya kikatili. Mtu anapaswa awe na haki ya kuheshimiwa na pia kuthaminiwa katika ndoa. Dharau inajitokeza wakati aidha mwanamke au mwanamume, anakosa kuthaminiwa, kuvunjiwa heshima na vilevile kuaibishwa anapotendewa maovu au kutumiliwa lugha chafu katika mawasiliano. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2008) Tabu anadharauliwa na Ngoma. Ngoma anamsemesha kwa dharau na pia anakosa kuheshimu ushauri wake kwamba, asiwe na mazoea ya kufika nyumbani akiwa amechelewa tena mlevi. Anapoulizwa kupimwa damu ili kuthibitisha hali yake kuhusu ugonjwa wa Ukimwi, anakataa na kumlaumu Tabu kwa kumsingizia kwamba ni yeye ameambukizwa ugonjwa wa Ukimwi. Anamweleza:

> "Sasa unaendea nini kupima kama unajiamini?" Ngoma aliuliza na kujifanya mkali akisema, "Labda wewe ndiye mwenye wasiwasi. Umeshafanya madhambi yako huko, sasa waniambia mimi tukapime…usinihusishe mimi." (uk. 137).

Kauli hii ya Ngoma ilimkasirisha Tabu si haba. Hatimaye, akanyanyuka pale alipokuwa kalala kitandani akiwa anamtazama kwa jicho la chuki, amejaa hasira kisha kuangua kilio. Vilevile ndoa hii ilikuwa na dharau kutoka kwa jamaa wa mume. Wakati wa matanga ya Ngoma Tabu alitengwa na kukosa kuhusishwa kama mwenyeji. Mwandishi anatueleza kwamba:

> "… Akabaki kama mtalaka wa marehemu; na wifi zake, Zubeda na Rukia, pamoja na shemeji zake wakawa wanamhesabu kama mtalaka… asiyehusika moja kwa moja na msiba ule. Sasa wao ndio wakawa wenyeji..." (uk. 295).

Kwa maoni yetu, hali ya jamaa kumtenga Tabu wakati wa matanga ilikuwa ishara tosha kuwa wanamdharau na ndoa yao haikuwafurahisha jamaa wao na kumtenga, kungemkosesha urithi.

Aidha, baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Paradiso* wamekifanya chuo cha ndoa kuwa kitega uchumi tena cha kulazimisha. Wanatekeleza hili lengo likiwa kufaidi kifedha na kuepuka fedheha. Mfano mzuri ni wa wazazi wa Nice (uk. 67). Joshua, anataka kumuoza Michael binti yake ambaye ameachana na Todd ili kuepuka soni ya kuonekana kama kahaba. Tulichukulia vilevile kwamba, alinuia kufanya hivyo ili atakapompandisha Michael cheo katika kanisa yao, mali na wadhifa huo

ungeweza kusalia katika familia yake. Jambo hili lingemnufaisha sana kwani bintiye atakuwa tayari amepata jiko.

Hata hivyo, kuwa na hisia chanya katika ndoa ni muhimu na baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Paradiso* wanajua umuhimu wa jambo hili. Lona analalamika kumhusu Joshua kwa kupoteza hisia na kumshuku kuwa na mke mwingine. Hali hii inamshurutisha kushirikiana na Adema kisha kumwendea kwa mganga, Angelina ili kumdhibiti; mganga anaitisha kiasi kikubwa cha pesa kama shilingi elfu ishirini hivi (uk.109). Mwandishi anatueleza:

> "Nina shida na mzee."
>
> "Shida gani na naona wewe ni mzee na anaonekana amekutunza vizuri?"
>
> "Ndio tulikuwa tunakaa vizuri lakini amebadilika sasa," Lona alisema.
>
> "Sasa unatakaje? Yaani unataka mzee afanyaje?" Lona aliulizwa.
>
> "Ninataka asioe..." (uk.108-109).

Kutokana na mazungumzo haya tuliona kwamba, matatizo ya mwanandoa kuogopa kutengwa na mwenzake na kutaka kuoa mke mwingine inazua hofu. Inamfanya mke kumwendea mumewe kwa unganga ili apendwe huku akitumia kiasi kikubwa cha pesa. Mapenzi yanapopungua kati ya wanandoa hali ya wasiwasi huota mizizi. Michael anapunguza mapenzi yake kwa Lydia, Lydia anakumbwa na wasiwasi hasa baada ya kuota kuwa kuna tishio la ndoa yao kuyumbishwa. Ni ukweli mtupu, mumewe anamuwaza Patricia na kujuta kumuoa. Kutokana na haya anakoma kumletea zawadi kama hapo awali. Pia, furaha aliyokuwa nayo aliporudi nyumbani inapungua (uk.150). Hali hii ilimshawishi Lydia kumshitakia Patricia kero lililokuwa moyoni kwani alihisi kulikuwa na mtu aliyekuwa akivuruga ndoa yao. Ilikuwa ni haki ya Lydia kulalamika kwani ni wajibu wa kila mwanandoa kuonyesha na kudhihirisha hisia chanya kwa mwenzake. Burke (2007: 7) anawashauri wanandoa kutiana hamu ili mahusiano yao katika chuo cha ndoa yakamilike. Kulingana na maelezo haya, Michael alipokosa kumsisimua mkewe aliweza kumuotesha mbegu ya wasiwasi.

Vilevile, tumeona kuwa ndoa inaweza kutawaliwa na ukosefu wa uaminifu unaochukuliwa kama kiungo muhimu. Maharusi hutoa ahadi ya kuwa waaminifu wanapofunga pingu za maisha kwa msingi wa dini ya Kikristo. Ndoa inapokumbwa na hali ya uzinifu, huwa imeingia doa. Kwa

mujibu wa Chapman (2008: 169-170), sifa ya kupendelea uaminifu katika chuo cha ndoa, imejengika katika ubinadamu wetu, na pia inahusishwa na uadilifu pamoja na unyoofu. Vilevile, katika sheria za Kenya kuhusu masuala ya ndoa (196:7), pana ithibati tosha kuwa endapo mwanandoa si mwaminifu, mwenzake anaweza kumpa talaka au akadai kutalikiwa.

Ndoa ya Lona na Mganga, inakumbwa na undanganyifu mwingi. Lona anapofanya mapenzi na Joshua kisiri kwa muda bila Mganga kujua. Inapojulikana, haoni aibu kumwacha mumewe Mganga na kuolewa na Joshua ambaye amesaidiwa kwa makazi katika nyumba ya Mganga (uk. 34). Hata hivyo baadaye, ndoa ya Joshua na mkewe tena inakumbwa na uzinzi. Lona ni mdanganyifu kwani anazini na kuzaa na watu wengine watoto Nice na Judy. Joshua naye anazaa watoto wawili na Leah, muumini wake amabaye alikuwa hajapata jiko (uk. 57).

Isitoshe, ndoa ya Kyalo na Salome pia, ina udanganyifu na uzinzi kwani Salome ana tamaa ya kupata mtoto na hii inampelekea kushawishika kwa urahisi kuzini na Musa. Kwa mujibu wa utafiti huu, tunaweza kusema kuwa kukosekana kwa uaminifu ni changamoto kuu inayowakabili watu wa matabaka yote wakiwemo watumishi wa Mungu na washiriki wa kanisa; na ni kinaya kwani ni wao huwaapisha na kuwashauri wanandoa kuwa waaminifu (uk. 50 -51).

Tena ni ukweli kwamba, kuoa wake wengi ni tatizo linaloikumba ndoa katika riwaya hii. Mango ana wake tano, hawara mmoja na watoto wengi ambao anashindwa kuwatunza. Tunaelezwa kwamba, wake zake wanajilisha na kuwasomesha watoto wao. Kwa mfano, Apondi analima shamba mithili ya trekta ili kujikimu. Tunaamini kuwa, ni hali ngumu ya maisha kama hii ndiyo inayokuwa chanzo cha maradhi ya kifua inayomkera na baadaye kumuua Apondi (uk.24). Tumeona tena kuwa, mtu anapofanya kazi, ni busara kuoa wake anaoweza kuwatunza ili ndoa yake isitumbukie nyongo. Asemavyo Tolstoy, jukumu kuu la nadharia ya maadili ni kuelekeza jamii namna ya kutatua matatizo yatakayojitokeza. Mawazo ya Tolstoy yana ukweli chungu nzima kwa vile wanajamii wakiwa na maadili wanaweza kuepuka matatizo yanayoweza kutokea katika ndoa zao. Hawana budi kutenda mema.

Tumeona kuwa, matatizo ya ndoa katika riwaya hizi mbili zimefanana sana. Zote zinayumbishwa na hali ya wanandoa kutokuwa waminifu, kuwa na pesa nyingi na kuwa na tamaa ya anasa.

### 3.1.7 Matatizo ya Uongozi

Viongozi katika nchi yoyote wanafaa kuwajibika katika kufanya kazi zao. Jukumu lao kubwa ni kuwaongoza wananchi ili waweze kupata fursa ya kupiga hatua za kimaendeleo katika maisha. Kwa mfano, katika Nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Maishani, kiongozi anayeweza kutegemewa na wale anaowaongoza ni yule anayewajibika. Kiongozi wa namna huyu ni mpenda haki na asiyeongozwa wala kutawaliwa na ubinafsi. Kuna baadhi ya viongozi wanaotumia nguvu na kuwanyanyasa wengine. Viongozi hawa wanakosa utu, kuwajibikia hadhi zao na athari ni kwamba wanaongozwa hukosa huduma muhimu. Nafasi ya uongozi huanzia katika familia. Maisha ya jamii hutegemea uchumi na chanzo cha maisha duni huwa mfumo mbaya wa uchumi. Uchumi thabiti hupunguza uzito wa hali ya maisha. Na suala la uchumi ndilo limejenga migogoro mikuu katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Mwandishi ametumia hali ya Ngoma kuitelekeza aila yake kama mojawapo ya misingi ya migogoro katika familia. Hali ya watu wengine kuwa na pesa na wengine kukosa pia kumechangia katika migogoro hizi. Ngoma kwa mfano, kuwakataza Tabu na Juma kuuza genge kunaashiria kuzimwa kwa tegemeo la kiuchumi la familia ya Tabu. Hii ni baada ya Ngoma kususia kumpa Tabu pesa za masurufu. Tabu anapata pesa za matumizi kwa kuuza mboga, nyanya na bidhaa nyingine katika genge. Anafanya hivyo kwa kushirikiana na mwanawe, Juma. Babake anaanza kulalamika kuwa Juma hataki kwenda msikitini kwa sababu anashiriki biashara na mamake. Ngoma kama kiongozi wa familia yake, hapo awali alikosea kuwafundisha wanawe kuhusu maswala ya dini kwani alitumia wakati wake mwingi katika anasa kama ulevi na kukimbizana na wanawake. Aidha, hakuwapa pesa za matumizi. Hali hii inamfanya Juma kumchukia babake kwa kutomjali mamake na kumfanya afanye biashara za kupika vitumbua, chapatti na kuuza gengeni la mboga ili waweze kujikimu. Kando na kuwa na pesa nyingi, mkewe anaishi maisha ya kimaskini na hata kukosa nguo nzuri. Kama anavyoshangaa Juma:

> "Kama baba yake ana pesa nyingi za kulewa pombe, kwa nini mama yake anaishi maisha ya kimaskini?" (uk. 34).

Mwandishi anatuonyesha kuwa uongozi huanzia katika familia. Baba kama kiongozi wa familia yake, anapaswa kuwa mfano mzuri. Ngoma anakosa kuwa kiongozi wa kuigwa kwa kukosa kuwajibika. Hii inasababisha familia yake kutafuta njia mbadala za kupata pesa za kujikimu. Familia yake inajipata katika hali mbaya ya maisha na uhusiano wao kudorora kwa sababu ya yeye

kukosa maadili ya kuitunza. Tuligundua kwamba, uthabiti wa familia hutegemea uongozi mwema kutoka kwa wazazi na hasa wa baba mzazi.

Katika riwaya ya *Paradiso,* kuna matatizo mengi yanayotelekezwa katika uongozi na mali. Kuna malumbano ya uongozi wa kanisa unaomsababisha Tonje kutengana na Mango kwa kuzozania washiriki na zaka. Mzozo unamshinikiza Tonje kufungua kanisa lake la New Pentecostal Bible Church, Kisauni. Tamaa ya washiriki na zaka pia inapanda chuki kati yake na Mango (uk. 45).

Kutokana na mazungumzo baina ya Zuhra na Michael, tumeweza kubaini kwamba, siku hizi watu wana tamaa, hufuata kunako miujiza ili matatizo yao kuhusu uchumi na jamii iweze kusuluhulishwa. Kuna kupigania uongozi wa kanisa ili kujinufaisha kutokana na sadaka. Hii ndiyo maana kunazuka ugomvi katika kanisa. Mwelekeo wa namna hii unawasambaratisha waumini.

Tamaa ya uongozi na mali katika kanisa inapanda chuki kiasi kwamba wanaotaka wadhifa, wanakuwa tayari kuwaua washiriki na wapinzani wao. Kwa mfano, Mango analishwa sumu kutokana na mpango wa Tonje. Anaugua nusura aionyesha dunia kisogo. Mwandishi alidhamiria kuziteka fikira zetu kwa kusimulia visa kadhaa vinavyolisawiri jinsi kanisa linavyokosa maadili. Anatueleza:

> "Zuhra aliamka na wasiwasi mkubwa. Kwa siku nne hajawa na furaha.
> Mango, alikuwa amelazwa… Leo Mango amefanyiwa dawa. Kisa
> maana ni uongozi na hiyo sadaka." (uk. 61).

Taswira tunayoipata kutokana na dondoo hili ni kwamba, badala ya viongozi kuwahimiza watu kudumisha amani na kutenda mema, wao ndio wanaoshiriki katika kufanya maovu. Hii ikiwa ni kinyume na maadili na ukweli wa mambo.

Vilevile, tamaa ya uongozi na kuhodhi waumini wa kanisa la Jerusalem Church, unazua ugomvi baina ya Joshua na Omutele. Baadaye, anaona hapakuwa na hoja kugombea kitu na kijana, Omutele na baadaye, anaanzisha kanisa lake la New Jerusalem Church anakoguria na wafuasi wake.

Tamaa ya umashuhuri inamfanya Joshua kumwonea Michael wivu. Hii ni kwa sababu ya namna anavyohubiri Michael, inayowavutia waumini wengi wa kanisa (uk. 55). Kiasi anavyozidi

kunyunyiziwa sifa, ndivyo uhusiano wake na viongozi wengine ulivyozidi kudhoofika (uk. 67). Utendaji wake wa miujiza haumfurahishi Joahua anayekuwa hana kipawa kama hicho na kwa sababu hiyo kila shughuli inanasibishwa na Joshua na Lona. Mwandishi anatudhihirishia kwamba:

> "Kila uchao uhusiano baina ya Michael na Joshua uliendelea
> kutumbukia nyongo. Ni kama majogoo wawili yaliyokaa katika
> kizimba kimoja. Kila mmoja katika jogoo hao alitaka utawala." (uk. 70).

Hapo kitambo, hali ya vuta nikuvute ilikuwa batini halafu baadaye ikawa jambo lisilositirika tena. Kisha kukafuatwa na vita vya kisaikolojia na kugawanyika kwa kanisa la New Jerusalem katika makundi mawili. Kundi moja likawa la Michael na lingine la Joshua. Tamaa ya mali inapelekea kanisa kukumbwa na uvumi, vidoko na udhabidhabina; kila mmoja anamsema mwenzake kwa mabaya. Kunakuwa na vita baina ya makundi haya ambapo Michael anajeruhiwa kwa kurushiwa kiti cha plastiki kinachompasua kichwa. Kisha inachochea hisia na hasira za wafuasi wake wanaoamua kuvamia kundi la Joshua, kulipiga na kulifurusha. Kunakuwa na sintofahamu, hali inayowavutia askari polisi wanaofika na kuzima fujo na kisha kutenganisha vikundi hivyo. Matokeo yakuwa, kanisa la New Jeruslem kuvunjwa. Joshua anasalia Olympic, naye Michael anaguria Fort Jesus.

Tuliweza kuona kwamba, tamaa ya uongozi na mali inasababisha kuvunjika kwa kanisa la New Jerusalem. Hatua hii inamhuzunisha Michael huku Joshua akifurahia na kuchangamkia kufurushwa kwa kundi la Michael na kuwalaani vijana wanaojitakia makuu kabla ya wakati wao. Tamaa inamfanya kutoa uamuzi wa kutowahusisha vijana katika maswala yake muhimu. Kwa minajili hii, anamfanya Lona kuchukua wadhifa uliokuwa wa Michael kama mojawapo wa makasisi wa kanisa la New Jerusalem. Naye Nyamongo mtoto wa mjomba wake anafanywa kuwa mhubiri.

Hata baada ya kutekeleza haya yote, uhasama unaosababishwa na tamaa ya uongozi na mali, unazidi kupenyeza mizizi na shina katika familia ya Joshua. Lona anataka kuudhibiti uongozi wa kanisa la New Jerusalem; anatimiza haya kwa kushirikiana na Adema kumwendea mumewe kwa mganga, Angelina ambaye anamganga. Anavichukua vitu vya Joshua kama vile nywele na kufungia kwenye karatasi ya plastiki na nguo ndani ya chupa hatimaye kumrejeshea Lona. Kutokana na utafiti huu, tulipata kujua kuwa baada ya mganga kukamilisha kazi yake, aliitisha

kiasi kikubwa cha pesa cha shilingi elfu ishirini hivi, huu ukiwa ni ubadhirifu mkubwa wa fedha. Ushirikina unakuwa na matokeo hasi kwani, unamfanya Askofu Joshua kughafilika akili. Shughuli zote za kanisa zikuwa zinafanywa na Lona. Hali hii inamfanya kujiona mshindi katika mapambano haya. Mwandishi anatujulisha kwamba, "Jicho la nje ambalo mume wake alikuwa ameanza kuwa nalo aliling'oa kwa ufundi." (uk. 113).

Tamaa ya mali vilevile inamfanya Joshua kulishawishi kanisa kuwa na mgombeaji katika siasa. Kama kanisa, wanafikiana kwamba, Gekonge, agombee kiti cha ubunge cha eneo la Langata. Endapo angefaulu, angelisaidia kanisa kupata misaada kutoka nchini za ng'ambo. Hata hivyo, Gekonge anabwagwa katika uchaguzi huo na kuzua huzuni kubwa pale kanisani. Tulichukulia kuwa wanaomuunga mkono wanahuzunika kwa sababu azma ya tamaa yao inafishwa na kutotimizwa na pia kujuta kupoteza kiasi kikubwa cha pesa.

Aidha, katika utafiti huu tuliona kuwa tamaa ya mali inamsukuma Amuko kumfanyia bintiye maovu kwa kulala naye angali bikira (uk. 57). Zaidi ni kwamba, anamuua ndugu yake ndipo aweze kupata mali. Tumechukulia kuwa, tamaa ya mali inaweza kumshurutisha mtu kutenda unyama ili kutimiza azma yake. Wanajamii wanapaswa kuongozwa na ushauri wa I. Kant unaopatikana katika nadharia ya maadili kwamba, urazini wa mwanadamu ndiyo muhimu na pia chanzo cha hadhi ya mwanadamu kujitawala. Ili mtu ajitawale na kutawala wengine anahitajika kutumia bongo na kuhakikisha kuepukana kutenda maovu. Anapaswa kuwa na maadili. Hata hivyo, matatizo ya uongozi yanayotokana na tamaa ni mengi sana katika riwaya ya *Paradiso* kuliko *Ua la Faraja*. Habwe ameelezea matatizo kama Amuko kumuua ndugu yake na pia kufanya mapenzi na binti yake ili aweze kuwa tajiri. Lona anamwendea Joshua kwa mganga ndipo aweze kumdhibiti na mengine mengi. Mkufya, amerejelea Ngoma kama mfano usio mzuri kama mzazi (kiongozi) kukosa kuwaelekeza watoto wake kuhusu dini. Mifano yote hii inaashiria uozo unaotokana na tamaa katika jamii.

### 3.1.8 Ushindani kati ya Usasa na Ukale

Usasa ni hali ya kufanya mambo au kuishi kwa kufuata utaratibu wa maisha ya kisasa bila kuzingatia mila na desturi za utamaduni fulani. Ni hali ngumu kwa mtu kujitenga na mila na desturi za jamii yake. Baadhi ya watu katika jamii husika hukumbwa na changamoto za kuzingatia mila pamoja na desturi za jadi na pia kuwepo kwa haja ya kufuata usasa. Changamoto hii ina athari hasi

katika maisha ya baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Ni katika mukatadha huu kuhusu ujadi, ambapo mhusika Queen ameangaziwa kama kajipata katika njia panda. Kutokana na tabia yake tuling'amua kwamba katika maisha yake, hakuzingatia mila wala desturi za jamii yake. Amesoma hadi Chuo Kikuu na kuhitimu kama mwanasheria. Anafanya kazi kubwa iliyo na mshahara mnono. Amejinunulia ploti na kujenga nyumba ya kifahari kisha kuzama katika bahari ya anasa kama kunywa pombe, kufanya mapenzi kiholela na kuishi katika nyumba yake nzuri. Hapata jiko. Anawatongoza wanaume na kuwapeleka kwake kushiriki tendo la ngono. Amekwishawahi kufanya hivyo na Omolo na pia Ngoma. Tabia kama hii ni kinyume na matarajio ya mila za Kiafrika. Ni kwa sababu hii mambo yanamwendea mrama. Anaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kufa kabla ya kuchumbiwa wala kuchumbia, kuolewa na kuzaa mtoto. Tunaelezwa:

> "Omolo alikwishakataa kuendelea kuhusiana naye toka siku ulipotokea mzozo baina yake na mwanamke huyo… kumkuta jirani yake, bwana Ngoma… Queen." (uk. 43).

Ni dhahiri kwamba, Queen hafuati mila za Kiafrika zinazomtaka mwanamke kuolewa, kuwa na mume mmoja na kujiheshimu. Tamaa ya anasa na kuishi peke yake bila mume inamfanya kujuta baadaye, baada ya kuambukizwa ugonjwa, kukosa mtu wa kumuoa na pia kukosa mtoto. Mwandishi anadhamiria kuonyesha kuwa, maisha bila mila hayana thamani yoyote. Pia, tuliona mtazamo wa kushikilia mambo yaliyopitwa na wakati ukionekana katika maisha ya Mashaka na jamaa zake. Wanataka mwili wa marehemu uoshwe katika chumba chake cha kulala. Hii ni kulingana na utaratibu wa mila ya jamaa yao. Lakini, Juma, Sheikh Rajabu na Dakitari Hans wanaonelea kuwa maiti ya Ngoma ioshewe kule hospitali ili kuepuka hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa Ukimwi. Tofauti hii inaelekea kusababisha mvutano baina yao; wanaofuata mila kama Mashaka na wasiofuata mila, watu wa usasa kama Juma na Dkt. Hans. Dhamira ya mwandishi ni kutaka kutuonyesha mgongano na mvutano uliopo katika jamii kuhusu ujadi na usasa ambao ndiyo chanzo cha migogoro katika jamii. Tena wanajamii wanaofuata mila huzitumia kuwanyanyasa na kuwadhulumu wale wasiofuata mila hizo. Kwa mfano, inakisiwa kuwa Mashaka na jamaa zake wanataka kutumia nafasi ya kufika chumba cha malazi cha marehemu ili wapate kunyakua stakabadhi na vitu vingine muhimu. Hii ni kwa sababu ya tamaa yao kubwa ya mali.

Kushukiwa huku kunamfanya Juma ahamishe vitu vyote muhimu hadi chumba chake na kuvifungia humo (uk. 300).

Hatua ya Juma kufanya hivyo, ilikuwa kuwazuia jamaa wasichukue chochote cha maana katika chumba. Jamaa haiwezi kuaminiana. Pia, mtazamo huu wa usasa upo katika maisha ya Asha. Ni mfanyabiashara mashuhuri anayemiliki, *Hotel Victoria,* hoteli ya kifahari. Anapenda anasa kama kunywa bia, kula vizuri, kucheza densi na kufanya ngono na wanaume wenye pesa kama Ngoma na Msafiri. Hajawahi kuolewa kwa sababu hawapendi wanaume wala kuchungwa. Kwa vile anapenda starehe, ana mazoea ya kubadilisha wanaume. Msafiri alimuuliza:

> "Wewe una mume?"
>
> "Hapana. Sipendi wanaume," Asha alimjibu.
>
> "Kwa nini?"
>
> "Sipendi kuchungwa… sipendi utumwa."
>
> (uk.79)

Kilichomfaidi Asha katika mila ni mafunzo aliyopata kutoka kwa nyanyake ambayo ni namna ya kumfurahisha mwanamume. Alipompata mzungu Hastings, akatumia mafunzo hayo kumfurahisha na kisha mzungu akamjengea hoteli. Hata hivyo, tumeona alitumia mafunzo hayo vibaya. Tulifasiri kuwa lengo la nyanyake kumfunza jinsi ya kumfurahisha mwanamume, ni kwa dhamira ya kumfurahisha mumewe ila si kila mwanamume.

Mila na utamaduni hubadilika na nyakati zinavyobadilika. Wanajamii wa riwaya ya *Paradiso* ni wa mwishoni mwa karne ya ishirini. Jamii hii inakumbwa na changamoto kwa kuzingatia kwake desturi na mila za jadi na pia kule kuwepo haja ya kufumbata usasa. Changamoto ya namna hii ina athari hasi katika maisha ya wanajamii wa riwaya ya *Paradiso.*

Desturi na mila za Kiafrika kwenye riwaya hii zinathamini watoto na ikiwa mtu hana watoto wengi huonekana kama hajakamilika (Njue et al; 2007). Jamii huona thamani ya mwanamume katika watoto atakaowazaa. Kulingana na mila na desturi ya Budalangi basi, Mango amewaoa wake wengi na kwa mujibu wa mila yao, mtu kama hangefanya hivyo, basi hangetambulika. Kwa sasa ni vigumu mtu kutekeleza mila na desturi za namna hii kwani maisha ya sasa ni ngumu na yanahitaji mtu kuwa na mapato ya juu. Kuoa wake wengi ni kama kujitia kitanzi. Katika kazi hii,

mwandishi anasimulia jinsi Apondi anakasirishwa na habari kumhusu Sakina. Habari anazodhania ni tetesi kwamba mumewe ana hawara. Mwandishi anaonyesha namna Apondi anavyolalamika kuhusu swala la Mango kuwa na wake wengi huku akiwa hana uwezo wa kuwakimu kwa kuwa na mapato duni:

> "Mtu hana haya na kipato chake kidogo hicho anajilimbikizia wanawake.
> Nyumbani ameshindwa kutuangalia tunatamba sisi na ukoko. Muhogo ni
> huo asubuhi na jioni. Watoto kusoma hawawezi." (uk. 15).

Tulibaini kuwa usasa, unakwaruzana na utamaduni jadi. Kwa mfano, Apondi anapoaga dunia, Mango anatakiwa afungiwe katika chumba na marehemu mkewe pasi na mtu yeyote na kama angeghairi kutekeleza haya, angeimaliza aila yake. Anaonekana kutoridhishwa kukubali kufanya kitendo hicho kwani ni mtumishi wa Mungu. Anawakumbusha wazee kwamba, mambo yalikuwa yamebadilika na watu hawapaswi kuishi katika Budalangi ya ujadi. Wazee nao wanashikilia kwamba ni sharti mila hiyo itimizwe (uk. 92).

Vilevile matatizo kati ya usasa na ukale yanajitokeza pale ambapo Mango anatakiwa kuonja kileo cha busaa ndipo wazee waweze kuendelea na kisha kaburi kuchimbwa. Tena anatakiwa kununua ngombe wa kuchinjwa na mbuzi wa kumpa babake Apondi (uk. 93). Kulingana na utafiti huu, tuliona kwamba, ni vigumu kwa wakati wa sasa mtu kutekeleza yote haya kwani kunahitajika pesa nyingi. Ndiyo maana tunamwona Mango akikabana koo na wazee kuhusu mambo haya kwani ni ya tamaa. Tunakubaliana na mawazo ya Rousseau (1755) kwamba, binadamu anafaa kuongozwa na sheria za kiasili zinazochangia binadamu kuwa mwema. Kwa maoni yetu, wanajamii wanafaa kuasi sheria zote za kiasili zinazomfanya mtu kuwa mbaya kama vile kutawaliwa na tamaa na badala yake waweze kuongozwa na sheria zenye maadili.

Tulivyoona hapa, migongano inayotokana na ushindani kati ya usasa na ukale, ni nyingi sana katika riwaya ya *Paradiso* kuliko *Ua la Faraja*. Mkufya amezungumzia usasa kama Queen kukosa kuolewa na kuleta bwana katika nyumba yake kishaa kufanya nao mapenzi. Anamsawiri Mashaka kama mtu wa ukale anayetaka maiti ya Ngoma kuoshewa katika chumba chake. Naye, Habwe anamsawiri Apondi kama mwanamke anayepinga ukale kwa kutoridhishwa na tabia ya Mango kuwaoa wake wengi kama vile Zuhra na Sakina. Mango anapinga ombi la wazee kumtaka aonje pombe kidogo ndipo wazee waendelee kunywa na pia Mango kulala na maiti ya Apondi.

### 3.1.9 Matatizo ya Mali / Pesa na Tamaa

Matatizo kuhusu umiliki na urithi wa mali yanadhihirika kupitia jamaa wa Mzee Ngoma kwa mfano, Mashaka, Kassim na ukoo wao. Wana tamaa ya mali kwani wanataka kupokonya watoto wa marehemu kaka yao, mali. Uroho wa mali ndiwo unawafanya jamaa ya Ngoma kuwa na kikao cha kuweka mikakati ya kutaka wosia kutoka kwa Omolo. Lengo kuu la kikao ni kwamba wanataka wajue magari yalipokuwa kisha wayachukue na kugawana. Vilevile, tamaa ya kuitwaa mali hiyo inawafanya kutishia kutoutambua wosia ambao Ngoma alimwachia Omolo. Tunakisia kwamba hali kama hii ya Mashaka kutaka kuja kunyakua mali ya Ngoma baadaye, ndiyo inamfanya kutopendelea Ngoma kujadili masuala ya mirathi yake kama angali hai. Tunaelezwa kwamba anapinga hali ya Ngoma kujadili mirathi kama hajafa kwani kufanya hivyo ni kufuru kumtangulia Mungu. Nia ya Mashaka inajitokeza wazi katika mjadala uliokuwa baina yake na Ngoma (uk. 276).

Mashaka anajua fika kuwa endapo mjadala kuhusu mirathi ya mali ungefanywa ilhali Ngoma amefariki, angeliibuka mshindi halafu wangetwaa wanachotaka. Juma ambaye ni mwanawe Ngoma, anashangazwa na hatua ya babake kutomwonea mamake huruma kwani anakataa kumhusisha katika uuzaji wa magari yake au ugavi wa mirathi. Anaonekana kukasirishwa na tabia hii si haba. Mwandishi anatudokezea kwamba, jamaa yake Ngoma wana hamu ya kuivamia mali yake kama angefariki. Ni katika hali hii ambapo tunamuona Omolo akimtahadharisha Juma kwamba mali yao ilikuwa hatarini kutoka kwa ndugu wa Ngoma ambao, hawakuwa na haki ya kuichukua (uk. 238).

Pia, wakati fulani Juma anagombana na Kassim na Mashaka kuhusu pesa. Wanamlaumu kuwa kuwa na pesa za babake na hata kumtaka azitoe kwa ajili ya msiba. Juma anakataa lawama hizo zote na kusema hakuwa na pesa zozote. Kutokana na mabishano hayo, tunaona namna tamaa ya pesa inaweza kuwakosanisha jamaa hasa wakati wa msiba.

Grace naye ana tamaa ya mali kwa vile anahisi kwamba, dadake ana haki ya kupata sehemu ya mirathi kutoka kwa mali ya mumewe; kauli ya Ngoma kutomhusisha dadake katika mirathi na pia kuwa na haki katika mali walizochuma naye kama mkewe, inamtonesha kovu Grace. Mwandishi anatueleza kwamba Grace anahisi:

> "… hana haja tena kuendelea kumhangaikia mtu yule asiye na utu

wowote ndani ya moyo wake." (uk. 224).

Kinachokuwa kero kwa Grace kiasi cha kumchochea kumuacha Ngoma akiwa mgonjwa mahututi ni tamaa ya kumtaka dadake kuhusishwa katika mpango wa kurithi mali. Tunaweza kutamahitisha kuwa, mali ya Ngoma ndiyo kisababishi kikuu cha matatizo ya yeye kutengwa na aila pamoja na jamaa zake.

Tena, tunamuona mhusika Msafiri akiliuza lori lake ili apate pesa za kujitibu. Hii ni baada ya kuzidiwa na ugonjwa wa Ukimwi. Anaambukizwa ugonjwa huu baada ya watu kuwa na tamaa ya pesa na kudanganyika kuwa ugonjwa wa Ukimwi unaponywa. Vilevile, Asha anakosa kumwonea huruma na anapozidiwa na ugonjwa anasafirishwa hadi kwao:

> "… Yule bwana milioni mbili na nusu alizolipwa zilimwishia kama
> mtu alienda kucheza kamari, akaliwa na kurudi mtupu hana kitu…( uk. 206).

Tunaona kwamba Msafiri hasaidiwi. Asha anapenda pesa zake na anapofilisika, mapenzi yao yanafika kikomoni. Rajabu anadokeza:

> "Hata ukiona, waambiwa mke wako anapenda pochi lako siyo utu wako.
> Hata ukoleze mapenzi kwa maneno matamu na vicheko, pochi likiisha
> na yeye anaisha…" (uk. 207).

La muhimu katika mahusiano ya mume na mke ni pesa. Swala la mapenzi ni kama halina mashiko kwani huyeyuka punde umaskini unapobisha hodi.

Aidha, kuna ubadhirifu wa mali kutoka kwa wenye mali wenyewe. Wanafanya hivyo baada ya wao kujionea uharibifu mkubwa wa mali inayowachiwa watoto mayatima. Watu waliokuwa na mali waliitumia wakidhani kwamba wakifa, watoto wao watakuja kutafuta yao wenyewe. Tamaa hii ya kutumia mali jinsi hii inawaacha wana wao mayatima wakiwa na mali kidogo. Tunaelezwa kwamba:

> "… hata wazee, busara yao…baada ya kuona mambo yaliyowapata watoto
> yatima baada ya wazazi wao kufariki… wakaamua kutumia mali walizochuma
> kwa starehe na kuwabakishia watoto kiasi cha kuwakuzia tu..." (uk. 208).

Kutokana na maelezo haya, tunaona kwamba namna mali ilivyotumiwa kwa starehe na anasa, ndivyo kulivyokuwa na kiwango kikubwa cha athari hasi. Kwa mfano, watoto wanasalia pasi na mali ya maana ya wao kurithi na pia kunakuwa na hali ya watu kuambukizana ugonjwa hatari wa Ukimwi. Kwa mfano, Queen anapolemewa na makali ya ugonjwa wa Ukimwi na kukaribia kuonyesha dunia kisogo, anaamua kumwandikia Omolo barua. Katika barua anayompa Bi. Kimaru ili amkabidhi Omolo, anaieleza waziwazi jinsi hati ya mali, nyumba na pesa zake zingerithiwa. Anamshauri Omolo amsaidie mamake kuzipata pesa zake zilizo kwenye benki na marupurupu alikokuwa akifanya kazi; zote zipewe mamake na azitumie kwa furaha. Hata hivyo, mamake hakufurahishwa na maelekezo hayo; anakerwa mno. Tulichukulia kwamba, jambo lililokuwa la maana kwa Bi. Kimaru lilikuwa kama watu wa familia yake wangekuwa hai. Hakuona umuhimu wowote wa pesa na baadhi yao wamekufa na kumuacha katika upweke. Anavyosema: “Furaha niipate wapi na nyote mumeondoka? Mlichonibakishia ni Dadii peke yake.” (uk. 179).

Vilevile, ni bayana kwamba, mali na pesa anazokuwa nazo Queen, inamtenganisha na jamaa zake. Hakuwa akiwatembelea nyumbani kwao wala jamaa yake kuja kumjulia hali katika mtaa wa Tandika. Tuliona kuwa anapougua anamtegemea na kumtumia Omolo. Anampa barua aipeleke kwa mama yake, Bi. Kimaru. Tena, tumeoona kuwa baada ya Omolo kumpeleka mama yake Tandika, wanakumbatiana huku wakitiririkwa na machozi. Hii ni ishara tosha kwamba imekuwa muda mrefu tokea watu wawili hawa wawe pamoja. Kulingana na uchunguzi wetu, tunaweza kusema kwamba kama Queen hangekuwa na pesa nyingi za kumhusisha katika anasa na starehe, jamaa yake ingemkaribia na; wangetembeleana kila mara. Lakini pesa zinamfanya azame katika anasa, kusahau jamaa yake na hatimaye kuambukizwa ugonjwa wa Ukimwi unaompelekea kujitoa uhai. Mawazo haya yanaungwa mkono na ujumbe katika nadharia ya maadili kwamba, ukamilifu wa kitu ni kiwe kizuri na maadili. Maadili inachangia katika ukamilifu wa kitu. Inabainika kwamba, wahusika wengi katika riwaya hii wanakosa maadili, wana upungufu.

Vilevile katika riwaya ya *Paradiso,* kuna matatizo mengi ambayo chanzo ni mali / pesa. Kwa mfano, mhubiri Mango anazozana na Askofu Tonje kwa sababu ya zaka kutoka kwa waumini. Hii inapelekea kugawanyika kwa kanisa. Aidha, Joshua analichukua gari linalofaa kuwa la kanisa na kuwa lake. Matatizo haya pamoja na mengineo yamebainishwa sana katika riwaya hii yamesababishwa na tamaa katika jamii.

### 3.2 Dini na Anasa

Dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna Muumba wa ulimwengu na ndiye mtawala wa kila kilichomo. Aidha, ni mfumo au aina fulani ya imani na njia ya kusali, kuabudu na kumheshimu muumba huyo kama ilivyo, katika dini ya Kiislamu, Kikristo na nyinginezo.

Katika utafiti huu tunamwona Ngoma kama mtu aliyesahau dini anapozama katika ulevi na kujihusisha na mapenzi kiholela. Hakuenda msikitini kuswali. Vilevile, hakushughulika kuwafunza wanawe kanuni za dini ya Kiislamu kama kuwahimiza kusali mara tano kwa siku jinsi inavyohitajika. Kwa kukosa kutimiza haya, kunawafanya watoto wake kutofuata kanuni hizi kwani kama mzazi, anakosa kuwa mfano mzuri wa kuigwa na watoto wake. Kupotoka kwake kunachangia pakubwa watoto wake kutokuwa waswalihina. Baadaye, anasingizia kubadilika na kuwa mshika dini anapogundua kaambukizwa virusi vya Ukimwi na Queen. Hali inayompelekea kutafuta faraja kwa Mungu; kila wakati anatoa sadaka. Anajifanya mshiriki na mshika dini na kisha anamtaka mwanawe kumwiga. Hali hii inazua tofauti baina yao mara tu anapoanza kumshurutisha kuhudhuria sala za alfajiri na zile za jioni kila siku. Juma anakataa kutii kwani huo ulikuwa ni wakati wake wa kwenda sokoni ya Kariakoo kumsaidia mama yake kuchagua na kununua bidhaa za kuuza katika genge. Isitoshe, mwanawe anamwona babake kama mtu katili aliyewatelekeza na pia kujifanya kushika dini baada ya mambo kumwendea mrama. Kutokana na matukio haya, tunaona kwamba hali ya mzazi kutumia nguvu zaidi kupita kiasi ili mwanawe atende kulingana na matakwa yake, inazua ugomvi na chuki baina yao. Ngoma kwa mfano, anamkorofisha Juma siku ya Ijumaa eti alikosa kwenda msikitini kusali. Hali hii inaibua majibizano makali baina yao tena yaliyojaa bezo (uk.117- 118).

Mwandishi anatuarifu kwamba, matamshi ya Mzee Ngoma yalimkasirisha Juma sana. Hii ni kwa sababu alimchukulia kuwa mnafiki, mzinzi na kutokuwa na haki ya kuwafundisha mambo ya imani. Aliiona nafsi ya Ngoma kama iliutukuza uovu. Ni katika hali hii Ngoma alichukua kibao ili kumwadhibu kwa kumpiga kichwani. Hata hivyo, Juma aliponea chupuchupu kwa kukwepa, kutoroka na kuenda kuishi kwa babu yake. Tumeona kuwa mzazi anapokosea na kuwasingizia watoto, hali hii huzua matatizo zaidi. Watoto huwa wanachunguza na pia kuelewa ni nani mwenye makosa. Utumizi wa nguvu kama kuwashurutisha kutenda jambo wasilotaka, hauwezi kufaulu na badala yake unavundisha mambo. Katika utafiti huu, tulichukulia maoni ya Leo Tolstoy (1960) kuwa ya manufaa anaposema kwamba, dini ni ya muhimu sana kwa vile huleta umoja baina ya

watu ambao hukisiwa ni sawa. Ngoma na familia yake wako sawa kwani wote ni wanadamu. Kwa sababu hii, anafaa kuweka dini mbele kuanzia mwanzo. Kutowafudisha watoto wake dini hapo mwanzo imechangia kuwepo kwa matatizo mengi katika familia yake.

Habwe anarejelea hali ya watumishi wa Mungu na familia zao kushiriki na kupenda anasa kupita kiasi. Wote wamepakwa uchafu wa anasa kwa kiwango kikubwa. Michael anapomuombea Amuka na suluhu kuhusu matatizo yake kupatikana, anaamua kumpa zawadi ya gari ambalo anakataa kulichukua. Baadaye, anaomba liondolewe kanisani ambapo linakabidhiwa Joshua kwa niaba ya kanisa. La kushangaza ni kwamba, gari hilo baadaye, linamilikiwa na familia ya Joshua kwani kila wakati linaendeshwa na Lona. Gari ambalo lingetumiwa kutekeleza kazi za kanisa, linabadilika na kutumiwa na mtu binafsi. Kisababishi kikuu kikiwa kutawaliwa na tamaa ya anasa.

Isitoshe, Joshua akiwa ni mpenda anasa, anajenga nyumba ya kifahari katika mtaa wa Woodley. Nyumba inayosambaa katika uga wa ekari moja. Vilevile, anasa inamfanya kuitumikia familia yake kwanza badala ya kumfanyia Mungu kazi katika nafasi hiyo na; kujichumia mali. Baadaye, anagundua kwamba, yote anayotekeleza yalikuwa kazi bure kwani anahisi alikuwa akifuata mambo ya ulimwengu na inakuwa ni kama kufuata upepo kwa vile nyumba hiyo, tayari inaanza kumchusha. Katika nyumba hiyo, hakukuwa na furaha kwani paliishi yeye, mkewe na Njoki, mjakazi wao. Hali hii inamkosesha furaha kiasi kwamba anaenda katika msitu wa Ngong kutalii mawazo yake ili ajue maana ya Ukristo ambao alikuwa ameanza kuutilia shaka. Anajuta kwa kujisemea:

> "Ni kweli nimemhadaa Mungu kwa siku nyingi. Nilikuwa siku zote
> hizo nafikiri nawajengea Nice na Judy maisha ya baadaye kwa
> kuwawekea viekezaji vya uchumi. Kumbe yote ni kazi bure." (uk. 103).

Kwa mujibu wa maneno haya, ni ukweli kwamba mja hawezi kumhadaa Mungu. Mwanadamu anafaa kumtumikia Mungu kwanza. Ndipo afaulu kutekeleza haya, anapaswa kuwa mwaminifu na pia atende haki ili kuepuka majuto hapo baadaye. Joshua akiwa Askofu, anakosa kumfanyia Mungu kazi na badala yake anatumia wakati wake mwingi kuekezea wanawe uchumi. Hii ni ishara fika kwamba ni mpotovu wa maadili. Tena, kulingana na uchunguzi tulioufanya, tuliona kuwa mwishowe, anajuta sana kufuatia hatua anayochukua baada ya mkewe kumwendea kinyume na kuzaa na wanaume wengine. Tukio hili linamfanya kupuuzilia mbali mapenzi kutoka kwa mkewe.

Wanandoa hawa wanavaa nguo za thamani kinyume na jinsi wanavyopaswa kuvaa wakiwa watumishi wa Mungu. Wanatembea kwa namna tofauti, wanahodhi pesa nyingi, magari na nyumba za kukodisha. Zaidi ya hayo, wanakula chakula kizuri kinachoashiria kuwa hawakuwa na matumaini na maisha ya ahera. Lona anatawaliwa na tamaa ya vitu vya dunia na kwa sababu hii hajali hata kuchukua hongo, kutumia matusi, kuua wala kudanganya. Wote anasa inawafanya kupoteza nadhiri ya kutenda mema. Hivi ni kusema kwamba, kwa kutumia vigezo hivi vya maisha, wanatenda kinyume na matakwa ya dini.

Hata baada ya Joshua na Lona kuionyesha dunia kisogo na Boribori kutua uongozi wa kanisa la New Jerusalem Church, anajihusisha katika biashara haramu ya kuuza mihadarati. Anafanya hivyo ili apate pesa nyingi zaidi zitakazomfanya aishi maisha ya anasa. Kwa bahati mbaya ananaswa na maofisa wa polisi na kufikishwa mahakamani, kushtakiwa na kufungwa jela pamoja na mkewe. Kifungo kinawafanya kuacha kumtumikia Mungu. Ni ukweli kwamba, anasa humshurutisha mtu kutenda maovu ili apate pesa za kutumia katika starehe. Mwanadamu anapofanya hivyo, hawezi kuihudumia dini ipasavyo kama Joshua na Lona wanavyofeli.

Tena, tumeona kwamba, mawimbi ya anasa hayakumtenga Michael kwani alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Patricia. Wanazuru mji wa Kisumu na kuonekana katika hoteli ya kifahari ya Sunset. Huu ni ushahidi tosha kwamba, hakutumia wakati wake sawasawa kumtumikia Mungu. Matokeo ya anasa yaani uja uzito wa Patricia unamsababishia matatizo ya kiakili na kukosa utulivu. Kutokana na uchanganuzi huu, tumeona kuwa, matatizo yanayotokana na dini na anasa ni mengi sana katika riwaya ya *Paradiso* kuliko *Ua la Faraja.* Hii ni kwa sababu, Habwe alinuia kuonyesha maovu yanayotendwa na watu wanaojichukua kuwa washika dini.

### 3.2.1 Mapenzi na Wivu

Mapenzi katika muktadha huu yanachukuliwa kuwa ni mahaba kati ya mwanamume na mwanamke. Mwanamume anaweza kuwa mume na mwanamke akawa mke. Wanapokuwa na uhusiano wa kimahaba, huwa na mvuto wa hisia kati yao. Wakati mwingine mahaba huanza kuwa na mvuto wa juu na pia kufifia muda unavyosonga mbele. Hali kama hii huwafanya wapendanao kukumbwa na changamoto. Kwa mfano, uhusiano wa wapendanao huingiliwa na wenye wivu na kuonewa gere.

Mango ana tamaa ya wanawake kwani ameoa wake wengi. Wanaoneana wivu. Kwa mfano, kuna husda kati ya Apondi na Zuhra. Wivu kati yao unaonekana wakati Apondi anapoonyesha kumchukia Zuhra wakati Mango na Apondi wanapowasili kwa Zuhra. Anamwona Zuhra kama mwizi aliyeingia mawindo pake (uk. 13). Tena Apondi anamwonea Sakina wivu na pia kushangazwa na umuhimu wa uhusiano wake na Mango. Anauita usaidizi anaoutoa wizi (uk.15). Apondi anamlaumu Mango kuwa na wake wengi ilhali ana kipato cha chini. Tendo linalomfanya kutowasomesha watoto wao na hata kuwapa lishe nzuri. Mwandishi anatuarifu kwamba:

> "Apondi alionyesha hasira ya wazi. Ama ni kweli walivyosema uke-wenza ni sumu baridi. Apondi alionekana kama aliyechomwa na msumari wa moto. Pumzi zilimwenda mbio kwa maudhi aliyokuwa nayo." (uk. 16).

Kutokana na maneno haya, tulichukulia kwamba mahusiano ya kimapenzi ya wahusika wengi yanazua matatizo ya wivu na chuki kwa sababu ya tamaa anuwai. Aidha kuna taswira inayomwonyesha Patricia anamwonea Lydia kinyongo kwani amefanikiwa kupata mume mzuri. Anashangazwa na sababu ya yeye kukosa bahati. Tamaa ya kuwa na mume kama Michael inamshinikiza hadi anapalilia mahaba naye, kisha kuwa mja mzito na kumzaa Mango Junior. Katika utafiti huu, tumechukulia kwamba tamaa ya kumnyakua mume wa rafiki yake, unasababisha migogoro baina ya familia na marafiki. Tumeshuhudia vilivyo kwamba, katika riwaya ya *Paradiso* wivu wa mapenzi ni mambo yenye athari hasi. Hii ni kwa sababu, wahusika wanachongeana, wanachukiana, wanachocheana na hata kupigana. Swala la kinyongo katika mahaba halifurahishi wala kuridhisha. Zaidi ya yote, linatamausha. Vaughn (2008) anadai nadharia ya maadili inazungumzia na kueleza namna ya watu kuishi vizuri. Ili waishi kwa upendo, lazima wawe na maadili mema. Watu wanaweza kutimiza haya ikiwa hawana wivu ama kufanya mambo yanayoweza kuiibua wivu miongoni mwao.

Naye, Mkufya ameshughulikia tatizo la mapenzi na wivu kwa ufupi sana. Kwa mfano, anasimulia tukio la Ngoma kugundua kwamba Queen ana uhusiano wa kimapenzi na Omolo kisha Ngoma anamchukia Omolo.

## 3.3 Hitimisho

Katika sura hii ya pili, tumetaja na kuchanganua baadhi ya matatizo yanayopatikana katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso*. Kuna uwiano mkubwa na tofauti kiasi wa matatizo haya. Huenda hali imekuwa hivi kwa sababu, waandishi Mkufya na Habwe, wote ni wenyeji wa nchi za Afrika Mashariki na wamekulia katika mazingira sawa ambayo yamewapa tajriba sawa katika maisha yao. Vilevile, matatizo haya yamechanganuliwa kwa kuzingatia riwaya zote mbili katika sehemu moja. Katika kufanya hivi, tumeweza kubaini uwiano na tofauti ulioko katika matatizo haya kwa kueleza vianzo na athari zake katika jamii. Tumegundua kwamba, matatizo katika riwaya hizi yanayosababishwa na tamaa. Kulingana na nadharia ya maadili, riwaya hizi zimesawiri matatizo yanayoibuka ikiwa jamii haina maadili. Umuhimu wa maadili ni kutusaidia kuepuka uibukaji wa aina hii ya matatizo. (Wamitila 2003 ; Wafula na Njogu 2007 na Vaughn 2008).

## SURA YA NNE

## USHAURI DHIDI YA ATHARI ZA TAMAA KATIKA *UA LA FARAJA* NA *PARADISO*

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumebaini njia zilizotumiwa kuchimuza tamaa na athari zake katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Mwelekeo huu umetolewa baada ya uchambuzi na ulinganishi wa kazi hizi mbili uliyoongozwa na nadharia ya maadili kuonyesha kuwa wasanii Mkufya na Habwe wametaja njia na kutoa ushauri katika kazi zao kuhusu namna ya kupiga vita maovu. Hisia dhidi ya maovu katika riwaya hizi ni za karibu sana na waandishi hawa wamebaini njia zinazofanana za namna ya kukomesha uozo huu katika jamii. Wamelishughulikia suala hili la tamaa kwa namna mbalimbali kama ukweli, kuchukua tahadhari, ushirikiano, utamaushi, tamaa ya pesa, msamaha, usawiri wa wahusika wa kitanzia, maombi na nyinginezo.

### *4.1* Ushauri Dhidi ya Tamaa na athari zake katika *Ua la Faraja*

#### 4.1.1 Ukweli kuhusu Ugonjwa Hatari wa Ukimwi

Baadhi ya wahusika katika *Ua la Faraja* wanakabiliwa na changamoto ya ugonjwa wa Ukimwi. Ugonjwa huu upo na umewafanya wahasiriwa wengi kuteseka na hali hii kuwa changamoto kwa wanandoa. Ukimwi unaenezwa kupitia tendo la ngono pasi na kinga. Mume au mke anauwezo wa kuambukizwa na kisha kumwambukiza mwana ndoa mwenziwe. Baada ya kuambukizwa, mtu huanza kuugua. Dalili zinazoonyesha kwamba mtu kaambukizwa virusi vya ugonjwa huu ni kuanza kukohoa kikohozi kisichokoma, kuugua na kifua kikuu, kukonda na kukondeana, kutokwa na upele, kuendesha sana na hatimaye kufa ikiwa hakuna hatua za dharura za matibabu zitakazochukuliwa. Ni vema kusema kuwa, hadi sasa ugonjwa huu hauna tiba. Ni bora watu watahadharishwe kwamba, unaua. Dawa ambazo zimefanyiwa uchunguzi na kuruhusiwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) ni zile zinazopunguza makali ya ugonjwa huu. Kile mhasiriwa anachotakiwa kufanya ni kufuata ushauri wa daktari kuhusu ugonjwa huu. Kwanza, akubali ukweli wa mambo kuwa yeye ni mgonjwa. Pili, atumie dawa kulingana na maagizo na ushauri wa daktari. Tatu, asithubutu kunuia kueneza ugonjwa huu wa Ukimwi. Nne, ikilazimu kushiriki ngono, afanye hivyo na mwenzake aliye naye katika ndoa au atumie mpira. Tano, azingatie ushauri nasaha kutoka kwa daktari na watalaamu wengine kuhusu janga hili. Na sita,

akubali kwamba ugonjwa huu ni kama magonjwa mengine. Akifuata ushauri wa daktari anaweza kuishi vyema huenda asife kwa sababu ya ukimwi. Mhasiriwa anahitajika kula vizuri na asiwe na mawazo mengi. Vilevile, asithubutu kuusambaza, kwani akifanya hivyo atakuwa anapunguza nguvu za kinga katika mwili wake na kuuweka mwili wake katika hali hatari ya mambukizi zaidi. Pia, si maadili mema kuwambukiza watu wengine kimaksudi. Watu wanafaa kufahamu fika kwamba, mtu akiambukizwa ugonjwa huu mambo yafuatayo hutokea: kuna kutengwa na wenzake, kuchekwa, kusemwa sana na kutatizika kisaikolojia. Wahasiriwa wanashauriwa kuwa tayari kwa athari hizi zote. Hata hivyo, akitumia dawa ipasavyo, mgonjwa anaweza kurefusha maisha yake na pia kumwezesha kuwalea na kuwasomesha watoto wake. Kwa upande mwingine, endapo mgonjwa hatafuata ushauri wa daktari, basi atakufa na kuwaacha watoto wake wakiwa mayatima. Wale hawajaambukizwa wanahitajika kujiepusha na tendo la ngono kabla kuolewa au kupimwa damu na kuhakikisha kwamba wako sawa. Tena, wahakikishe wamekoma kushiriki ukahaba au ngono bila kinga. Mathalan, katika riwaya hii, Queen anamwambukiza Ngoma virusi vya ugonjwa huu, naye anamwambukiza mkewe, Tabu na pia Asha. Asha anawaambukiza watu wengine kama vile Msafiri. Wahusika wengine wanaoambukizwa virusi ni pamoja na Chiku na Pendo. Wote hawa inaaminika kuionyesha dunia kisogo. Tabu ni kielelezo cha wahasiriwa wanaofuata ushauri wa daktari na kuweza kuishi kwa muda na hata kuwashughulikia wanawe. Ni mfano wa mwenezaji maadili kama alivyoamini Aristotle katika nadharia ya maadili anasema kwamba, binadamu anafaa kuiga mema na kuacha mabaya. Watu wakitenda mema maishani wataepukana matatizo mengi. Habwe hajatoa ushauri kuhusu Ukimwi kwa sababu hakuna kisa wala janga la Ukimwi katika kazi yake.

### 4.1.2 Tahadhari Dhidi ya Ugonjwa wa Ukimwi

Tahadhari ni mojawapo ya maadili muhimu katika jamii. Neno hili hutumiwa kila mara tunapozungumzia mathalan watu watahadhari palipo na hatari na kadhalika. Hapa neno tahadhari linatumika kama onyo kwamba kuwa macho kuonyesha kuwa mtu amewajibika na basi ni mwadilifu na ikiwa haajibiki, si mwadilifu. Mtu aliyetahadhari anaweza kutegemewa katika kufanya maamuzi na pia kutenda matendo anuwai kwa njia iliyo adilifu. Tukizingatia kigezo cha maisha, mtu aliyetahadhari ni yule anayeweza kuaminiwa katika kuvumbua/ kuanzisha jambo na tena kuchukulia majukumu yake kwa makini. Isitoshe, mtu aliyetahadhari huchukuliwa na hutumika kama kielelezo cha uadilifu. Mtu wa aina huyu hutathmini matendo yake ya awali kwa

makini kiasi kwamba hukubali iwapo amekosa kisha kuchukuliwa majukumu apewayo kwa tahadhari kwa kuwaza anapaswa kutenda nini na vipi ili matokeo yawe yanayofaa. Mtu asiyetahadhari ni yule asiyechukulia maisha yake kwa uangalifu. Tahadhari basi inaweza kuchunguzwa kutumia nadharia ya maadili kwa vile inahusu mtu kuwa muadilifu.

Kwa maoni yetu, Mkufya anazungumzia swala la tahadhari katika riwaya yake ya *Ua la Faraja*. Riwaya hii inasimulia kuwa kuna wahusika ambao hawakutahadhari katika maisha yao, na hatima yao ikawa kukitia mchanga kitumbua chao. Anarejelea mfano wa Ngoma, Queen, Asha, Pendo, Chiku, Msafiri na kadhalika. Wote hawa wanahusika katika tendo la ngono pasi na tahadhari ya kutumia kinga kisha wanaambukizwa virusi vya Ukimwi. Mhusika Queen anamtahadharisha Omolo kwamba, atafute msichana mzuri, wapime damu kuhakikisha kwamba hawana virusi hivi kisha aoe na awe na familia. Vilevile, mhusika Jose anauza kondomu za kutumia wakati wa mahaba kama tahadhari dhidi ya ugonjwa huu hatari. Wasomaji pia wanatahadharishwa wasikose kuwajibika kuhusu mapenzi, la sivyo watajuta namna wahusika hawa walivyojuta kwa sababu ya tamaa zao. Maoni haya yanatiliwa mkazo na mawazo ya J.J. Rousseau (1962) katika nadharia ya maadili kwamba, ili mtu aonekana mwema ni lazima atende mema. Kwa mujibu huu, wanajamii wanapaswa kutenda mema ili waweze kuonekana ni watu wazuri. Habwe hajatoa ushauri wowote kuhusu Ukimwi kwa vile hajalishughulikia.

#### 4.1.3 Ushirikiano

Kwa mujibu wa Gwako (2016: 62), ushirikiano unachukuliwa kama hali ya watu kuungana na kusaidiana kufanya jambo. Ili watu washirikiane ni lazima kuwe na uhusiano mwema / mlahaka mwema na uelewano ya wanaohusika. Mkufya anasisitiza umuhimu wa mlahaka mwema / uhusiano mwema na ushirikiano katika kila jambo. Anarejelea Omolo kama mhusika aliye na mlahaka mwema wa kushirikiana na watu. Kwa mfano, anawasaidia Queen na Ngoma wanapougua (uk.134- 144, 216- 218).

Mwandishi anaonyesha tabia ya jamaa ya Ngoma kutoshirikiana na jamaa ya Tabu katika mazishi ya Tabu kwa madai kwamba wametengwa katika ugawi wa urithi. Tamaa ya mali inawafanya kuichukia familia ya Ngoma. Tena wanasherehekea wanaposikia Ngoma ni mgonjwa (uk.215). Mwandishi anaonekana kupinga tabia ya namna hii kwani inabomoa mshikamano wa familia na kufanya hali ya mambo kuwa magumu. Anahimiza ushirikiano kutoka kwa marafiki kama daktari

Hans wanaokuwa na familia yake Ngoma wakati wa kuugua na hata msiba wake. Aidha, Mkufya anaonyesha wazi kwamba si rahisi mtu kufanikiwa akiwa peke yake. Ni muhimu tena lazima kuungana na kusaidiana na wenzake. Anaangazia jamaa ya Ngoma kuhudhuria na kushiriki mazishi yake. Yote haya ni thibitisho tosha kwamba uhusiano na ushirikiano ni jambo muhimu mno hasa katika jamii (uk. 301-303).

Kwa upande mwingine anapiga vita hali ya jamaa kama vile Mashaka na Rukia kutawaliwa na tamaa ya kutaka kutua mali wakati wa maombolezi (uk.302-303). Isitoshe, kuna tabia ya madugu kususia kumtembelea Ngoma anapougua. Ushahidi kuhusu kutelekezwa anapougua unapatikana anapolalamika, “Nimekuwa kama sina ndugu.” (uk.273).

Pia, ushirikano kutoka kwa wanajamii wakati wa msiba wa matanga umeangaziwa na mwandishi Habwe katika kitabu chake cha *Paradiso* kuhusu mazishi ya Apondi. Kanisa alikoshiriki inafika, bwanake, mwanawe na hata viongozi wa eneo hilo wanafika kumuomboleza. Tena, analopinga mwandishi ni tamaa ya waombolezaji hawa yaani tamaa ya mali na ulafi

Naye, Karinge (2013: 88), anachukulia ushirikiano na mahusiano ya kijamii kama ni mfano wa ujamaa katika jamii ya kimapokeo ya Kiafrika ambao unasababisha uhusika wa kila mwanajamii katika maisha ya jamaa yake. Kwa maoni yake, kila mmoja ana haki ya kusaidiwa kwa kila njia na jamaa yake. Pia ni jukumu la anayesaidiwa kuwasaidia watu wanyonge vilevile. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mfano maridhawa unaoangaziwa ni wa Asha na Catherine kuanzisha hazina ya mayatima ili kuwasaidia mayatima kujua namna ya kutumia mirathi yao (uk. 307). Mwandishi anapinga hali ya watu kuwa na tamaa ya vitu kwani inavunja hali ya kuwa na ushirikiano (uk.215). Wasemavyo Njogu na Chimerah katika nadharia ya maadili ni kwamba, wanadamu pamoja na viumbe wote walio hai, wana sifa ya kitu kiitwacho tabia wasichozaliwa nacho. Mtu hujifunza tabia ambayo ni aina mbili, chanya na hasi. Kwa maoni yetu, mtu anafaa kujifunza tabia chanya iliyo ya manufaa kwa jamii na kuacha tabia hasi inayosababisha maovu. Kwa mujibu huu, jamii inashauriwa kutenda mema kama vile kuacha tamaa. Kutokana na maelezo haya, tumebaini kwamba, ushirikiano umeshughulikiwa sawa katika riwaya ya *Ua la Faraja* na *Paradiso.*

### 4.1.4 Kutopoteza Matumaini Maishani

Mtu hukata tamaa ikiwa hali ya maisha imekuwa ngumu. Ugumu wa maisha huweza kusababishwa na ukosefu wa pesa na hata mahitaji mengine muhimu kama mavazi, chakula na makazi. Mara nyingi watu hutamauka wanapokuwa wagonjwa. Maumivu yanayosababishwa na ugonjwa usiosikia tiba humfanya mtu kutamauka. Watu wanahimizwa kutotamauka maishani wanapokabiliwa na hali gumu ya namna hii. Mwandishi amewatumia wahusika daktari Hans, Tabu na Queen kama mfano wa kuwahimiza wanajamii kutotamauka. Hans anamweleza Tabu kwamba akitumia dawa ya kupunguza makali ya ukimwi ipasavyo, huenda akaishi hata zaidi na kifo chake kisiwe kitasababishwa na ukimwi (uk. 194). Anafuata ushauri nasaha anaopokezwa na Hans kama daktari bila mapuuza hata chembe. Anapohisi vibaya, humwendea Hans na kutaka ushauri (uk. 183-198). Hii inamfanya kuwa na matumaini ya kuishi kwa muda na kuwatunza wanawe hadi wawe wakubwa. Inabainika kwamba mwandishi haridhishwi na hatua anayochukua Queen ya kujitoa uhai kwa sababu ya kutamauka. Anamsawiri kama mtu aliye na dhana baya kuhusu maisha. Anajishawishi kwamba maisha hayana maana na ndipo anaamua kujitoa uhai (uk.68-69; 141-142). Kwa mujibu wa mwandishi, watu wanapaswa kuwa wavumilivu wanapopatwa na janga kama la ukimwi. Wanastahili kumeza dawa kulingana na ushauri wa daktari, kupata ushauri nasaha, kukubali hali yao, kuwa na matumaini ya kuishi na kuwa wavumilivu. Mhasiriwa pamoja na jamii kwa jumla haipaswi kukata tamaa kinyume na isemavyo mhimili huu kwamba, 'uzuri au ubaya wa kitendo inalingana na jamii'. Mtu hapaswi kujitoa uhai kwa kisingizio kuwa kitendo kama hicho kwake ni cha kawaida. Kujitoa uhai ni haramu mbele ya Maulana na hata sheria za nchi, hivyo basi, si maadili.

Askofu Joshua anaonekana kupoteza matumaini kuhusu maisha. Hii ndiyo maana anaenda katika msitu kwenda kusaka nafsi yake kuhusu bidii yake. Amewatengezea Nice na dadake maisha, kumbe yote ni kama kazi bure. Nice na Judy si watoto wake. Hali ya kwenda katika msitu inaashiria hali ya hatari. Tumechukulia kwamba, huenda anafikiria kujiua kwa sababu ya kutamauka. Tofauti kati ya visa hivi viwili katika *Ua la Faraja* na *Paradiso* ni kwamba, Queen anajiua kwa kupoteza matumaini ya kuishi. Joshua hajiui kwa sababu ya kutamauka badala yake baada ya kujitambua na kujijua anarudi kwake nyumbani. Kujiua si maadili.

### 4.1.5 Mipango katika Maisha

Mtu anapotaka kufanya jambo ni sharti awe na kanuni fulani za kumwongoza. Hii ni ikiwa anatarajia matokeo mema yanayofaa na yanayokubaliwa na wanajamii. Uzingativu wa mpango huchukuliwa kama uadilifu kwani ni nadra sana kwa jambo linalofanywa kwa mpango kuwa na matokeo yasiyoridhisha. Wanajamii wanahimizwa kuwa na mpango wanapotaka kufanya jambo lolote. Wasitawaliwe na tamaa. Ni kwa sababu hii Mkufya anamtumia mhusika Ngoma kama kielelezo cha mtu anayekosa mpango wa matumizi ya pesa yake na kushiriki kuiletea familia yake balaa. Kwa mfano, ana pesa nyingi lakini hazifai familia yake. Anakunywa pombe sana, kushiriki ukahaba na pia kuitelekeza aila yake. Mwisho, anaambukizwa virusi vya ugonjwa hatari wa Ukimwi na kuishia kumwambukiza mkewe, Tabu. Uambukizi huu unasababisha vifo kwao wawili na kuwalazimu wana wao kusalia mayatima. Kama Ngoma angekuwa na mpango, uozo huu wote haungetendeka. Tunapokuwa na pesa ni bora tuwe na mpango ili kuepuka janga la namna hii. Tukirejelea mhimili katika nadharia ya maadili unaosema, ‘dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga jamii kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii’, mhimili huu unakoleza mawazo ya Mkufya ya kuandika mambo yanayoijenga jamii kama vile, kuitaka iwe na mpango mzuri maishani na kukemea uovu wa kukosa mpango wa kutenda mema maishani kama anavyokosa Ngoma.

Mhusika Queen, vilevile anakosa kuwa na mpango. Hata baada ya kukamilisha masomo na kupata kazi, hakujihusisha na mpango wa kupata jiko. Baadala ya kufanya hivyo, licha ya kuwa na pesa nyingi anajitoma katika anasa ya ulevi na kushiriki ngono pasi na kinga. Hatima yake ikawa ni kuambukizwa virusi vya Ukimwi. Hii inamfanya kuugua, kuteseka, kutorokwa, kukejeliwa, kusemwa vibaya, kuchekwa na mwisho kujitoa uhai kwa sababu ya kutamauka. Mwandishi amemtumia Queen kama kielelezo cha watu wanaosoma na kupata kazi kisha kukosa mpango katika maisha hata baada ya kuwa na pesa nyingi. Queen anafariki kama hana mume wala mtoto. Wasomi wanahizwa kuwa na mpango wanapofanya kazi na kuwa na pesa nyingi. Wajiepushe kutawaliwa na tamaa. Mtu aliye na mpango, huepuka soni kwa kufanya mambo ipasavyo. Kwa kuwatumia wahusika kama Omolo, Hans, Tabu na Grace kama vielelezo ya watu waliokuwa na mpango na kufaulu kwa njia moja au nyingine, mwandishi anawahimiza watu kuwaiga na kujiepusha na tamaa isababishayo fedheha. Habwe, amewasawiri wahusika kadha ambao wana mipango maishani kisha wamefaulu na wale ambao hawana mipango na kukosa kufaulu. Mango

anakosa kufaulu maishani kwa sababu ya kuoa wake wengi. Joshua anakuwa na mipango ya kuwajengea watoto wake maisha bila kujua si wa damu yake. Boribori anajihusisha katika ulanguzi wa madawa ya kulevya ili apate pesa nyingi hatimaye mpango huu mbaya unamfanya kunaswa na polisi kisha kushtakiwa na kufungwa. Kutokana na utafiti huu, tumebaini kwamba suala la mipango katika maisha limerejelewa sawa na waandishi wote wawili kwani wamezungumzia matukio tofautitofauti kuihusu.

### 4.1.6 Kutowambukiza watu wengine Virusi vya Ukimwi

Takwimu za WHO (UNAIDS) zinaonyesha kwamba mwaka wa 2018 watu 25.7 milioni walikuwa wanaishi na virusi vya Ukimwi katika kanda la Mashariki na Kusini mwa Afrika. Na idadi ya 470, 000 wameaga dunia na unaenea kwa kasi sana. Sababu ya kuonea hivyo imetajwa kuwa: huenezwa kimakusudi kwa watu wasiokuwa nao hasa kupitia tendo la ngono. Umaskini umetajwa na kulaumiwa katika kuchangia sana kuenea kwa ugonjwa huu hatari. Mkufya, amewatumia wahusika kadha katika riwaya hii kama wasaka hela / tonge walioambukizwa virusi vya ugonjwa wa ukimwi na mwisho wakaenda jongomeo. Hawa ni pamoja na Pendo na Chiku. Wao pia ni pingamizi na kizingiti kikubwa katika kutumia kondomu wakati wa ngono sababu kuu ikiwa wanadhamiria kueneza ugonjwa huu wa Ukimwi. Kutokana na fasiri yetu, wahusika hawa wanapata kufaulu kutekeleza maovu haya kwani, mazingira wanamofanyia kazi, yanawapendelea watu hasa wakilewa, huwa hawana mwelekeo. Tena, wao hujilazimisha na pia kuwashawishi wateja kushiriki mahaba nao. Ili tuweze kudhibiti aina hii ya tamaa na athari zake katika jamii, tunapaswa kuwa na mikakati sawasawa. Mwandishi, anabainisha wazo la kutowaambukiza watu wengine virusi vya ugonjwa huu wa ukimwi, kwani kuwambukiza wengine kimakusudi ni tendo la kukosa maadili. Mkufya anamwangazia Tabu kama mhusika ambaye hakuwambukiza watu wengine virusi vya ugonjwa huu, hasa kimakusudi. Wahusika wengine wanaoonekana kupiga vita mambukizi ya kimakusudi ni Daktari Hans, Grace na hata Omolo. Naye, Queen baada ya kuwambukiza watu wengine virusi vya ugonjwa huu na kupitia machungu ya makali yake, anangamua kwamba kufanya hivyo ni kukosa utu, jambo lisilokubaliwa na si uadilifu. Yeye pia anaanza kushauri wanaotaka kuoa kupima damu kabla ya kufanya hivyo. Waoe, wawe na familia na wajiepushe na kumangamanga. Jamii inahimizwa kwa sauti moja kuipiga vita maambukizi ya kiholela. Inaweza kufaulu kufanya hivyo wakitumia mawazo ya Plato na Tolstoy katika nadharia ya maadili kwamba, jukumu kuu la nadharia hii ni kuelezea namna ya kutatua matatizo ya jamii.

Nadharia ya maadili imeeleza bayana namna mtu anafaa kuishi. Anapaswa kuwa na maadili yaani kutenda mema. Habwe, hajatoa ushauri kuhusu janga la Ukimwi kwa sababu hajalishughulikia.

**4.1.7 Kutokuwa na Tamaa ya Pesa / Mali**

Mtu anapotawaliwa na tamaa huwa si mwadilifu tena. Tamaa / uroho humfanya mtu kupoteza mwelekeo na badala ya kufanya jambo ipasavyo, hufanya kinyume. Hali kama hii huwaacha watu wakilalamika kuhusu utendakazi wa aina hii. Tunaweza kusema kwamba, tamaa husababisha wengine kudhulumiwa. Wanaopaswa kupata kitu fulani hukosa na wanaostahili kukosa, hupata. Hali kama hii huzalisha chuki, ulazaji damu, lawama na mateso. Kwa mujibu wa mwanafalsafa Immanuel Kant katika nadharia ya maadili, 'kitu kinachoidhibiti akili ya mwanadamu ni dhamira au kusudio (bora kuliko matilaba)'. Hii ina maana kwamba, ni fikira inaamua tendo ambalo ni la kimaadili. Kwa kufuata usemi huu wa Kant, ni vyema mtu kufikiri kutenda tendo lisilokera. Mtu akifanya vizuri itakuwa ni uadilifu. Watu wasitawaliwe na tamaa ya pesa / mali. Ushauri huu ni wa thamani sana kwa yeyote anayetarajia baraka kutoka kwa wanajamii. Mkufya anawahimiza wanajamii kujiepusha kuwa na tamaa hasa ya pesa / mali.

Kwa mujibu wa Kanyange (2016: 33), tendo la tamaa ya pesa linaweza likatathminiwa kuwa uadilifu kwa misingi zifuatazo: Kwanza, utumiaji wa kigezo cha ubinadamu. Katika kigezo hiki, mhusika mwenye tamaa ya pesa ni mtu anayetarajiwa kuwa na uwezo wa kutofautisha kile kilicho zuri na baya kuthibiti hisia zake za mali / pesa. Aidha, wanajamii hawa wana uhuru wa kuchagua waongozwe na tamaa yao ya mali / pesa za haraka ama wavumilie wazitafute pesa/ mali kwa njia iliyo halali. Pili, ni kigezo cha fikira zilizo na urazini wahusika wanapoamua kukubali kutawaliwa na hisia zao za tamaa ya pesa / mali inayowafanya kushiriki katika hali isiyo halali huwa katika ufahamu kamili kufanya hivyo, tunawatarajia waweze kufanya uamuzi wa busara wa kutokuwa na tamaa. Katika kufanya hivyo, tendo kama hili linaweza likabainishwa kama ni adilifu au si adilifu.

Tunaweza kusema kwamba, kichocheo kikuu cha wahusika cha kuwa na uchu wa mali / pesa ni kupunguza uchungu wanaohisi kwa kutokuwa na mali / pesa kwa vile wanatarajia kuwa na mali / pesa nyingi. Matarajio yao ni kwamba kuwa na pesa nyingi kutawapunguzia uchungu.

Vilevile, tunaweza kutumia pia vigezo vya kupima kiasi cha uchungu uongezwao ama upunguzwao na tendo fulani; tendo la kuwa na tamaa ya pesa / mali lina athari anuwai, kama zifuatazo: kwa kuzingatia kigezo cha ukali, uchungu wanaohisi wahusika unaongezeka kwa

kiwango cha juu kwa vile wanajitenga na familia ya Ngoma na pia wanakosa kupata sehemu ya mirathi kutoka kwa Ngoma. Pia kama jamaa yake, wanahisi kufurahia ushirikiano wao na famila ya Ngoma kama jamaa na wanajamii. Mkufya, ameangazia wahusika tofautitofauti katika riwaya hii wanaotawaliwa na tamaa ya pesa / mali na kisha mambo yao yakawaozea. Mathalan, Asha anaongozwa na uroho wa pesa na kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi baada ya kufanya mapenzi na Ngoma aliyekuwa mgonjwa wa ukimwi (uk. 71). Tamaa ya pesa/ mali inamtenganisha Ngoma na jamaa yake. Hali hii inadhihirika kutelekezwa anapougua katika hospitalini. Wanadai kwamba hawafaidi kwa kukosa kuwasaidia. Wanamkejeli asaidiwe na pesa zake. Hata anapoaga dunia jamaa yake ina haja tu na pesa / mali yake kama magari. Tendo kama hili si la uadilifu hata kidogo. Ili kuhakikisha mambo yanakuwa shwari siku za usoni, wanajamii wanatahadharishwa kutokuwa na tamaa ya pesa / mali. Ni bora watafute mali / pesa zao kwa bidii na njia za halali.

Sawa na Mkufya, Habwe ameshughulikia swala la kutokuwa na tamaa ya pesa / mali kwa mapana. Ametoa mifano ya watu kama Askofu Tonje kutengana na Mhubiri Mango kwa sababu ya tamaa ya pesa, Ametoa taswira ya watu kama Mango kuwekewa sumu katika chakula kwa sababu ya kupigania uongzi katika kanisa. Joshua na Lona wanasawiriwa kama watu wenye tamaa ya mali / pesa. Wanachukua vitu vya kanisa na kuvifanya vyao. Kwa mfano, gari lilotolewa na Amuko. Chifu Owaki ana tamaa ya kupewa ng'ombe katika matanga ya Apondi. Waumini wa kanisa la Apondi wanataka pia ng'ombe, sukari na pesa ili itumike katika mazishi ya Apondi. Tofauti ilioko baina ya kutokuwa na tamaa katika kazi hizi mbili ni kwamba, katika *Paradiso*, wahusika wenye tamaa ya pesa / mali wamehusishwa sana na mambo ya dini.

### 4.1.8 Kuwasaidia Mayatima

Katika utafiti huu, tumelishughulikia neno 'shirika' kama kitu kinachomilikiwa na watu wawili au zaidi. Shirika inapoanzishwa huwa na lengo la kusaidia wanajamii kutatua shida zao za aina aina wanazokumbana nazo ambapo mtu asipojiunga na shirika hujipata anashindwa kutatua matatizo yake. Kwa mfano, namna ya kupata pesa au kupata na kuzitumia pesa. Shirika huwezesha wanajamii kutohisi uzito wa matatizo waliyo nayo, na ndiyo maana wakale walinena, 'umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu'. Kwa vile jamii ya sasa imetawaliwa na tamaa / uroho, kuna umuhimu kwa wao kuanzisha shirika/ mashirika ili yaweze kuwasaidia katika usuluhishaji wa shida wanazokumbana nazo. Muungano huu utawafunza namna ya kukabiliana na athari hasi za uroho na pia utumiaji mbaya wa pesa/ mali bila mpango na hii inakuwa kama kidhibiti cha utumiaji

wa rasilimali. Wanajamii wanatahadharishwa kufuata ushauri wa mashirika ili wapate kufaidi na maisha yao kuimarika. Ndiyo maana Mkufya, ameangazia suala hili la shirika la hazina ya mayatima kwani anaelewa fika kwamba tatizo la ubadhirifu wa mali ya mayatima limekuwa donda dugu/ sugu katika jamii yetu. Ili tatizo hili liweze kutatuliwa na kuwasaidia wanajamii wasiojiweza, lazima tuwe na shirika kama hili. Pia, ili shirika kama hii itimize malengo na matakwa yake, sharti isimamiwe na viongozi waadilifu. Wahusika Asha na Catherine Hastings, wanachukuliwa kuwa ni waadilifu kwani wamenuia kuanzisha shirika ili mali ya mayatima isije kuvamiwa na malalaghai au watu wengine.

Habwe hajaangazia shirika la hazina moja kwa moja. Anachofanya ni kuzungumzia mashirika kwa jumla ambayo yanatekeleza mjibu uliyo sawa na hili. Mashirika kama haya yanasimamiwa na kanisa, hata hivyo yanakabiliwa na shutuma tele ya mapendeleo na kashfa ya ufisadi. Mashirika haya hayawasaidii watu namna inavyokusudiwa na huu si uadilifu (uk.153). Mawazo haya ya ushirikiano yanaweza kuungwa mkono na mchango wa Tolstoy katika nadharia ya maadili kwamba, ‘sanaa iweze jenga udugu miongoni mwa watu bila ubaguzi namna yoyote wa kitabaka’. Watu wanapaswa kushirikiana hasa wakati wa shida ili kutatua matatizo yao. Wasiwabague watu wanyonge. Walio na mali wawasaidie maskini. Wakiishi hivi, yatakuwa ni maadili yanayokubalika.

### 4.1.9 Kukiri Makosa na Kuomba Msamaha

Msamaha ni jambo la hekima kwani laweza kutatua malumbano/ mzozo ambao ungesababisha maovu hasa vita. Kuna umuhimu wa kuomba radhi kwa Mungu vilevile kwa binadamu wenzetu ili kuendeleza uhusiano mwema. Mkufya na Habwe wamewiana katika kushughulikia swala la kuomba msamaha. Teneti ya nadharia ya maadili iliyotuongoza inasema kuwa, ‘fasihi ina wajibu wa kuadilisha jamii’, waandishi hawa wametimiza wajibu wao kwa kuwaeleza wanajamii umuhimu wa kuwa na msamaha na kuomba msamaha ikiwa mtu amekosea kwa nia ya kuregesha uhusiano mwema kwa wanajamii wenzake. Hivyo basi, kupitia riwaya hizi, funzo muhimu unajitokeza ya kwamba, msamaha ni njia ya kipekee/ mwafaka ya kutatua matatizo katika jamii. Msamaha unaweza kutazamwa kwa njia zifuatazo: wanaume kuwaomba wanawake msamaha, wanawake kuwaomba wanaume msamaha, wanawake kuwaomba wanawake wenzao msamaha na wanaume kuwaomba wanaume wenzao msamaha. Msamaha kutoka pande zote unakubaliwa kama tendo la uadilifu.

Katika *Ua la Faraja* swala la msamaha limejitokeza wakati Ngoma anakiri makosa yake kwa Tabu na watoto wake. Anakubali kuwatelekeza na hata kumwambukiza Tabu maradhi yatakayomfisha (uk. 291- 292). Ili msamaha wake usitiliwe shaka, anafanya kuutoa mbele ya Sheikh Rajabu. Juma pia anamwomba babake msamaha na kisha unakubaliwa na babake baada ya Juma, Grace na Omolo kumsihi (uk. 241).

Katika *Paradiso*, Habwe anamsawiri Patricia akiwaomba Lydia na Michael msamaha kwa kuingilia ndoa yao na kutaka kuivuruga. Tena anamwomba Lydia msamaha katika kuchangia mkasa uliopelekea kupelekwa hospitali (uk. 183). Katika riwaya hii tunashuhudia hali ya wanaume kuwaomba wanawake (wanyonge) msamaha na wanakubali. Kuna msamaha kutoka kwa Kyalo. Anamuomba Salome msamaha kwa kumjeruhi ambapo Salome anakubali (uk. 58). Na pia, Michael kuamua kumwomba Lydia msamaha kwamba hatarudia kosa kama hilo kwani lilimletea izari katika marafiki (uk. 169).

Wanajamii wanashauriwa wawe tayari kuomba msamaha wakati wowote wanapokosa. Pia wanahimizwa kukubali msamaha kutoka kwa wengine wanapokosewa. Kuomba na kukubali tendo la msamaha ni uadilifu wa kuleta na kujenga maridhiano miongoni mwa wanajamii. Kama wanavyosema Njogu na Chimerah katika nadharia ya maadili kuhusu tabia ni kwamba, kuna tabia chanya na hasi. Kuomba msamaha itachukuliwa kama tabia chanya na kukosa kuomba msamaha kama tabia hasi. Wanajamii wanafaa kuomba msamaha wanapokosa. Mkufya na Habwe wametoa ushauri huu kwa hali iliyosawa.

### *4.2.* Ushauri Dhidi ya Tamaa na athari zake Katika *Paradiso*

#### 4.2.1 Ushauri / Nasaha

Ushauri unachukuliwa kama maoni anayopewa mtu ili yamsaidie kufikia mapatano fulani na watu wengine. Vilevile neno ‘ushauri’ linaweza kuchukuliwa kama ni maelekezo ya kitaalamu anayopewa mtu ili aweze kufanya kitu/ jambo fulani. Kuna ushauri unaoweza kufaulu na kuboresha kufanya jambo na kuna ushauri unaoweza kuharibu utekelezaji jambo kama ushauri mbaya. Tunafaa kuwa macho ni ushauri gani mzuri na upi mbaya tunaposhauri ama kushauriwa.

Tumeona kuwa ili jambo lolote lifanikiwe ni lazima pawe na ushauri mzuri. Kuna matatizo yanayozuia mafanikio na kudhoofisha nyanja zingine za maisha. Mifano ni tamaa nyingi, kama

inayowakumba Patricia, Michael, Mango, Amuko, Lona, Joshua, Chifu Owaki na washiriki wa Kanisa la Budalangi (uk. 94 ).

Baadhi ya wahusika wameonyesha umuhimu wa ushauri kutoka kwa washauri kama kanisa na wazee wenye hekima kuhusu ndoa na maisha kwa jumla. Kwa mfano, Agripina anashauriwa na Michael kuhusu siri ya nyumba (uk. 99). Naye Mango, wazee wanamshauri kuwaacha wake wengine ili awe mfano mzuri kwa watu wengine kama kiongozi wa kanisa na tena, kufahamu kwamba, ndoa kati ya mke mmoja na mume mmoja ina mapenzi zaidi (uk. 21). Pia, Michael anapotaka kumtumikia Mungu, anatafuta ushauri kutoka kwa Askofu Tonje na baba yake mzazi. Michael anamshauri Amuko kuhusu uwezo wa Mungu kuhusu maisha, kwani Amuko anatawaliwa na tamaa kisha kumtoa ndugu yake kafara. Anataka kuombewa ili maisha yake yasiwe na matatizo (uk. 40- 41). Kwa upande mwingine kuna ushauri mbaya kutoka kwa Joshua na mkewe, Lona. Wanamshauri Michael amuoe Nice ambaye ni kiruka njia (uk. 69).

Chapman (2008: 12), anasema kwamba, ushauri nasaha ni muhimu katika maisha/ ndoa na ushauri humridhisha anapowaona walio katika ndoa aliowashauri wakiboresha ndoa zao. Ni kweli kuwa ushauri unaozaa matunda mema hufurahisha. Ili tusiwe tena na tamaa au kutawaliwa na tamaa ya kupata vitu kwa njia isiyo halali, tunafaa kuwa na washauri wema na tayari kushauriwa.

Hali ya kushauriwa ipo vilevile katika kazi ya Mkufya, *Ua la Faraja* na inatekelezwa na mtalaamu daktari Hans. Anawashauri Omolo, Grace, Tabu, Ngoma na hata Juma kuhusu ugonjwa wa ukimwi na maisha kwa jumla. Vilevile, kuna ushauri unaopotosha kutoka kwa Chiku na Pendo kuwashawishi wateja wajihusishe katika tendo la ngono pasi na kinga ya kutumia kondomu zinazouzwa na Jose. Basi, lililo la maana ni ushauri unaofanikisha maisha ambayo unafaa kuendelezwa miongoni mwa wanajamii, kama anavyosema Hough katika nadharia ya maadili kwamba, ‘jukumu kuu la nadharia hii ni kupendekeza jinsi ya kutatua matatizo ya jamii’. Kwa mujibu huu, ushauri uliotolewa na wahusika, ni lazima utatatue matatizo ya jamii. Tumeoana kuwa ni katika riwaya ya *Paradiso ku*na nasaha nyingi za kupotosha. Kama vile ushauri wa Pendo na Chiku.

### 4.2.2 Matumizi ya Wahusika wa Kitanzia

Mkufya na Habwe wametumia wahusika wa kitanzia kama kielelezo cha kuonya watu walio na tamaa katika jamii. Tumewashughulikia wahusika wanoanguka na pia kufa kama wahusika wakuu

na hata wale si wahusika wakuu huku udhaifu wao ukiwa umesababishwa na tamaa tofautiofauti. Kuna baadhi ya watu ambao huanza kwa kutenda mema na baadaye huishia katika kutenda maovu. Mabaya wanayoshiriki kuyatenda huwaharibia sifa na kufifisha mema wanaotangulia kufanya. Mara nyingi maangamizi yao hutokana na tamaa. Ufifiaji wa aina hii huwakumba mashujaa na wasio mashujaa. Kwa mfano, mhusika Musa anatawaliwa na tamaa ya ngono na kuzini na Salome ambaye ni mkewe Kyalo. Wanavumaniwa, kupigwa na habari ya kushiriki tendo iliyo haramu kusambaa na kumpa soni. Kama kiongozi wa kanisa, hafai kujihusisha na tendo la kufedhehesha kama hili. Anaaibika na kuasi kumtumikia Mungu. Baadaye, anaanzisha biashara na kumkejeli Mungu. Kama adhabu kutoka kwa Maulana, biashara yake inaporomoka na kisha anashikwa na kichaa. Hatima yake inakuwa kugongwa na gari na kuaga dunia (uk.106). Tanzia ya Musa inatufunza kujiepusha kutawaliwa na tamaa. Katika nadharia ya maadili tunaona kwamba, mtu ataiga tabia mzuri endapo atampata yule wa kumwelekeza kutenda mema ikiwa angali mchanga. Tumeona kwamba, Musa alikuwa ni kiongozi wa kanisa aliyestahili kuwaongoza washiriki kutenda mema. Ni bayana kwamba, Joshua aliyemteua kama kiongozi hakumfunza maadili akiwa mchanga kiroho. Hii ni kwa sababu, Joshua pia ni mzinifu na Musa anamuiga. Anapopatikana anatenda kosa inadhihirika kwamba uongozi unamshinda kwani hangewaongoza waumini kutenda mema.

Pia, Lona na Joshua wanatawaliwa na tamaa kisha kumiliki kila kitu kinachonuiwa kuwa cha kanisa. Uroho unawafanya kutenda kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Kama adhabu, wawili hawa wanahusika katika ajali ya barabara na kuionyesha dunia kisogo (uk. 133-134).

Wahusika wengine wanaotawaliwa na tamaa ya kutenda kinyume na matakwa ya kanisa ni Boribori na mkewe (Judy). Wanashikwa na kushtakiwa kwa kosa la kuhusika katika ulanguzi wa madawa ya kulevya. Wanaangamia kwa kushtakiwa na kufungwa jela miaka kumi na kuacha mali waliyopata kwa njia ya haramu (uk. 217-218).

Vilevile, kuna wahusika wa tanzia katika riwaya ya *Ua la Fraja*. Ngoma na Queen kama wahusika wakuu wanafariki kwa sababu ya tamaa ya ngono (uk. 171-172; 293). Wanapokaribia mauti wanaomba msamaha na kuwashauri watu waliobaki kuiga kutenda mema. Tena, wahusika wasaidizi walioonyesha dunia kisogo kwa kushiriki katika tendo la ngono ni pamoja na Pendo na Chiku. Wanajipata katika hali hii kwa sababu ya tamaa. Ili tuweze kuepuka adhabu na vifo vya namna hii, wanajamii wanatahadharishwa kutotawaliwa na tamaa. Waandishi hawa wawili

wamerejelea matukio ya wahusika wa kitanzia kwa namna inayokaribia kuwa sawa. Hata hivyo, Habwe amewafungamanisha wahusika na swala ya dini, naye Mkufya na maisha ya anasa.

### 4.2.3 Ushirikiano Katika Jamii

Ili kuwepo na ushirikiano wa watu ni sharti kuwe na uhusiano na uelewano mwema kati ya wanaohusika. Habwe, anasisitiza umuhimu wa ushirikiano na uhusiano mwema katika utekelezaji wa kila jambo. Sawa na riwaya ya *Ua la Faraja* kuna watu ambao wana ushirikiano na wale wasiokuwa na ushirikiano. Wale hawana ushirikiano wanatawaliwa na tamaa. Hali hii inailetea jamii athari hasi. Kama mfano, Mashaka na wenzake kukosa kushirikiana na jamaa ya Tabu katika mazishi yake. Kwa upande mwingine, wale walio na ushirikiano husuluhisha matatizo yao kwa pamoja na hawakumbwi na mzigo mkubwa. Kwa mfano, ushirikiano katika mazishi ya Queen. Katika riwaya ya *Paradiso*, washiriki wa kanisa la Budalangi Pentecostal Church wana ushirikiano. Wao ni kama jamii katika maombi. Mathalan, Apondi anapougua na kuaga wote wanajumuika kumshughulikia. Mwandishi amesawiri kwamba, ushirikiano hurahisisha mambo wakati kuna hali ya dharura na endapo watu hawana ushirikiano, hulemewa na kujuta ikiwa mabaya yamewafika. Pia, Patricia na mamake wanashirikiana kuwalea watoto wa Patricia. Hali hii inarahisisha mzigo wa malezi na kuufanya kuwa mwepesi. Nao walimu wa shule anakofunza Lydia, wana ushirikiano kwani wanamtembelea na kumjulia hali akiwa anaugua na kulazwa hospitalini. Hivyo basi, ushirikiano ni kitu cha fahari na thamani. Huu ndiyo udugu anaozungumzia Leo Tolstoy katika nadharia ya maadili kwamba, watu wawe na umoja pasi na tabaka. Tumeona kuwa waandishi hawa wamesawiri hali ya 'ushirikiano' kwa kiwango kinachokaribia kuwa sawa.

### 4.2.4 Umuhimu wa Uvumilivu

Mtu anafaa kuwa mvumilivu kwani mvumilivu hula mbivu. Mwanadamu anapaswa kufahamu kwamba katika maisha kuna wakati wa furaha na pia wakati wa huzuni. Anafaa ajitayarishe kukabiliana na changamoto zinazojia nyakati hizi zote bila kujitia mashaka. Mawaidha haya yanapaliliwa na kurutubishwa na mhimili wa nadharia ya maadili iliyotuongoza kufanya utafiti kuwa, 'dhamira ya msanii ni kuandika yanayojenga jamii kimaadili huku akikemea yanayopotosha jamii.' Licha ya changamoto azipatazo ulimwenguni, mwanadamu anapaswa kuwa mvumilivu, kuiga mema na kuepuka / kukemea maovu ili kuendeleza maisha yake.

Katika riwaya hii, Habwe amesimulia visa vya uvumilivu. Ameonyesha namna Lydia anavyovumilia anaposoma hadi anakamilisha masomo na kuolewa kama hajapata uja uzito nje ya ndoa (uk. 110).

Mhusika Kyalo pia anakuwa mvumilivu kuishi na Salome ambaye ni mkewe kwa muda bila kujaliwa kupata mtoto na bila kuoa mke mwingine. Wanavumilia hadi wanapobarikiwa kupata mtoto.

Kwa hakika uvumilivu ni kitu cha thamani kwani Patricia anakosa kuwa mvumilivu na kufanya mapenzi kabla ya ndoa. Tendo hili linamfanya kuzaa watoto kadhaa kabla ya kupata jiko. Hali inayopelekea mama yake mzazi kutoridhishwa na tabia hiyo na kusababisha ugomvi baina yao. Kutokana na mifano hizi, Habwe ameonyesha umuhimu wa watu kuwa wavumilivu kwani uvumilivu huzaa matunda mabivu.

Pia, Mkufya katika riwaya yake amezungumzia uvumilivu. Grace anavumilia kwa kukosa kufanya mapenzi ya mwili hadi anapoolewa na Omolo. Omolo pia anavumilia na kutojihusisha na mapenzi. Sawa na Habwe, Mkufya amewasawiri wale wamekosa kuvumilia na kuharibu maisha yao kwa kukimbilia anasa. Kwa mfano, Ngoma, Asha, Queen, Chiku, Pendo na Msafiri. Riwaya hizi zote zinaonyesha matumizi ya uvumilivu kwa hali inayokaribiana sana. Hii ni kwa sababu ya idadi ya wahusika wametajwa kuwa wavumilivu au kukosa kuwa wavumilivu.

### 4.2.5 Umuhimu wa Maombi/ Sala

Tukiongozwa na nadharia ya maadili tuliona kwamba, wafuasi wa nadharia hii kama vile Plato na Tolstoy, walipendekeza kwamba sanaa ilifaa kuwa ya kidini ili iweze kuwaelekeza watu wawe na tabia njema. Hivyo basi, riwaya hizi za Habwe na Mkufya zinasawiri maadili ya kidini kwa kuwashawishi wahusika fulani kumtegemea Mungu katika kila jambo kupitia maombi kwa vile maombi yanahusishwa na maadili. Katika riwaya ya *Paradiso*, Habwe anarejelea umuhimu wa maombi ya dhati. Amewasawiri wahusika wanaoomba kwa dhati na Mungu akajibu maombi yao. Kwa mfano, Michael anapokuwa mgonjwa kwa muda mrefu, anaomba na Mungu akajibu maombi yake kwa kumponya. Vilevile, anamwombea Amuko anayetoa ndugu yake kafara na pia kutenda tendo la ngono na binti yake aliyekuwa bado ni bikira. Uwezo wa maombi unamwezesha Michael kuyaona haya yote. Mwandishi anadhihirisha uwezo wa maombi kumfanya mtu anayekuwa mfungwa wa pepo baya kufunguliwa na kuwa huru. Michael anapomuombea Amuko, Mungu

anampa uhuru na kuishi maisha mzuri yenye maadili. Pepo baya iliyokuwa imembugudhi kwa muda mrefu usiku kucha inatoweka. Mfano mwingine unaodhihirisha umuhimu wa maombi ni wa Salome ambaye anakosa mwana kwa kipindi kirefu sana. Anaomba, akaamini na kuvumilia. Mungu anamjibu kwa kumjalia kupata mtoto.

Vilevile, mwandishi ameonyesha ubaya wa kutoomba. Kwa mfano, aliyekuwa mtumishi wa Mungu, Musa anapomuasi na kumkejeli Mungu, anapatwa na mabaya kama vile biashara yake kuanguka, anacharukwa na akili na hatimaye kuaga dunia kwa kugongwa na gari barabarani. Kutokana na mifano hizi michache, mwandishi Habwe ameonyesha umuhimu wa mtu kutegemea maombi katika kila jambo na wala asiwe na tamaa.

Naye, Mkufya, ameangazia umuhimu wa maombi. Amefanya hivyo kwa kuwasawiri wahusika wanaotegemea maombi inayoboresha maisha yao na pia wale hawategemei maombi na maisha yao yakadorora na kuenda bendi. Mathalani, Ngoma hapo awali hakujihusisha na maombi. Alizama katika anasa na kuambukizwa virusi vya ukimwi. Aidha, Queen kama Ngoma, hakuomba. Anaogelea katika bahari ya anasa kisha kuambukizwa virusi vya ukimwi, kujuta, kuteseka kwa uchungu wa ugonjwa huo na kisha kujitia kitanzi. Kuna wale wanaoomba na kuvuna mema kutokana na maombi yao. Mathalan, Tabu, Grace na wengineo. Ingawa Tabu mumewe anamwambukiza virusi vya Ukimwi, anapata kuishi kwa muda kiasi kutokana na ushauri wa daktari Hans na pia kujihusisha na maombi. Ni kutokana na maombi Mungu anaweza kumjalia kuishi kwa muda na kisha kuwalea watoto wake hadi wakawa watu wazima na pia kuwasomesha. Kwa upande wa Grace, maombi inamfanya kuwa mvumilivu na kutojihusisha na anasa hadi anapofanikiwa kupata mume wa kumuoa.

Hadi hapo, tunaweza kusema kwamba, maombi yamesawiriwa kama lulu ya tunu kwa maisha ya mwanadamu. Kutokana na maelezo katika riwaya hizi, maombi imetumika kwa kiasi kilicho sawa.

### 4.2.6 Kukiri Makosa na Kuomba Msamaha

Hatua ya kukiri kosa na kuomba msamaha ni uadilifu. Kukiri kwamba umetenda kosa huwa na umuhimu kadha. Kwanza, huondoa shuku / hofu katika jamii kuhusu ni nani anayefanya kosa. Pili, anayetenda kosa hujulikana na nafsi yake huwa huru; hukoma kutatanishwa kisaikolojia. Tatu, humtahadharisha anayetenda kosa kukiri na kuomba msamaha kuwa macho asirudie kufanya kosa kama hilo tena.

Ndoa kadha za wahusika wa riwaya ya *Paradiso* zinaanza kwa furaha. Tukiwarejelea Amulega na Amulega (2009: 31) wanasema kwamba, hii ni hatua ya kwanza ya ndoa kuwa na furaha na raha tele. Hatua ya pili ya ndoa inahusu matatizo ambayo wanandoa wanaanza kuona ila na upungufu wa wenzao. Ni katika hatua hii wanandoa kila mara hukorofiana kwa kuwa hawajaelewana barabara. Tena, binadamu anapokuwa katika jamii, kukosana ni jambo lisilo geni. Anayekosewa huhisi uchungu. Basi, msamaha humwondolea uchungu anayekosewa, naye anayekosa huacha kujuta na kujilaumu.

Baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Paradiso* wanajikakamua kuomba msamaha kama silaha ya kuzinusuru ndoa zao na hata za wenzao. Hawa ni Michael anayemwomba Lydia msamaha kwa kumjeruhi (uk.169) na Patricia anayemwomba Lydia msamaha kwa kupelekea kupigwa na kujeruhiwa na hata nusura kuisambaratisha ndoa yao (uk.183). Kulingana na Chapman (2008: 179), msamaha ni muhimu katika kuiponya ndoa baada ya mzozano kujitokeza. Anasema kuwa kuna sifa mbili muhimu katika msamaha: aliyekosa kuomba msamaha, na kisha aliyekosewa kukubali kumsamehe mkosaji kwa dhati kutoka moyoni mwake.

Hali kama hii ikifanyika, wanandoa na wengine wanayohusika kuzisambaratisha watazirutubisha na kuzistawisha ndoa. Amulega na Amulega (2009:169) wanaafikiana na Chapman (ibid) kwa kusema kwamba, tendo la msamaha husababisha kuongezeka kwa upendo katika wanandoa na pia kuwashawishi kubadili mienendo mibaya. Kwa sababu hii msamaha ni jambo la hekima; ni muhimu kuomba msamaha kwani huleta furaha. Tukirejelea mawazo ya Rousseau (1755) katika nadharia ya maadili, kwamba, 'upendo ni kitu muhimu katika familia na ndiyo msingi wa furaha', tuliweza kuona kuwa bila msamaha si rahisi kuwa na upendo, na ili upendo na furaha ipatikane, ni lazima tuwe na msamaha. Hivyo basi, jamii inahimizwa kuzingatia ushauri wa kuomba msamaha ndiyo ipate kuishi kwa upendo na furaha.

Mkufya, ametoa mfano wa Ngoma anamwomba Tabu msamaha kwa kumwambukiza virusi vya Ukimwi na kuwatelekeza. Tena, Juma anamwomba Ngoma msamaha, kisha anasamehewa. Katika utafiti huu, tumeona kwamba, Habwe ametumia ushauri wa kuomba msamaha sana kuliko Mkufya.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumebaini ushauri kuhusu tamaa na athari zake katika *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Ushauri uliobainishwa unawiana na kutofautiana kwa ukaribu. Kwa mfano, Mkufya amebaini ushauri kuhusu ugonjwa wa ukimwi na pia aina zingine za tamaa. Anasema kwamba, ugonjwa huu upo na unaenezwa sana kupitia tendo la ngono pasi na kinga. Anapendekeza watu wajiepushe kushiriki ngono pasi na kinga tena wakome kuwaambukiza wengine makusudi. Hoja hii imeangaziwa na kupambanuliwa zaidi kwa kutumia vipengele kama: tahadhari kuhusu ugonjwa wa ukimwi, ushirikiano wa watu, kutotamauka na vingineo. Swala la ukimwi unaosababishwa na tamaa lipo tuu katika riwaya ya *Ua la Faraja* lakini katika *Paradiso* halipo. Habwe hajaliangazia. Hata hivyo, uwiano unaopatikana katika kazi hizi ni ubainishiji wa ushauri kuhusu aina aina za tamaa. Kwa mfano, tamaa ya pesa / mali, umuhimu wa ushirikiano, msamaha, na kadhalika. Haya pamoja na mambo mengine mengi yanapambanua ushauri uliyobainishwa kuhusu athari za tamaa. Watu wanahimizwa kushirikiana kupiga vita maovu yanayopatikana katika jamii ili waweze kuishi vizuri.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa hitimisho la utafiti na kuthibitisha malengo yetu. Vilevile, tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye.

### 5.1 Matokeo

Baada ya utafiti, tumebaini kuwa Mkufya na Habwe wamefaulu kushughulikia jinsi dhamira ya tamaa imekuzwa na kuendelezwa. Wametumia wahusika na mbinu za lugha kufanikisha lengo hili. Mkufya ametumia wahusika kama Ngoma, Queen, Asha, Chiku na Pendo kuthibitisha namna aina ya tamaa inavyosababisha matatizo yanayoathiri jamii. Pia, Habwe amewatumia Michael, Mango, Owaki, Amuko na Patricia kuelezea tamaa na uozo wake katika jamii. Aidha, wametumia mbinu za lugha kama vile urudiaji, majazi, ishara na uzungumzi nafsia kuelezea tamaa. Tumebaini kuwa, waandishi hawa wanawiana kwa kiasi namna wametumia mbinu hizi. Hata hivyo, Mkufya ameweza kuelezea matukio mengi ya tamaa kuliko Habwe. Hii inaonyesha tofauti ilioko kati ya riwaya hizi.

Vilevile, tumeweza kubaini aina ya matatizo ya tamaa yanayopatikana katika riwaya hizi ambayo yanawiana na kutofautiana kwa kiwango fulani. Kati ya matatizo tuliyoshughulikia ni ulevi katika jamii, udanganyifu, ulafi, uzinzi na mengineo. Matatizo haya yanapatikana katika jamii ya riwaya zote hizi na yanaiathiri jamii ya riwaya hizi kwa kila hali. Pia, tuliona kuwa matatizo haya yanaweza kuepukwa ikiwa kuna maadili katika jamii hizi.

Mwisho, tulibaini ushauri uliopendekezwa katika *Ua la Faraja* na *Paradiso* namna ya kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na tamaa. Tuligundua kuwa riwaya zote mbili zimependekeza njia kama ushirikiano, kutotamauka, ushauri nasaha na mengineo. Lakini, Habwe hajapendekeza ushauri kuhusu ugonjwa wa Ukimwi kwa vile hajaushughulikia. Zaidi ya haya, riwaya hizi ni kichocheo cha wosia kwa jamii na hivyo basi, ushauri wao unafanana. Aidha, tumeona kuwa wanajamii wanaweza kushinda tamaa ikiwa wanafuata ushauri wa Mkufya na Habwe. Kwa mfano,

wanajamii wanahimizwa waishi kwa upendo, watangamane na kuombana msamaha. Isitoshe, tumegundua kuwa baadhi ya ushauri ambao Mkufya na Habwe wametoa unatofautiana kwa kiwango fulani. Sababu ikiwa ni mazingira na tajriba walizopata kutegemea mazingira walimokulia yaani Mkufya anatoka Tanzania na Habwe anatoka Kenya.

Vilevile, tumeona kwamba riwaya za *Ua la Faraja* na *Paradiso* zinakaribia kufanana kwa namna zinavyoshughulikia swala la tamaa na athari zake katika jamii. Tumepata kujua kwamba; waandishi wa riwaya hizi wanawiana sana namna wanashughulikia maudhui ya tamaa kwa sababu, mwelekeo waliotumia umetawaliwa na utu, dini, utamaduni na maadili katika jamii. Kwa mfano, Mkufya anaashiria kutoridhishwa na Queen kujitoa uhai. Naye Habwe anaonyesha taswira ya huruma namna gari linavyomgonga Musa na kuaga dunia. Hii inaonyesha kwamba waandishi hawa wana utu. Tuligundua kwamba, sababu ya kuwiana kwa Mkufya na Habwe kimaudhui na kimtazamo ni kwamba, wote ni wenyeji wa Afrika Mashariki.

Katika utafiti huu, tulidhamiria kufanya mambo kadha. Kwanza, tumeonyesha namna waandishi wa *Ua la Faraja* na *Paradiso* wameshughulikia tamaa na athari zake katika jamii kwa kuchanganua namna dhamira ya tamaa ilivyokuzwa na kuendelezwa katika riwaya hizi. Pili, tumebaini tamaa na athari zake katika riwaya zote mbili. Tatu, tumebaini ushauri kuhusu tamaa na athari zake. Katika kufanya hivyo tumeelezea sana kuwiana kwa waandishi hawa wawili kuhusu suala la tamaa. Tena, ni hisia yetu kwamba, waandishi hawa wawili wana mwelekeo ulio sawa na pia uhusiano wa karibu tukizingatia jinsi wameshughulikia tamaa. Hata hivyo, wanatofautiana kiasi kuhusu maswala kama ugonjwa. Mkufya amezungumzia Ukimwi, naye Habwe anarejelea magonjwa tofauti kama kuumwa kwa tumbo, kifua na kuendesha, ugonjwa uliyomfisha Apondi.

### 5.2 Muhtasari

Katika tasnifu hii, tumechunguza tamaa na athari zake katika jamii katika riwaya mbili za *Ua la Faraja* na *Paradiso.* Tumetumia nadharia ya maadili katika kufanikisha utafiti huu ambao unatilia mkazo kwamba, lengo kuu la kazi ya fasihi ni kuadilisha wanajamii. Nadharia hii imeweza kutupa mwelekeo ipasavyo kwani inapendekeza jinsi ya kutatua matatizo na migogoro katika jamii na kuijenga jamii iliyo bora, yenye utendaji mema na iliyostawi na kuwa na maelewano.

Tumechanganua jinsi waandishi wameishughulikia maudhui ya tamaa na hatimaye tumebaini chanzo cha kuwiana kwao.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Tunapendekeza kwamba, watafiti wa siku zijazo walinganishe na pia kulinganua tamaa na athari zake katika jamii kwa kujikita katika na kwa kulinganisha na kulinganua tanzu za ushairi na tamthilia, tamthilia na riwaya, tamthilia na hadithi fupi, riwaya na haditi fupi au mashairi na hadithi fupi.

## MAREJELEO


Anyang'o, A. P. (2016) .'Usawiri wa uovu katika Riwaya teule za Ben R. Mtobwa'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.( Haijachapishwa )

Gwako, B. J. (2014) .'Uchanganuzi Linganishi wa swala la maadili kwa vijana wa kiume katika Tenzi mbili: *Siraji* na *Adili'.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijachapishwa )

Habwe, J. (2014) . *Paradiso.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Hagberg, G. L. (2008) . *Arts and Ethical Criticism.* Blackwell Publishers Ltd.

Haji, Z. R. (2019) . 'Kuchunguza Dhamira na fani katika nyimbo bembelezi za watoto: Mifano Katika Makunduchi'.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Huria cha Tanzania. ( Haijachapishwa)

Hough, G. (1999) . *An Essay on Criticism.* Britain: Redwood Press Limited.

Kipkemoi, R. A. (2018) . 'Simulizi za virusi vya Ukimwi / Ukimwi zinavyodhihirika katika Nyimbo za jamii za Kenya Kibaadausasa'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi. ( Haijachapishwa)

Masoud, H. S. (2018) . ' Kutathmini Usawiri wa Mwanamke katika riwaya ya Mfadhili'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania. ( Haijachapishwa)

Mkufya, W.E. (2008) . *Ua la Faraja.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999) . *Research Methods.* Nairobi: Acts.

Muthui, K. E. (2019) . 'Tathmini ya Maudhui katika Tamthilia teule za Kiswhili zinazotahiniwa shule za Upili nchini Kenya: Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016)'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha South Easter n Kenya. (Haijachapishwa)

Ngome, M. D. (2014) . ‘Uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za Harusi za Wadigo na Waswahili’. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu, K. na R. (1999) . *Ufundishaji wa* Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Plato (1960) . *The Republic.* Harmondsworth: Penguin.

Rousseau, J. (1994). *Discource On Origin* of *Inequality.* Frankline, P. (Trans), Oxford: Oxford University Press.

Tanui, S. C. (2014) . ‘Usawiri wa Maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo maadili mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu nyeusi’. Tasnifu ya Uzamili. ChuoKikuu cha Kenyatta. ( Haijachapishwa)

Vaughn, L. (2008). *Doing Ethics Moral Reasoning and Contemporarry issues.* New York: W. W. Norton and Company.

Wamitila, K. (2002) . *Kanzi ya Fasihi*: *Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

__________(2003) . *Kichocheo cha Fasihi*: *Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

__________(2003) . *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia.* Nairobi Focus Publication.